

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 26 Juni, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba katika Kanuni yetu ya 38 siku ya Alhamisi ni siku ya maswali kwa Waziri Mkuu. Lakini tuliiitengua ile Kanuni kutokana na kwamba Waziri Mkuu ndiye mwenye hotuba tunayoendelea kujadili hivi leo na atajibu kesho. Kwa hiyo, tunaendelea na utenguzi wa ile Kanuni mpaka tutakapokuja siku nyingine. Katibu endelea na *Order Paper!*

MASWALI NA MAJIBU

Na. 104

Ukarabati wa Barabara ya Kamena-Msasa-Ibondo-Katoro

MHE. KABUZI F. RWILOMBA aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Kamena-Nyabulolo-Gengesaba-Busanda-Msasa-Ibondo-Katoro ni muhimu sana kwa Maendeleo ya jimbo la Busanda kwani pia ni kiungo kikuu cha Wilaya ya Chato, Geita na Wilaya za Shinyanga na kuwa barabara hiyo inapita kwenye maeneo ya uzalishaji wa pamba, mahindi, mihogo, mtama, mpunga, maharage na mazao ya ng'ombe.

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha ili kukamilisha ukarabati wa barabara hiyo?

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina mtandao mkubwa wa barabara wenyе jumla ya km. 963. Naomba kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa barabara ya Kamena-Nyabulolo-Gengesaba-Busanda-Msasa-Ibondo-Katoro ni muhimu sana kwa Maendeleo ya jimbo la Busanda kwani ni kiungo kikuu cha Wilaya ya Chato, Geita na Wilaya ya Shinyanga na kwamba barabara hii inapita kwenye maeneo ya uzalishaji wa pamba, mahindi, mihogo, mtama, maharage na mazao ya ng'ombe. Barabara hii ina jumla ya urefu wa km. 52.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa mwaka wa fedha 2007/2008 Halmashauri ya Wilaya ya Geita ilitengewa bajeti yenye shilingi milioni 769.13 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye jumla ya urefu wa km. 760 na kuimarisha daraja la Mkoba na ujenzi wa makalvati.

Hata hivyo kwa mwaka huo wa fedha wa 2007/2008 Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwenye mpango wake wa barabara haikutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Halmashauri ya Wilaya ya Geita imetengewa jumla ya shilingi milioni 794 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa km. 643. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 24.3 ni kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi (*spot improvement*) kwa barabara ya Katoro-Ibondo-Gengesaba km 11.2 na shilingi milioni 6 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya mara kwa mara (*routine maintenance*) kwenye sehemu ya Nyarwanzanja-Nyakamwaga kwenye eneo la (Kamena-Gengesaba) kati ya shilingi milioni 18.8 zilizoombwa na Halmashauri. Ni imani ya Serikali kwamba fedha hizo zitasaidia kupunguza matatizo ya barabara yaliyoelezwa.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa umahiri wake na wepesi wa kujibu maswali japokuwa amekaa kwa muda mfupi. (*Makofit*)

Ni kweli kwamba zililetwa milioni 700 katika Wilaya ya Geita. Lakini kwa barabara zilizopo Wilaya ya Geita na hali zilizonayo hizo fedha hazikuweza kutosheleza, zilifanya kazi robo tu, hazitosh, na ukubwa wa Geita unahitaji fedha nyingi zaidi karibu ya bilioni 2. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufikiria upya ya fedha hizo wanazozileta ambazo ni chache ambazo zinashindwa kwenda kwenye barabara zingine ? Swali la pili. Barabara hii kwa sababu ya urefu wake na hali iliyokuwa nayo na barabara hii zamani ilikuwa ndiyo barabara kuu ya kutoka Kagera kuelekea Shinyanga ikipitia Geita na tumekwishiombea kwenye Wizara kwamba ipandishwe, tumeshafanya vikao vyote katika Wilaya

NAIBU SPIKA: Uliza swali, tafadhali uliza swali.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Ni lini sasa hii barabara itapandishwa daraja ili ipunguze mzigzo kwa Wilaya ya Geita?

NAIBU SPIKA: Ni hilo tu Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyozungumza sasa hivi hapa tuko kwenye Bajeti na hapa nimetaja kiasi cha shilingi milioni 760 ambazo ziko katika *projection* na katika maombi ambayo yataletwa hapa na ambayo kesho Mheshimiwa Waziri Mkuu atawaomba kwamba mpitishe hapa. Anazungumza Mheshimiwa Rwilomba kwamba anavyoiona barabara yenyewe inaweza ikahitaji hata bilioni 2. Ni ukweli usiopingika kwamba Bajeti inapoonyesha tu uwezo ulionao kimapato na matumizi yako na kusema kwamba sasa naweza nikasema hapa kwa niaba ya Serikali kwamba hela hizo zitapatikana nitakuwa simtendei haki yeye mwenyewe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, *microphone* !

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Ninachowea kusema hapa Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba wao wanatakiwa sasa waangalie jinsi ambavyo hizi zilizotengwa zinaweza zikawekwa katika vipaumbele walivyojiwekea kama Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Rwilomba aangalie yeye na wenzake ni kwa namna gani wanaweza wakazitumia hizi hela zilizotengwa kidogo kwa ajili ya kazi hiyo.

Lakini la pili anazungumzia kuhusu suala la kupandisha gredi barabara hii ambayo nimezungumzia hapa. Kwanza mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Rwilomba jinsi anavyoihangakia barabara hii na barabara zake zilizoko katika Jimbo lake la Busanda. Ninachowea kusema tu ni kwamba utaratibu uliowekwa na Serikali ni kwamba wao wenyewe katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita wanatakiwa wakae, wazungumze kuhusu barabara hii kupandishwa daraja. Wakitoka pale wanaipeleka kwenye kitu kinachoitwa Bodi ya Barabara ya Mkoa na baada ya kupeleka katika Bodi ya Barabara ya Mkoa wanaipeleka kwenye kitu kinachoitwa Kamati ya Ushauri ya Mkoa yaani *The Regional Consultative Committee* ambayo ile ikishapitisha sasa ndiyo inapelekwa katika Mamlaka zinazohusika. Naamini umuhimu ulioelezwa hapa nina hakika kabisa kwmaba Mamlaka zinazohusika zitakubaliana na rai inayoletwa hapa ya kupandisha daraja barabara hii iliyozungumzwa.

MHE. ERNEST G. MABINA: Nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa pesa hizi zinazotolewa kama milioni 700 ambazo zimetolewa Wilayani Geita huwa zinachelewa sana kutolewa hasa tunapopitisha kwenye bajeti na kupelekeza zinapofika mawilayani unakuta kwamba zinakuja kwenye mwezi wa kwanza kwenye mwaka unaofuata. Hivyo kusababisha pesa nyingi katika Halmashauri karibu zote huwa zinarudi za matengenezo ya barabara. Je,

Serikali inasemaje ili kuweza kuwahisha tunapopitisha hapa tu basi pesa zinapelekwa katika wilaya zetu. Serikali inasemaje katika suala hili ? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika,

NAIBU SPIKA: Kifupi tu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Ndiyo nitaeleza kwa kifupi. Tutakachofanya sisi kama Serikali na maelekezo yameshatolewa tayari na wala sio hela hizi tu zinazozungumzwa za barabara. Hata zile za *Qwick Wins* hata za MMES na MMEM zote mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba hela hizi zinakwenda haraka iwezekanavyo ili ziweze kufanya kazi hizi za maendeleo kama ilivyotarajiwa. (*Makofi*)

Na. 105

Jiji la Tanga kugawanywa katika Wilaya mbili

MHE. NURU AWADHI BAFADHILI aliuliza:-

Kwa kuwa Tanga ni Jiji kama yalivyo Majiji ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha na kwa kuwa Majiji hayo yana Wilaya zaidi ya moja kama vile Jiji la Mwanza lenye Wilaya mbili na Kata ishirini na moja:-

Je, ni lini Jiji la Tanga lenye Kata ishirini na nne litagawanywa katika Wilaya mbili ili kuboresha huduma za kiutawala kwa wananchi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kuweka sawa maelezo yake ya utangulizi kwa sahihisho kwamba Arusha sio Jiji bali ni Halmashauri ya Manispaa. Tanzania ina Majiji manne tu, ambayo ni Dar es Salaam, Tanga, Mbeya na Mwanza. Baada ya sahihisho hilo naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika kugawanywa kwa eneo la kiutawala hufanyika kwa mujibu wa taratibu zilizopo na kwa kuzingatia vigezo vya uanzishaji wa maeneo mapya ya kiutawala. Utaratibu unaelekeza kwamba wananchi kupitia wawakilishi wao kwenye Baraza la Madiwani hupendekeza mgawanyiko huo baada ya kuona haja ya kufanya hivyo. Kisha mapendekezo yao hupelekwa kwenye Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*) kwa ushauri kama upo. Kisha mapendekezo hayo huletwaa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambapo hupitiwa na baadaye Mheshimiwa Rais hupewa ushauri wa kuhusu mapendekezo ya mgawanyiko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika mambo ya kuzingatiwa katika hatua zake hizo na hususani kugawanya na kuanzisha Wilaya mpya ni haya yafuatayo:-

- (i) Eneo la Wilaya mpya na inayobaki baada ya mgawanyo kila moja lisipungue kilomita za mraba 5000.
- (ii) Idadi ya watu wa Wilaya mpya na inayobaki baada ya mgawanyo wasipungue 250,000.
- (iii) Idadi ya Tarafa kwa Wilaya mpya na inayobaki baada ya mgawanyo kila moja zisipungue 5, Kata 15 na Vijiji 50.
- (iv) Uthibitisho kuwa jiografia ya eneo husika inasababisha utoaji wa huduma kuwa mgumu.
- (v) Uwezo wa Serikali na utayari wa wananchi kuchangia uanzishwaji wa Wilaya mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika nitumie fursa hii kueleza kwa ufupi kwamba Jiji la Tanga lina kilometra za mraba 600. Kati ya hizo kilometra za mraba 548 ni nchi kavu na kilometra za mraba 52 ni eneo la maji. Jiji hili lina kata 24 na kwa mujibu wa takwimu za makadirio ya mwaka 2007, lina jumla ya watu 265,549. Kwa msingi wa maelezo haya na kwa kuzingatia taratibu zilizopo katika mchakato wa kugawa maeneo ya kiutawala sambamba na vigezo vyake kama nilivytangulia kufafanua. Jiji la Tanga litagawanywa katika Wilaya mbili mara tu litakapokidhi vigezo nilivyovitaja. Inawezekana zipo hoja na maelezo maalum ya kuhitaji Wilaya mbili. Hata hivyo, kama hivyo ndivyo, Ofisi yangu inashauri kwamba hoja za mahitaji hayo zijengwe vizuri na kuziwasilisha kama utaratibu unavyohitaji ili nguvu zake (*strengths*) zionekane na kutathminiwa kabla ya kuchukua uamzi wa kuligawa jiji hilo.

MHE. NURU AWADHI BAFADHILI: Ahsante nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Hata kama vigezo havikukidhi, je iwapo watu wetu wanazidi kuongezeka na huduma zinakuwa zinawafikia katika hali ngumu. Je, Serikali haioni sasa huu ni wakati muafaka Tanga iwe na Wilaya ili iweze kukidhi kuhudumia wananchi wake?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, hili ambalo analizungumzia, anazungumzia kwamba watu wanaendelea kuzaliwa na watu wanazidi kuongezeka na kwamba hatimaye utafikiri idadi hii ambayo inazungumzwa hapa na katika majibu haya moja ya vigezo ambavyo nimevielezea hapa ni kwamba kama kunaonekana kwamba kuna tatizo la utoaji wa huduma katika eneo linalohusika basi hii itakuwa ni sehemu ya hoja ambayo itakuwa inajengwa kwa ajili ya kuomba hiyo Wilaya mpya ili huduma hizo ziweze kufika kwa wananchi.

Lakini haiondoi ukweli kwamba utaratibu ambao nimeueleza hapa utabidi uzingatiwe ili kuona sasa baada ya hoja ile uwezekano wa kufanya hivyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Killimbah swali la nyongeza kwa kifupi.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa huu mgawanyo wa Wilaya si kwa Wilaya tu bali hata Kata na Vijiji. Sisi huko Iramba tu tayari tulishawasilisha maombi kuhusiana na suala la mgawanyo wa baadhi ya Kata na Vijiji kama vile vya Songambele ili kiwe vijiji viwili na navinukuu. Kijiji cha Kizozo ili kiwe kijiji kingine cha Msamsao. Maombi haya yapo Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, tayari kwa takriban miaka miwili iliyopita. Je, vile vigezo ambavyo tayari tulishatimiza na tukaleta maombi hayo, hivi vijiji sasa mtaviruhusu ili viwe vijiji kamili ?

NAIBU SPIKA: Mwenzako alikuwa anazungumzia Jiji. Wewe unazungumzia vijiji. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, tutakapokuwa tuna-*wind up* hapa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tutatoa majibu hapa kuhusu swali hili ambalo Mheshimiwa Killimbah analizungumzia na tunazingatia hili kwa sababu tunajua kwamba sasa tunakwenda kwenye uchaguzi huu wa vijiji kwa hiyo tutahakikisha kwamba kwa kweli yale maombi ambayo yameletwa na yanakidhi vigezo vile vilivyowekwa yanatekelezwa kama yalivyoombwa.

Na. 106

Ofisi za Uhamiaji, Forodha na Polisi

MHE. MOHAMED S. SINANI alijibu:-

Kwa kuwa daraja la umoja ambalo linajengwa sasa kwenye Mto Ruvuma, linatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2009 na kuunganisha nchi yetu na Msumbiji:-

- (a) Je, Serikali inajiandaa vipi kwa majengo na vifaa vitakavyohitajika kwa Ofisi za Uhamiaji, Forodha, Polisi na kadhalika ?
- (b) Je, kwa upande wa wenzetu wa Msumbiji nao wanajiandaaje?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika katika mkutano wa pamoja na wenzetu wa Msumbiji uliofanyika mwaka 2007 ilikubaliwa kwamba kila Taasisi ya Serikali inayopaswa

kuwepo eneo la mpakani ihakikishe inajengwa Ofisi zake. Hivyo, Serikali kuititia Bajeti yake ya 2008/2009 inaona uwezekano wa kujenga jengo la pamoja katika eneo la Mtambaswala/Masuguru ambalo litakuwa na Ofisi za Forodha, Uhamiaji na Polisi pamoja na vitendea kazi muhimu ili kuhakikisha huduma katika eneo la mpaka zinapatikana kabla ya daraja hilo kuanza kutumika rasmi mapema mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa mujibu wa upande wa Serikali ya Msumbiji, hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi zote muhimu. Aidha kwa zile Idara na Taasisi ambazo tayari zimepata fedha ujenzi wa Ofisi hizo unatarajiwa kuanza wakati wowote kuanzia sasa katika eneo la Negomane.

Mheshimiwa Naibu Spika lengo la Serikali zote mbili ni kuona kwamba Ofisi zote muhimu kwa upande wa Msumbiji na Tanzania zinakamilika kabla ya daraja hilo kuanza kutumika rasmi.

MHE. MOHAMED S. SINANI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa majengo yaliyopo katika mipaka yetu hayana hadhi ukilinganisha na yale yaliyopo katika nchi ambazo tunapakana nazo. Yaani majengo mengine ya nyasi, Ofisi zingine zimo katika konteina. Je, Serikali itajenga majengo mengine ambayo yanaendana na karne yetu hii?

Swali la pili, je haya majengo ambayo yatajengwa katika mpaka wa Mtambaswala yatakuwa yanafanana na haya au yatakuwa ni ya aina yenye hadhi kubwa? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majengo ama uhadhi wa majengo ambayo Serikali inatarajia kujenga hapana shaka ni azma ya Serikali kwamba majengo ambayo tutajenga yatakwenda na wakati na ninadhani hizi jitihada zinafanyika hata katika mipaka mingine ya hapa Tanzania. Kwa hiyo, ningependa kumjibu kwa kifupi kwamba hilo kwa kweli litafanyika kwa sababu daraja lenyewe liko katika utaratibu wa kukamilishwa.

Kuhusu swali la pili, kama majengo yatafanana na yale ambayo wenzetu wanajenga. Hakika *plan* ni moja na mfadhili ni huyo huyo *European Union* na pesa ambazo tumezipata na hapana shaka tutajenga majengo ambayo kidogo yanafanana.

Lakini bado niseme kwamba kila nchi itakuwa bado ina uhuru wa kuongeza vitu vingine ambavyo wanataka kuviweka. Hii najibu kwa kuzingatia kwamba Mheshimiwa Sinani ni mtaalam aliyebolea katika mambo ya ukontraktu wa majengo. Kwa hiyo, ndio maana anauliza masuala ya hadhi lakini nataka nimhakikishie kwamba hilo linazingatiwa na litafanyika. Ahsante sana.

MHE. YONO S. KEVELA (K.n.y. MHE. RICHARD S. NYAULAWA)
aliuliza:-

Kwa kuwa vituo/vizuizi nya askari wa barabarani ni vingi na vinaleta kero kubwa kwa usafirishaji kwa wafanyabiashara kwa mfano, barabara kuu ya kutoka Dar es Salaam – Tunduma ina vituo takriban 25 vinavyohudumiwa na askari iwa barabarani wasiopungua 100 kwa wastani wa askari wanne kwa kila kituo na kwa kuwa, zipo kero nyingine zinazoambatana na hiyo kama vituo vingine kuwa mbali na miji/vijiji ambako hakuna huduma za choo, maji wala chakula.

Ucheleweshwaji wa ukaguzi wa magari ya mizigo kwenye vituo kwa takriban saa 8, kutokana na kuwepo kwa mazingira ya rushwa ; mabasi ya abiria kwenda mwendo wa kasi kupita kiasi na kusababisha ajali na vifo nya watu, kuwepo kwa wahalifu mbalimbali wengine wakiwa na silaha kusafiri kwenye mabasi, na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji kutokana na kupoteza muda mrefu kwenye kituo, rushwa na usafirishaji kutokuwa na tija:-(a) Je, Serikali haiwezi kupunguza vituo hivyo ili kupunguza gharama kwa kuwa na ripoti ya ukaguzi inayoweza kutathminia na vituo vinavyofuata?

(b) Je, kwa nini Serikali isiweke matuta barabarani sehemu ya kuingia/kutoka kijiji kimoja hadi kingine ili kupunguza askari wa barabarani na kuondoa mazingira ya rushwa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika vizuizi nya barabarani huwekwa kwa amri ya Kamanda wa Polisi wa Mkao kwa mujibu wa Kanuni za Huduma za Jeshi la Polisi (*Police General Orders (P.G.O.)*) Na. 316 kwa madhumuni na malengo yafuatayo:-

(i) Kuzuia kuingia kwa wahalifu katika Wilaya au Mkao.

(ii) Kuzuia kutoroka kwa watuhumi wa wanaotafutwa na wafungwa walitoroka magerezani na watu wengine wavunjao Sheria za nchi.

(iii) Kuzuia uingiaji wa silaha haramu, madawa ya kulevyta, wahamiaji haramu na kadhalika.

(iv) Kuzuia kutendeka kwa makosa ya usalama barabarani ikiwemo mwendo wa kasi wa magari, magari mabovu, madereva wasio na leseni, kubaini Madereva wanaoendesha magari Wakiwa wamelewa na watumiaji wote wa barabara ambao wanakiuka matumizi sahihi ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika katika barabara ya Dar es Salaam – Tunduma kuna vituo vidogo nya kudumu nya usalama barabarani kumi na moja (11). Kamanda wa Polisi wa Mkoa ana uwezo pia wa kuweka vituo vidogo vinavyohamahama (*movable check points*) kadri atakavyoona inafaa kwa madhumuni niliyoleza hapo juu. Kila kituo kina wastani wa idadi ya askari watatu (3) mpaka wanne (4) amba majukumu yao ni kupima mwendo kasi wa gari, kiwango cha ulevi cha dereva, mwandishi wa *notification* na mkaguzi wa gari. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Naibu Spika kwa mujibu wa Sheria ya Barabara, barabara kuu hazitakiwi kuwekwa matuta kwa sababu mwendo wa chini unaotakiwa kutembea katika barabara hizo ni kilomita 80 kwa saa. Hivyo uwepo wa matuta barabarani unawenza kusababisha ajali na safari kuchukua muda mrefu zaidi. Alama za barabarani (*Traffic signs*) ndizo zinazotakiwa kuwekwa ili kuongoza mwendo wa gari kwa kumtahadharisha dereva maeneo ya miji, madaraja, watembea kwa miguu na sehemu ya kuvuka wanyama na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi litaendelea kuwachukulia hatua kali askari wote watakaobainika kutenda kazi zao kinyume na maadili mema ya Jeshi la Polisi.

MHE. YONO S. KEVELA: Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Spika, wakati anajibu swalii la msingi Naibu Waziri alikuwa anazungumzia kuhusu suala la matuta na uzoefu unaonyesha kwamba matuta huwa yanakinga sehemu kubwa ya ajali.

Nina mfano hai pale hai, sehemu ya Halali watu wanagongwa mara kwa mara katika Jimbo la Njombe Magharibi pale kati ya Mbeya na Iringa matuta hayapo.

Naomba Serikali inieleze kinagaubaga, huoni kitendo cha kuweka matuta pale wanahatarisha usalama? Hili la kwanza.

La pili nichukue nafasi ya pekee kushukuru kituo cha Polisi ambacho wameniletea Jimboni kwangu pale Illembula. Je, ni lini wataongeza idadi ya askari wanawake? (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Lazima uwe na sababu za kuleta askari wanawake. Ni sababu zippi? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi sijakana kwamba matuta hayana umuhimu na tumesema yanakuwepo mahala ambapo yanahitajika kuwepo.

Lakini dai la kusema kwamba yawepo katika *highways* hizi barabara ambazo zinakwenda masafa marefu kwa kweli hilo ni suala ambalo haliwezekani na ni suala ambalo halitendeki kwa sheria za kimataifa. Isipokuwa pahala ambapo karibu na miji na mahala ambapo kwa kweli ziko hatari ambazo ni dhahiri basi Serikali huchukua za makusudi kuhakikisha kwamba matuta kama hayo yanakuwepo.

Kuhusu eneo sasa alilolitaja, hilo kalitaja na nadhani wataalam wetu watatazama na kuona kama nini la kufanya kuhusu hiyo rai aliyoiwasilisha Mheshimiwa Mbunge Yono Kevela.

Kuhusu kituo cha Polisi ambacho kimejengwa katika kijiji chake cha Ilembula. Ningependa kumjibu Mbunge Yono kwamba hilo suala ambalo tutalifikisha kwa Makamanda ambao wanahuksika na kuwa-*allocate* hawa katika kazi na wataona kama upo umuhimu wa kuwepo askari wanawake au la. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri. Tafadhali kwanza Mheshimiwa Ndugai ukae kwanza.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa majibu ya ziada na baada ya kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kuhusiana na vivuko au matuta kwenye barabara zinapoingia kwenye vijiji au miji.

Serikali baada ya kutambua kero kubwa ya wananchi na hiki kimekuwa kilio kikubwa cha vifo ambavyo vinatokea kwenye barabara hizi kuu zinazoingia katika miji na katika vijiji. Imetambua kikwazo ambacho tunacho katika Sheria ambayo tumeipitisha Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007.

Lakini pamoa na kikwazo hicho Serikali sasa hivi iko katika taratibu ya kuangalia kwa namna ya dharura ili iweze kuondosha kasoro hii kwa kuweza kuweka matuta katika kila maeneo yale ambayo yanahatarisha maisha ya binadamu.

Kwa hiyo Serikali inalishughulikia sasahivi na tutahakikisha tunalifanya kwa umuhimu wake kwa sababu maisha ya binadamu na maisha ya wananchi Watanzania ni muhimu zaidi kuliko jambo lingine. Ahsante sana. (*Makofi*).

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swalii dogo moja la nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, kwa majibu yake mazuri kwa swalii la Mheshimiwa Nyaulawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii langu linahusiana na vituo barabarani. Mheshimiwa Nyaulawa kwenye swalii lake la msingi ametoa mfano wa kutoka Tunduma hadi Dar-es-Salaam, vituo karibu 20 njiani na ukitoka Mwanza kuja Dar-es-Salaam, sijui kuna vituo vingapi vya Polisi. Nakubaliana nawe kwa maelezo ya kiusalama kwamba ni kwanini vituo viwe vingi. Lakini nauliza je, kwa sababu za kibiashara na kwasababu za

kiuchumi hatuoni kwamba kwa biashara ya ndani ya nchi na hata kwa nchi jirani kama za Burundi, Rwanda, tunaifanya nchi yetu isiweze kushindana na Kenya na Uganda kibashara kwa kuweka vituo vingi sana vya polisi njiani, kiasi cha kuwa ni kero sasa? (*Makofi*).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mawaziri kama wanataka kujibu wawe wanajibu tu. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ningependa nimjibu Mheshimiwa Ndugai, Mwenyekiti wetu, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema kwamba labda niweke *record straight*, kwasababu Ndugu Nyaulawa katika swali lake anasema kutoka Dar-es-Salaam mpaka Tunduma kuna vituo, *Road Blocks* 25. nasikitika kusema kwamba si kweli, kwasababu vituo vilivyopo ni vituo 11 tu. Na hii ni kwa idadi ya hesabu tulizokwanazo na ndivyo ilivyo. Kwa hiyo sio 25 ni 11, hiyo naomba nilieleze sikutaka kulijibu kwenye jibu langu la msingi kwa njia hiyo. Lakini la pili ni kwamba kweli kuna biashara na biashara ni kitu muhimu na nchi husika kama alivyosema Mheshimiwa Ndugai. Lakini pia na sisi tunazingatia kwamba yapo masuala ya usalama wa Taifa letu kwasababu tumekabiliwa na hii ni kweli kabisa, wimbi la wavamizi, wahamiaji haramu na watu amba wanakuja katika nchi.

Nasikitika kusema nchi alizozitaja ni nchi ambazo kwa kweli wamekuwepo watu wengi amba wanakuja katika maeneo mengi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyoo inabidi tu-*balance* kati ya usalama wa watu wetu na mali zao na pia *facilitation* ya wafanyabiashara wa nchi zetu. Lakini ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Ndugu Mbunge Ndugai, kwamba rai aliyoisema ni muhimu kwamba pawepo na *balance* kati ya ku-*facilitate* biashara ili wafanyabiashara wetu waende vizuri lakini pia tusiweze ku-*compromise* mambo muhimu ambayo yanahusu usalama wa nchi yetu na raiya wake, ahsante sana.

Na. 108

Ongezeko la Vitendo Viovu Nchini

MHE. MARTHA J. UMBULA aliuliza:-

Kwa kuwa, vitendo vya ubakaji vinashamiri sana ndani ya jamii yetu licha ya kupigiwa kelele na wananchi pamoja na Serikali; na kwa kuwa, watuhumiwa hutolewa magerezani kwa dhamana jambo linaloweza kuwapa fursa ya kuviendeleza vitendo hivyo au kujaribu kuharibu ushahidi hali inayosababisha hata mauaji:-

(a) Kwa kuendelea kuwepo kwa vitendo hivyo kwa wingi hapa nchini. Je, Serikali haioni kuwa imeshindwa kuvidhibiti na kusababisha hofu kwa jamii?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa, hivi sasa baadhi ya wabakaji wanabaka na kuua ili kupoteza ushahidi kama ilivyotokea Haydom tukio ambalo lilitokea Hydom Wilayani Mbulu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijashindwa kudhibiti matukio ya ubakaji katika jamii. Aidha Serikali inafahamu kuwa baadhi ya watuhumiwa hutenda makosa ya mauaji baada ya kubaka. Tukio lililotokea katika Kijiji cha Hydom Wilayani Mbulu ni moja kati ya matukio ya namna hiyo. Hata hivyo Serikali, Wananchi, Taasisi na Wadau imekuwa inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika kudhibiti makosa hayo. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(a) Mmomonyoko wa maadili katika jamii umechangia sana kuongezeka kwa vitendo vya ubakaji.

(b) Kukuwa kwa teknolojia ya mawasiliano ambapo kumekuwepo maonyesho ya picha za ngono katika kumbi za video, kumbi za usiku za starehe, *Casino* na *Night Clubs*, na programu Fulani katika *TV*, simu za mikononi, matangazo na mambo mengine mengi pamoja na majarida ambayo yanatolewa ambayo yanapotosha yanaipotosha jamii.

(c) Utumiaji wa madawa ya kulevyo kwa vijana imekuwa ni kichocheo kufanya vitendo vya uhalifu ikiwemo ubakaji.

(d) Kushamiri kwa imani ya ushirikina mionganii mwa wanajamii ambapo baadhi ya waganga wa kienyeji wamekuwa wakitoa masharti kuwa endapo utambaka mtoto mdogo utaweza kuwa tajiri na kujipatia mali nyingi au utaweza kujiepusha na majanga mbalimbali katika maisha.

(e) Wazazi wengi hawako karibu na watoto wao hivyo watoto kukosa uangalizi wa karibu ikiwemo elimu juu ya maisha yao ya kila siku na tabia mbalimbali katika jamii na hivyo kusababisha watu walio karibu na watoto hao kutumia nafasi hiyo kuwabaka na kuwalawiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikishirikiana na vyombo vingine vya nchi na wadau mbalimbali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali kukabiliana na vitendo viovu vya ubakaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kuwapa pole wahanga na ndugu wa wahanga wa matukio haya ya ubakaji. Aidha, naomba wananchi wote waelewe kwamba mafanikio ya Jeshi la Polisi katika kupambana na uhalifu wa aina zote ikiwemo ubakaji yanategemea sana ushirikiano wetu kwao.

Hivyo tudumishe ushirikiano huo kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu kwa vyombo nya dola na wanajamii tubadilike kwa kujiepusha na vitendo ambavyo vinachangia mmonyoko wa maadili katika jamii na imani za kishirikiana. Ahsante.

MHE. MARTHA J. UMBULA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza napenda kumpongeza na kumshukuru Naibu Waziri, kwa majibu yake ya kina kuhusu swali hili. Lakini pamoja na hayo nina swali dogo la nyongeza.

Unapoweka mikakati ya kutatua jambo Fulani lakini lile tatizo likawa halitatuliki, inabidi urudi mezani na kuweka mikakati mipy kama utakuwa hujakata tama. Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kutunga sheria mpya kwasababu inaelekea hii iliyokuwepo haikidhi kutatua jambo lililopa, ahsante sana (*Makofi*).

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Martha Umbulla, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati tuliyonayo mpaka sasa hivi siwezi kusema kwamba imeshindwa au haikuweza kuzaa matunda. Suala la ubakaji nisingependa kwenda katika undani wa maeleo kwasababu ni kitu ambacho kinafahamika, linategemea sanasana na watu kujitokeza kutoa taarifa. Lakini kumekuwa na matatizo hapa nikiri, niseme kwamba watu ambao wamekuwa wanaweza kutupa taarifa ambao wanaweza kuwa ni mashahidi katika matukio mbalimbali wamekuwa waoga kujitokeza, wamekuwa wagumu kushirikiana na Polisi ama vyombo husika katika upelelezi wa kuweza kutafuta *solution* katika matatizo kama haya.

Kwa hiyo, ndio maana nikasema kwamba ni kweli tunaendelea kulitafutia ufumbuzi, lakini nadhani mpaka sasahivi sheria ambayo tunayo si mbaya lakini kubwa ningependa nichukue nafasi hii labda kuwaomba Watanzania na jamii kwamba watusaidie washirikiane na polisi ili tunapozungumzia kwamba tuna polisi jamii ama ulinzi shirikishi kwamba tuwe pamoja na vyombo vinavyohusika katika kutafuta suluhu. Na Serikali imekuwa inajitahidi, Polisi wamekuwa wanajitahidi katika njia mbalimbali kama kutoa zawadi, kama kujaribu kuwashamasisha wananchi waweze kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyu nakubaliana naye kwamba mwendo ni mdogo lakini tukitizama takwimu tumejitetahidi katika kupata *cases* mbalimbali lakini bado tutapenda wananchi wajihusishe zaidi katika kusaidia vyombo nya dola ili tuhakikishe kwamba tunakabiliana na tatizo hili.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naibu Waziri, ameeleza tu kwamba wanaendelea na mikakati lakini hakueleza ni hatua zifi za dhati ambazo Serikali inachukua linaloweza kuwaogopesha hawa wabakaji ambao siku kwa siku wanazidi kuwaumiza watoto wetu, akina mama na hata vijana wetu wa kiume? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwanza kumpongeza Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri sana aliyojatoa katika kujibu swali hili ambalo liko mbele yetu. Ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kusema kwamba sheria yetu ambayo inashughulikia makosa ya kujamiihana ni kati ya sheria nzuri sana ambayo iko katika Bara la Afrika.

Ukiangalia sheria yetu ambayo ipo kwenye vitabu vyetu vya sheria, makosa ya kujamiihana yakitendeka, wale wanaofanya makosa hayo wanajikuta kwamba wanawenza wakatiwa hatiani kwa zaidi ya miaka 30 kwa makosa ya kujamiihana, hatua mabyo haichukuliwi katika nchi nyingi katika Bara la afrika. Na kwa suala la kufuutilia kesi hizi ningependa kusema kwamba kwanza kwa mfano katika kesi hii ambayo imesemwa katika kijiji cha Hydom.

Pamoja na kwamba kwa mara ya kwanza kesi hii ilivyofuutiliwa watuhumiwa waliachiwa kutokana na kutokuwa na ushahidi wa kutosha. Kutokana na kwamba Serikali yetu inathamini maisha ya watu, Serikali iliamua kufuutilia tena hawa watu waliofanya makosa hayo na jarida limefunguliwa upya na watuhumiwa wanafuatailiwa (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwafahamisha wananchi kwamba Serikali haitalala. Pale ambapo matokeo haya yanatokea tutafuutilia hata kama kwa mara ya kwanza ushahidi utakuwa haujakamilika Serikali itaendelea kufuutilia. Na ningependa kuwafahamisha wale ambao wanatenda makosa kama haya kwamba Serikali haitalala, hatakama itachukua miaka 100 hawa watu tutawafuata, tutawapata na tutawatia hatiani (*Makofi*).

Na. 109

Ujenzi wa Shule za Sekondari Ngara

MHE. FEETHAM F. BANYIKWA aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Ngara haina Sekondari ya Serikali yenyewe Kidato cha Tano na Sita:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga shule za aina hiyo katika Wilaya ya Ngara.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufudni, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Feetham Banyikwa, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Ngara ni moja ya Wilaya nchini ambazo hazina Sekondari ya Serikali yenye Kidato cha Tano na Sita. Nia ya Serikali ni kuwa na angalau shule 2 za Sekondari zenye Kidato cha Tano na Sita katika kila Wilaya. Nia yetu ni kupanua nafasi za kudahili wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne na wenye sifa za kuijunga na Kidato cha Tano kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa inatekeleza mpango wa kugeuza shule kongwe za Serikali za bweni zenye Kidato cha Nne kuwa za Kidato cha Tano na Sita. Sambamba na mpango huu, Serikali inahimiza kila halmashauri zikishirikana na wananchi kuanzisha Shule za Sekondari za Kidato cha Tano na Sita. Shule hizo zitimizie masharti yafuatayo:-

(i) Kuwe na vyumba vya madarasa angalau 2 kwa Kidato cha TanojSita; angalau nyumba tatu za walimu wa Kidato cha TanojSita.

(ii) Mabweni ya kutosheleza kukaa wanafunzi wa Kidato cha TanojSita na nyumba ya mlezi wao.(iii)Vyoo angalau matundu 3 (iv)Kuwe na jiko pamoja na bwalo la chakula na samani zake.

(v) Maktaba, maabara kwa masomo ya Sayansi pamoja na huduma za maji, umeme na mawasiliano. Pamoja na michango ya wananchi katika halmashauri husika, Serikali kwa kuititia *MMES* imekuwa ikitoa ruzuku katika ujenzi wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, mabweni, maktaba na vyoo.

Aidha, Serikali hutoa ruzuku kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Halmashauri au Wilaya ambayo itatimiza vigezo viliviyotajwa itatoa taarifa Wizarani ili Wakaguzi wa shule waridhie kufungua madarasa ya Kidato cha 5 na 6 katika shule hiyo.

MHE. FEETHAM F. BANYIKWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu Mazuri ya Naibu Waziri, kwa kuwa, shule za Sekondari za Ngara Mjini na Kabanga, zinakidhi masharti yoote yaliyoorodheshwa kwenye jibu la Naibu Waziri, Je, ni lini Serikali itaridhia shule hizi kuwa za kidato cha tano na kidato cha sita?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundni, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Professor Feetham Banyikwa*, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, amezitaja shule hizo kwa majina kwa kutumia Bunge lako Tukufu, naomba kumuelekeza Mkaguzi Mkuu wa Kanda ya Ziwa, aende maramoja akazifanyie ukaguzi shule hizo halafu atupatie taarifa Wizarani na sisi tutaweza kutoa kibali pale tutakaporidhia. Asante (*Makofi*).

MHE. JACKSON M. MAKWETA: Mheshimiwa Naibu Spika, asante. Kwa kuwa shule za *form five* huchukua wanafunzi kwa kutegemea ufaulu na sio mahali wanapotoka. Na nianyo mifano kwamba shule katika Wilaya yangu zimechukua wanafunzi zaidi ya 80% kutoka nje ya wilaya, kwahiyio kwa kuwa shule hizi si za Wilaya, na hutegemea ufaulu.

Je, isingekuwa uwe mkakati wa Wizara kutekeleza azma hii ya kujenga *form five* na *six?* (*Makofi*).

NAIBU SPIKA: Nilijua swali hilo litaulizwa kwahiyio ndio maana nikampa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri (*Kicheko*).

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundni, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makweta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimthibitishie kwamba katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, *MES II*, tunayo matarajio ya kujenga shule mbili angalao kwa kila Wilaya, Kwa maana ya moja ya wasichana na moja ya wavulana ya kidato cha tano hadi cha sita. Naomba wananchi kwa pamoja tushirikiane kuhakikisha azma hiyo ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili, Kwa pamoja. Nia tunayo na dhamira ya Serikali ni kubwa, naamini tutafanikiwa.

Na. 110

Mpango wa Wanafunzi Kuendelea na Masomo katika Shule Zilizo Ndani ya Kata Zao

MHE. ABDUL J. MAROMBWA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeanzisha *MMES* ili kuhakikisha kuwa, wanafunzi wote wanaofaulu kwa kila Kata wanaendelea na masomo katika shule zilizo ndani ya Kata; na kwa kuwa, utekelezaji wa mpango huo umegubikwa na matatizo kadhaa kama vile

upungufu wa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza, upungufu wa walimu na vifaa vya kujifunzia:-

- (a) Je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya kina ya kuona faida na changamoto zilizopo katika utekelezaji wa mpango huu ili uende vizuri?
- (b) Kwa kuwa Mipango ya Wafadhili kama vile MMEM ilikiuka Sheria ya Elimu (1978) kwa mkondo mmoja mwalimu mmoja na mwalimu mmoja wanafunzi 40 (1:40). Je, Serikali haioni kuwa Mipango hiyo ya Wafadhili inaweza kuathiri Shule zetu za Sekondari zenye wanafunzi wachache?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI aljibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Serikali inafanya tathmini ya kina na kuona faida na changamoto mbalimbali zilizopo katika utekelezaji wa Mpango wa *MMES*. Katika mwaka 2007/2008 Wakaguzi wa Shule walifanya tathmini ya kina kuhusu utekelezaji wa Mpango wa *MMES* na kubainisha mafanikio na changamoto mbalimbali. Aidha, Waratibu wa Sekondari wa kila Wilaya wamekuwa wakifutilia kwa karibu zaidi utekelezaji wa mpango huo. Mafanikio ya mpango huu ni pamoja na ongezeko la Shule za Sekondari ambalo limewezesha idadi kubwa ya wanafunzi wanaohitimu Darasa la Saba kufaulu kujeunga na Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwepo na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa Mpango wa *MMES* ambazo ni pamoja na upungufu wa walimu hasa wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Luga, Uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeongeza nafasi katika Vyuo vya Ualimu vya ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada ili kuweza kuchukua walimu wanafunzi wengi kwa lengo la kupata walimu wa kutosha ili kukidhi mahitaji. Aidha, imekuwa ikipeleka fedha za vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, (b) *MMEM* na *MMES* ni sehemu ya programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu *ESDP* na ni mipango inayowashirikisha wafadhili, wadau na wataalamu mbalimbali kwa makusudi ya kuleta maendeleo ya elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mipango ya *MMEM* na *MMES* imewezesha kuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi na kuzidisha ukubwa wa madarasa hususan katika Shule za Msingi. Hata hivyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Elimu imekuwa ikiweka mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya walimu wanaohitimu katika vyuo mbalimbali.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa na swali moja tu la nyongeza. Kwa

kuwa,l Ilani ya Chama cha Mapinduzi, inataka kila Kata iwe na shule yake ya sekondari na kwa kuwa, kuna baadhi ya Kata hazina ulata wa kujaza wanafunzi wa mkondo mmoja. Je, Serikali inatoa ushauri gani kwa Kata hizo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niseme kwamba kabla ya kujenga shule lazima kuwe na ukaguzi au tuite kwa lugha ya kitaalamu, upembusi yakinifu, hatakama agizo la Ilani liliagiza. Ilani inatamka, angalao shule moja kwa kila Kata, haikutamka lazima shule moja kila Kata. Na mambo ya msingi ya kitaalamu ya kuzingatiwa ni kuona kwamba shule itakayojengwa ijengwe mahali ambapo itawezesha vijiji vingine kuweza kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri ziko baadhi ya shule na katika kujibu hoja za Wabunge, tutatolea mfano wa shule ambayo ilijengwa mahali ambapo haiwezekani miundombinu yoyote, lakini ilikuwa ni kwasababu za kisiasa, Diwani alitaka atambulike, shule ile imejengwa na haitumiki.

Sasa naomba niseme shule hizi zijengwe kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wetu. Maana sisi ni viongozi wa siasa, tunao wataalamu wa elimu, wa uhandisi, nakadhalika. Naomba tuzingatie hayo, tutaepuka kujenga shule na kukosa wanafunzi (*Makofi*).

NAIBU SPIKA: Wengine mutachangia kwenye hotuba ya Waziri. Tunaenda Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, atauliza swali.

Na. 111

Miradi ya Maboresho kwa Wananchi

MHE. SHALLY J. RAYMOND aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kabla ya swali langu kujibiwa naomba kuwe na marekebisho, neno makazini lisomeke kama makazi.

Kwa kuwa, katika Awamu ya kwanza, familia za vijiji zikiwemo familia za mkoa wa Kilimanjaro, zilinufaika sana na Mradi wa Kopa ng'ombe lipa ndama katika kuboresha afya za watoto, makazi na kuongeza kipato:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kurejesha upya programu hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo;:-

Mheshimiwa Naibu Spika, programu ya “Kopa Ng’ombe Lipa Ng’ombe” imekuwa ikitekelezwa hapa nchini chini ya miradi mbalimbali, ikiwemo Mradi wa Mitamba Duniani (*Heifer Project International (HPI)*), Mradi wa kuendeleza wafugaji wadogo wadogo katika mikoa ya Tanga na Kagera, Mradi wa kuendeleza ng’ombe wa maziwa katika Nyanda za Juu Kusini yaani mikoa ya Iringa na Mbeya na miradi iliyofadhiliwa na mashirika na asasi zisizo za kiserikali na vikundi mbalimbali kuanzia miaka ya 80. Mingi ya Miradi hii imekwisha maliza muda wake lakini baadhi ya vikundi katika maeneo have vinaendeleza utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi unaoendelea kutekelezwa hadi sasa ni ule wa Mitamba Duniani ambao unatekelezwa katika mikoa yote nchini. Katika mwaka 2007/2008 kupitia mpango huu, jumla ya mitamba 6,091 imesambazwa hapa nchini, ikiwa ni pamoja na mitamba 31 iliyosambazwa katika Mkoa wa Kilimanjaro. Idadi hii ndogo kwa mkoa wa Kilimanjaro inatokana na ukweli kwamba tayari mkoa huu una ng’ombe wa maziwa wengi, wanaokadirisha kufikia 137,910, aidha, wafugaji wengi hupenda kuhamilisha ng’ombe wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kupata mitamba kutoka kwenye Mpango wa Mitamba Duniani ambao Makao Makuu yake yapo mjini Arusha, ni kwa mwombaji binafsi ama kikundi kuwasilisha maombi kwenye Mpango huo. Mpango huwapatia wafugaji masharti ya namna ya kupokea, kufuga na kusambaza mitamba hiyo kwa wafugaji wenzao.

Napenda kuwashauri wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na wananchi wengine wote nchini ambao wangependa kunufaika na mradi huo kuwasilisha maombi yao kwenye mpango. Mpango kama huu unaweza pia kuanzishwa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Wilaya (*DADPs*) endapo Halmashauri na wafugaji watapenda kuibua miradi ya aina hiyo. Wizara yangu itakuwa tayari kushirikiana na wafugaji hao ili kufanikisha mipango ya aina hiyo.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika jibu la msingi alilotoa Naibu Waziri, amesema wazi kwamba mitamba 31 kwa Mkoa wa Kilimanjaro ni michache sana na kwa kuwa ng’ombe hao hatuwategemei tu kwa maziwa na hivyo wanavyozungumza kwamba wanahamishwa, tunazungumzia hapa wale ng’ombe wa *zero grazing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni kwamba kwa kuwa, huu mradi umeonesha mafanikio ufanyiwe sasa hali ya kuboreshwa na kurudia tena kuwapatia kila Kaya ng'ombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa, *SACCOs* zilizoanzishwa watu wameingia kwenye *SACCOs* na kipato kile walichokuanacho wengi wao kutoka katika mauzo ya maziwa haya, na kwa kuwa baada ya kuweka akiba katika *SACCOs* hawana cha kuendelea na wanatarajia sasa Serikali iwave *project* ambayo itawapa uzalishaji na kuendeleza kuapta kipato ili waweze kuwekeza. Serikali haioni sasa ni wazi kabisa mradi huu ukaanzishwa upya? (*Makofi*).

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shally Raymond, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba hii mitamba dunia ipo nchini kote na wananchi wanaweza wakiwasilisha maombi yao wanaweza kupewa mitamba bila matatizo. Huu mradi uko katika kanda nne, kuna kanda ya Dar-es-Salaam, ambayo inahusisha mikoa ya Dar-es-Salaam, Pwani, Zanzibar, Lindi, Mtwara, Morogoro na Dodoma.

Kanda ya Mwanza, inahusisha Mwanza, Kagera, Kigoma, Mara, Shinyanga na tabora. Kanda ya Kaskazini Mashariki inahusisha Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Singida na Kondoa. Kanda ya Mbeya, inashirikisha Iringa, Ruvuma, Mbeya na Rukwa.

Kwa hiyo, mwananchi yejote yule ambaye atahitaji kupata mitamba hawa, awasiliane tu na huu mpango wa mitamba dunia na watampatia mitamba bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuibua miradi. Ni kweli kwamba wananchi hawana pesa na wanglipenda kufuga. Kama nilivyosema tuna mpango wa *DADPs*, ambao unapata hela kutoka *Agricultural Sector Revolvement Program* ambao katika miaka saba utakuwa na trilioni mbili na 492 bilioni.

Sasa tungeliomba wananchi waibue mipango wapitishie katika *DADPs* na *DADPs* iweze kuweka programu ambayo Halmashauri iweze kuweka mipango ambayo wananchi katika sehemu hizo wanaweza kukopeshwa mitamba kwa kutumia hii njia angalao hawana pesa halafu wakawa wanalipa ng'ombe kuwasaidia wenzao. Asante sana.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Simanjiro kwa makusudi kabisa kuitia Halmashauri yao waliamua kutenga takribani shilingi milioni 100 kwa nia ya kuapatiwa mitamba na madume bora ya mbegu kwa azma ya kuboresha mifugo yao.

Je, Waziri anaweza kuwaeleza wananchi wa Simanjiro ni wapi sasa wanaweza wakapata mitamba na madume hao bora kwa bei nafuu na bila urasimu wowote?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:
Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Wizara yangu inayo mashamba ambayo yanaweza kuwapatia wananchi mifugo, mitamba ama madume kama wanayahitaji.

Mfano, katika mkoa wa Mbeya tunao Kitulo, ambako tunazalisha mitamba 68 kwa wastani kwa kila mwaka, mitamba hiyo ni ya aina ya *Fresien*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ngerengere Morogoro tunazalisha wastani wa mitamba 57 ambayo ni chotara ya flesheni na borani, Sao Hill Iringa tunazalisha wastani wa mitamba 124 kwa mwaka ambayo chotara kati ya borani na ashire, Nangaramo Mtwara tunazalisha mitamba 62 kwa mwaka wastani wa hiyo ambayo ni chotara kati ya borani na ashire, chotara kati ya borani na flesheni, Mabuki Mwanza tunazalisha mitamba wastani wa 307 chotara kati ya flesheni na borani, Kibaha Pwani mitamba wastani wa 41 chotara kati ya flesheni na boran.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mwananchi yejote anayehitaji ng'ombe wa kisasa anaweza kuwasiliana na mashamba yetu haya. Lakini vilevile sasa hivi tumeona kwamba kusema kwamba kuchukua madume unayapeleka katika sehemu mbalimbali hawatoshi. Sasa hivi kituo chetu kile cha *Artificial Insemination* pale Arusha kwa sasa hivi kina mbegu zaidi ya 70,000 ambayo unaweza kufanya *Artificial Insemination* na mwaka huu kimepewa hela zaidi ya milioni 500 na 100 ni kuzalisha mbegu zaidi ya 100,000. Kwa hiyo, kama unahitaji mitambo tutakupatia ukitaka mbegu utapatiwa na utaalam, tutakupatia. Kwa hiyo, wananchi wajitokeze wachukue nafasi hii kuendeleza mifugo nchini. (*Makofit*)

Na. 112

Ubora wa Mchele Unaolimwa Hapa Nchini

MHE. MWAJUMA H. KHAMIS aliuliza:-

Kwa kuwa, tumekuwa tukishuhudia mara nyingi baadhi ya mchele unaozalishwa hapa nchini na kuuzwa madukani unakuwa na vijiwe vidogo vidogo ambavyo vinaleta athari kwa afya za walaji:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia wakulima wetu kuzalisha na kuuza mchele ulio bora bila vijiwe hivyo ili kunusuru afya za walaji?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, baadhi ya mchele unaozalishwa na kuuzwa madukani hapa nchini, unakuwa na vijiwe vidogo vidogo.

Hii inatokana na wakulima walio wengi kuanika mpunga wao chini au katika barabara mara baada ya kuvuna. Ukaushaji huo ndio chanzo kikuu cha vijiwe katika mchele. Serikali kwa kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inaendelea kuhamasisha matumizi ya maturubai au sakafu za saruji wakati wa kuanika mpunga na kutoa mafunzo ya usindikaji bora wa zao la mpunga kwa wakulima wa zao hilo. Wizara pia imetoe kitabu cha “Teknolojia za kuhifadhi, usindikaji na matumizi ya mazao ya nafaka baada ya kuvuna”.

Kitabu hicho kimesambazwa katika Halmashauri zote za Wilaya kwa ajili ya rejea ya wataalam wa ugani. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Viwango (*TBS*) inawahamasisha wenyewe vinu vya kukoboa mpunga wawe na mashine za kuchambua na kuondoa vijiwe ili kuongeza ubora wa mchele na kunusuru afya za walaji.

MHE. MWADINI A. JECHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, kuzalisha mchele usio na vijiwe ni pamoja na kuweka mashine za kisasa za kukobolea mpunga na kwa kuwa, mashine nyingi za kukobolea mpunga hapa nchini zinazotumika ni za kizamani kiasi ambacho hazikidhi haja inayokubalika.

Je, Serikali iko tayari sasa kuwakopesa vikundi vya akina mama na vijana mashine nyingi za kisasa ili kuondoa tatizo hili la vijiwe kwenye mchele?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge la nyongeza kama ifuatavyo. Wale wanashughulika na biashara hii wanaweza kupata mikopo kutoka sehemu mbalimbali, *SIDO* ni mojawapo ya maeneo ambayo huwa yanatoa mikopo ya mashine.

Lakini vilevile viko vyombo vingine vya fedha ambavyo vinawenza vikatoa mikopo kwa ajili ya kuwapatia mashine zenye teknolojia ya kisasa ili kuondoa tatizo hili.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa muda wa maswali umefika lakini swali namba 113 limefutwa na kwa faida ya Wabunge wengi ningependa kueleza kwamba, kama ulikuwa na swali halafu kwa sababu moja au nyingine likaamuliwa kufutwa mwenye *onus* ya kuomba kusema swali lake linafutwa ni yule Mbunge aliyeuliza na siyo huyo anayejibu. Kwa hiyo, ningependa hiyo mfahamu ni Kanuni ya 41 (b) ndio inaeleza

kwamba, kama yule aliyeuliza swali ndiye atakayesimama na kusema naomba kuliondoa swali langu na siyo vinginevyo. Hii nimeisema kwa sababu Wizara iliyokuwa inahusika ndio ilikuwa inaleta barua hapa kwamba swali hili limeondolewa tumeandika kwa Spika, hapana, anaondoa mwenye swali.

Tangazo lingine ni wageni, na hili nalo ninaomba Waheshimiwa Wabunge tukumbuke na itakuwa leo mara ya mwisho kusoma wageni walioandikwa kwa vikaratasi vilivyoletwa kama hivi. Itakuwa leo ni mara ya mwisho kwa sababu utaratibu tuliookubaliana nao mnapeleka Ofisi ya Bunge, kwa sababu mgeni huyo humwoni hapo ukasema kumbe kuna mgeni pale ngoja nimpelekee Spika, hapana. Leo ni mara ya mwisho, vikaratasi hivi leo vya mwisho kesho wenyeviti hakuna kupokea vikaratasi hivyo, tufuate utaratibu. (*Makofi*)

Wageni ambao wameletwa rasmi hapa wapo wageni wa Mheshimiwa Monica Mbega, ni Waheshimiwa Madiwani 17 kutoka Iringa Mjini naomba wasimame walipo, karibuni sana, hawa wanaongozwa na Naibu Mstahiki Meya Mheshimiwa Shadrack Mkusa, tafadhali anyoshe mkono, tuna wageni wa Mheshimiwa *Dr. Cyril Chami*, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, wao ni wanafunzi sita kutoka Shule ya Sekondari ya Marianne ya Bagamoyo wakiongozwa na Indiolata Cyril Chami, sasa sijui ndio nani?

Waheshimiwa Wabunge, wapo Dodoma kufanya utafiti wa utawala bora, wale wanafunzi wasimame wa kutoka Marianne Bagamoyo. Hii ni shule ya wasichana ni moja ya shule *best in the country*. Hongera sana mimi nimefika kule, ni shule moja nzuri sana kwa wasichana, tumefurahi sana, karibuni sana, tuna wageni wa Mheshimiwa *Dr. Guido Sigonda* wao ni wakulima, wafugaji na wapiga kura wake jumla wako sita, wale wageni wa Mheshimiwa *Dr. Guido Sigonda*, ahsante sana nashukuru na jinsia imekuwa *taken care of*, ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Halafu tuna wanafunzi 50 kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri Dodoma. Hili ni kundi lingine naona walimu wameamua kufanya hivyo, naomba wasimame wanafunzi wa kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri Dodoma. Nadhani mpaka tutakapomaliza wanafunzi wote watakuwa wamepitia hapa, ahsante sana na walimu wao. Tuna wanafunzi wachungaji 51 kutoka Chuo cha Biblia cha *Assemblies of God* hapa Dodoma, naomba wachungaji wasimame, ahsante sana na karibuni sana katika ukumbi wetu. Tuna wageni wa Mheshimiwa Shibiliti, mmoja ni mtoto wake Bwana Emmanuel Dalali Shibiliti, nadhani yeye amemaliza *Form Six* na anategemea kujiunga na Chuo Kikuu, yuko wapi huyu Shibiliti mdogo, karibu sana. (*Makofi*)

Kuna wageni wa Mheshimiwa William Shellukindo ambao ni mgeni wake Bwana Idd Washokera, yeye ni mgeni wa Mheshimiwa Shellukindo, Ndugu Washokera yuko wapi?, tuna wageni wengine wa Mheshimiwa *Capt. Komba* ambao ni Ndugu Flora Mbasha, yeye ni mwimbaji wa nyimbo za injili yuko na Bwana Mbasha yaani hapo

nafikiri ni *Mr and Mrs* na wasanii wenzao wa kundi lake, hao wasanii wengine wasimame, ahsante sana tunashukuru kwa hizo nyimbo za injili. (*Makofî*)

Kama nilivyosema Waheshimiwa Wabunge, Bunge huendeshwa kwa utaratibu, tukienda kwa utaratibu mzuri mambo yetu yanakuwa mazuri, hii ni pamoja na wageni wenu kuleta taarifa iandikwe isomwe vizuri.

Matangazo yanahusu kazi, kwanza kabisa Ndugu Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI Mheshimiwa Leadiana Mng'ong'o anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI kuwa leo tarehe 26 kutakuwa na kikao cha Kamati saa tano asubuhi katika ukumbi Na. 428 ghorofa la nne Jengo la Utawala, halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Mheshimiwa George Malima Lubeleje anaomba niwatangazie wajumbe kwamba leo tena tarehe 26 katika chumba Na. 216 kutakuwa na kikao cha Kamati saa tano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kuwa leo tena tarehe 26 kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika saa saba mchana katika chumba Na. 227.

Pia Dr. Raphael Chegeni yeche ni Mwenyekiti wa Tawi la CPA Tanzania anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya CPA Tanzania kuwa leo tarehe 26 kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika katika ukumbi Na. 133 ghorofa ya kwanza katika Jengo la Utawala saa saba mchana.

Pia Mheshimiwa Leadiana ambaye pia ni Mwenyekiti wa hii Kamati ya Kuratibu Mambo ya UKIMWI walipokuwa kwenye kikao cha Wabunge cha Kimataifa IPU ni *Inter Parliamentary Union* alifanikiwa akateuliwa na Rais wa IPU kuwa mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya Masuala ya UKIMWI yaani *Advisory Committee on HIV Aids* yenye jukumu la kushauri na kutoa mafunzo kuhusu masuala ya UKIMWI kwa Wabunge Duniani, maana yake ile *Inter Parliamentary Union* ni ya Duniani.

Sasa yeche ameteuliwa kuwa mjumbe wa Kamati hiyo kwa muda wa miaka minne kuanzia Mei mwaka 2008 mpaka Mei 2012 na Kamati yenyewe ina wajumbe 12 ambao wanateuliwa kutokana na uwanaharakati wao katika masuala ya UKIMWI, kwa hiyo tunafuraha sana kumpongeza Mheshimiwa Leadiana Mng'ong'o ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge wa Afrika kuhusu UKIMWI na mnafahamu na hapa ni TAPAC ni yeche kwa hiyo amebobebe mambo haya tunaomba tumpongeze sana na ni Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Iringa. (*Makofî*)

Tangazo lingine ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Spika ameondoka leo hii asubuhi kwenda *Pretoria South Africa* kwenye Mkutano wa Kamati Tendaji ya SADC Parliamentary Forum, yeche ni mjumbe katika Kamati ya Utendaji na kwamba hicho kikao ndicho kinachofanya maandalizi ya kikao cha kawaida cha SADC

kitakachofanyika kwetu Tanzania mwezi Novemba, kwa hiyo ameondoka leo Jumatatu atakuwa na sisi kazini, kwa hiyo sisi tunaendelea na kazi.

Tangazo lingine Waheshimiwa Wabunge, nina barua zote hizi zinaniambia kwamba wanaomba niwapendelee kuchangia humu. Haiwezekani, Waheshimiwa Wabunge haiwezekani kwa sababu tunabandika majina pale na kila mtu anajua atachangia namna gani na tunafanya hivyo makusudi kwa sababu ni kweli kabisa wajumbe ambao wanatakiwa kuchangia sasa hivi ni 51 na majadiliano yetu haya tunaishia leo na kwa wastani tunachangia watu 22 tu.

Sasa ukisema mimi nikupendelee lazima useme nimwondoe nani? Ukisema mimi nikupe nafasi wewe niambie tu nimtoe nani basi, mimi hapo nitafanya. Kwa hiyo ndugu zangu tutafuata orodha hiyo vinginevyo hatuwezi kufanya kwa sababu hakuna namna, tukitaka amani hapa tufuate taratibu, kwa hiyo baada ya kusema hayo ninaomba tuendelee na kazi, Katibu. (*Makofi*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

(*Majadiliano yanaendelea*)

NAIBU SPIKA: Jana jioni tulipokuwa tunaahirisha kikao wafuatao walielezwa kwamba wajiandae, nao ni Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwaga, Mheshimiwa *Dr. Chrissant Mzindakaya*, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuberi, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, mjiandae, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwaga.

MHE. MKIWA A. KIMWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza ninapedna kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo na kunipa afya nami kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu kuweza kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kuwapongeza vijana chini ya umri wa miaka 17 wa timu ya mpira ya Mkoa wa Mwanza kwa kufanya vizuri na kuweza kuingia nusu fainali katika mashindano ya *KOPA COCA COLA*, Wabunge wote wa Mkoa wa Mwanza tunawaunga mkono na tuko pamoja nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea kwanza kabisa suala la wafanyakazi wa Viwanda vya Samaki vya Mwanza, naniomba Serikali ichukulia maanani sana suala la wafanyakazi wote wanaofanya kazi katika viwanda vya watu binafsi hasa wawekezaji.

NAIBU SPIKA: Punguzeni mazungumzo.

MHE. MKIWA A. KIMWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, vijana hawa wanaofanya kazi katika Kiwanda cha *Vick Fish* walifukuzwa kazi na mwajiri bila kufuata sheria za kazi.

Vijana hao wamechukua hatua zote za kisheria mpaka wana barua ya kutoka kwa Katibu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini mwekezaji huyu hasikii lolote wala chochote na wala haitaji kutoa haki ya aina ye yeyote kwa vijana hawa. Hivi ninaiomba Serikali kuiuliza juzi tumesikia Wabunge wamefukuzwa kwenye hoteli ya mwekezaji ya VIP, leo hii mwekezaji mwingine anapata barua kutoka kwa Katibu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini haina utekelezaji wa aina ye yeyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barua hiyo ninayo hapa iliyotoka kwa Katibu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa ningependa niulize, Watanzania ndani ya Tanzania haki yao iko wapi na haki yao wakaipate wapi? Kama mwekezaji anafikia mpaka kudharau ofisi maana yake Katibu wa Rais ni maagizo kutoka kwa Rais, amefikia kudharau na kutochukua hatua ye yeyote Serikali. Mimi ninaiomba Serikali na ninaishauri ifuatilie suala hili kwa umakini ijue hawa vijana hatma ya maisha yao, kwanza wanahangaika, hawajalipwa haki zao, wana familia zao pia na bado hawajatendewa haki ya aina ye yeyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kuongelea suala la maji katika Jiji la Mwanza, tumesikia hapa kwamba bajeti ya maji imeshuka baada ya mradi mkubwa wa maji ya Shinyanga – Kahama kukamilika. Lakini cha ajabu kama siyo cha kusikitisha Jiji la Mwanza maji ni matatizo makubwa sana, kuna shule za sekondari ziliziko maeneo ya Nyasaka, zilizoko maeneo ya Kiloleli hazina maji na kuna shule za *boding* pia za wasichana wanachoka maji mtaroni ndio wanaenda kufanya nayo shughuli nyingine ndogo ndogo kama kuoga na kufua, hivi kweli tunauliza wananchi wa Mwanza maji yanakuja Kahama na Shinyanga wakati Mwanza tuna shida kubwa sana ya maji ambayo maji hayo yangweza angalau kufika kwenye maeneo muhimu ya jiji, ni ndani ya jiji sijakwambia vijihi vya nje ya jiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ninakwambia hata mimi linanigusa, nyumba ninayoishi mimi mwenyewe ya kwangu mwenyewe tangu nimeweka maji nimepata maji labda kwa mwaka mara moja na niko katikati ya Jiji la Mwanza, sasa tunaiomba Serikali, ninafikiri kuna usemi unaosema, mpishi huonja mchuzi chumvi jikoni lakini Serikali yetu haijui huyu ni mpishi, huyu amekaa mezani anasubiri kuletewa, au huyu anahitaji kitu gani katika kitu ambacho ni rasilimali ya mkoa ninaotoka na si Mkoa wa Mwanza peke yake ni Kanda ya Ziwa nzima tuna shida ya maji kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali sasa ieleteze macho yake kwa wakazi wa Mwanza, wanawake wanaamka saa saba za usiku kwenda kusubiri maji ya kulinda kiangazi kama hiki, matokeo yake ni wanawake kwenda kufanya mambo ya ajabu huko huko mitoni wanakokwenda kulinda maji kwanza maji ni machafu, kila mtu anachota kwa ndoo yake anayoitaka ye ye kwa muda wa usiku mkubwa. Ninaombwa

Serikali iliangalie hili na iwaangalie wananchi na hasa wanawake wa Jiji la Mwanza na wanafunzi wanaoishi katika maeneo yenye shida ya maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia sheria au uchangiaji wa maendeleo, mimi sipingani na maendeleo na wala sizuui wananchi kuchangia maendeleo. Lakini uchangiaji wa maendeleo haya umekuwa ni kero na karaha, wananchi wanachangia maendeleo yao lakini inakuja kufikia sehemu maendeleo yale wanaoyachangia wananchi inakuwa adha, pesa zinazochangiwa na maendeleo hazifanyi kazi inayopaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa mfano katika kijiji kimoja kilichoko mjini hapa hapo Igogo mtendaji wa kata akichangisha pesa za sekondari, sekondari zinajengwa chini ya viwango, sekondari zinabomoka na zikishabomoka anawachangisha tena mara ya pili wananchi wale wale, Serikali imefikia kiasi kwamba kuwachangisha wananchi watendaji bila kuwasomea mapato na matumizi ya shughuli hizo wanazochangia.

Hivi ninaomba kuiuliza Serikali pale tunaposema kwamba tunachangia maendeleo ni kwamba kumnyonya mwananchi au mwananchi kuona alichokichangia kinamsaidia? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimeenda katika Jimbo la Sengerema katika Kijiji cha Busweru, mtendaji wa kijiji amechangisha pesa za kujenga shule, shule hiyo imejengwa, shule hiyo imebomoka mtendaji wa kijiji anatoa amri kwa askari wa kijiji ambao ni mgambo shule hiyo imebomoka, mtendaji wa kijiji anatoa amri kwa askari wa kijiji ambao ni mgambo wawachangishe watu tena kwa nguvu.

Lakini nilisikia Mbunge wa Jimbo hilo akisema mwizi ni yule ambaye anabomoa ndio mwizi si mwizi ambaye habomoi, hakuna mwizi mbaya kama mwizi anayeiba kwa kalamu anaibu nguvu za wananchi, anawanyonya wananchi na kisha anawalazimisha wananchi kuchangia tena kwa mara nyengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali ifuatilie katika Kijiji cha Busweru kuangalia suala hili kwa undani zaidi kwa sababu wananchi wameshachoka na katika majibu ya maswali yaliyoulizwa hapa katika Bunge la 11 walisema kuchangia maendeleo ni lazima na mtu akimkataza mtu kuchangia maendeleo ashtakiwe, hivi kweli tutashtaki kwa watu wanaofanya ufisadi? Kwa sababu ufisadi hauanzii juu, usifadi uko chini, pale mnavenporta kitu fulani kichangiwe mnawapa watu wengine njia ya kutafuta ulaji kweye kitu kile, kwa hiyo mimi ninaiomba Serikali iwe makini sana kwa hilo vinginevyo tutakuwa tunawanyonya damu hawa wananchi ambao wanatakiwa kupata angalau pato lao la Sh.1,500/= kwa siku na anapochangia Sh.20,000/=, Sh.20,000/= haifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mfano mdogo, Wilaya ninayotoka kuna Shule moja ya Msingi inaitwa Isenga, Isenga ile ina watoto zaidi ya 3,000 lakini inatakiwa kila mtoto achangie Sh.20,000/= ya choo, siyo kila mzazi kila mtoto hivi tunatoka wapi, tunaenda wapi na tuko wapi, hivi nchi hii kweli tunawatakiwananchi mema?

Mwananchi huyu anaishi kwa kipato cha Sh.1,500/= kwa yule anayefanya kazi asiyefanya kazi anaishi kwa kipato cha shilingi ngapi? Na watoto kama 3,000 kila mtoto achangie Sh.20,000/= ina maana hicho choo ni choo ni handaki la kuzika watoto hao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali, Serikali inakuwa na dhamira nzuri lakini watendaji wao wana dhamira mbaya na dhamira chafu sana, suala hili nilishamfikishia Mbunge wa Jimbo Mheshimiwa Diallo na nilimwomba alishughulikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda ya Ziwa tunaposema Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Mwanza una wavuvi, wavuvi hawa wanavua na kuliingizia pato Serikali bila kupewa nyenzo na Serikali wavuvi hawa wanavua kuliingizia pato Serikali kwa juhusi zao wenyewe na elimu waliyorithi kutoka kwa mababu zao, ninakuja kwa Serikali, Serikali inapomkuta mvuvi yule na kokolo inamwambia kwamba huu ni uvuvi haramu.

Mwaka 2006 nilichangia katika Bajeti ya Maliasili na Utalii alikuwa Waziri Mheshimiwa Diallo na Mheshimiwa Diallo aliahidi atasaka godauni zote zinazoingiza nyavu hapa Tanzania na kuweza kukamata makokoro, mpaka leo ni kimya hatujaambiwa ni kokoro ngapi zimekamatwa hatujaambiwa kwamba ni kiasi gani cha nyavu halafu zilizopo kwenye magodauni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaiomba Serikali ahadi hizo walizotupa zisiishie kwenye makaratasi tu kwani mvuvi huyu ananunua nyavu kutoka dukani Serikali inajua, nyavu hizi zinaingia nchini zinalipiwa na VAT Serikali inajua. Lakini ni yule mvuvi akiichukua nyavu tu akaingiiza ndani ya ziwa anaambiwa hii nyavu ni haramu, kaitoa wapi?

Tunaiomba Serikali hawa wananchi ni wananchi maskini, hawa wananchi wanatumia elimu yao wenyewe waliyopewa na babu zao kwa sababu Serikali haiwajali pamoja na kwamba kusema kuna mikopo ya uvuvi lakini wavuvi wengi hawapati mikopo ya uvuvi kwa sababu kwanza imekuwa na usumbufu kupita kiasi, naomba na hili pia liangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa Hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 75 Ibara ya 105 ameongelea Jiji la Dar es Salaam na kwamba bado wanafanya angalau wameunda Kamati ndogo ya kufanya mapendekezo ya Jiji la Dar es Salaam.

Kwa hiyo, ametuomba Mkoa wa Mwanza kwa kuwa tunataka kuunda Halmashauri mbili kama Jiji la Dar es Salaam tusubiri kidogo.

Ninaiomba Serikali kwa sababu Serikali ni sikuvi na huo mchakato waliouweka usichukue muda mrefu tunawaomba Halmashauri ya Jiji la Mwanza iweze kutumia Halmashauri mbili kama kikao cha Madiwani kilivyopitisha na kikao cha Mkoa kilivyopitisha.

Nina imani Jiji la Mwanza pia ni watu karimu, wanaweza wakafanya hiyo kazi na mojawapo ni kuwasogezea wananchi huduma karibu za Halmashauri ya Jiji kwani tumejenga jengo tayari liko tayari likisubiri kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Seriali ituruhusu kwa sababu Dar es Salaam si mfano. Mwanza tunaweza tukafanya vizuri zaidi ya Dar es Salaam. Nafikiri hata katika usafi Jiji la Mwanza tunaongoza kwa usafi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea kidogo suala la Mahakama ya Kadhi. Suala la Mahakama ya Kadhi limekuwa likipigiwa kelele sana huku Tanzania Bara na suala la Mahakama ya Kadhi si suala la itikadi wala si suala la kusema kwamba ni la sera ya chama fulani.

Napenda kusema kwamba mchangiaji aliyemalizia kwa jana jioni alisema Wabunge wa *CUF* tumechupia kwenye suala la Mahakama ya Kadhi, si kweli.

Ninapenda kumfahamisha kwamba Mahakama ya Kadhi inashughulikia ndoa, talaka na mirathi na ndoa, talaka na mirathi katika vitabu vya *Quran* vimeeleza waziwazi. Kwa hiyo, hii ni *agenda* ya Waislam wote na si sera nimeeleza waziwazi.

Kwa hiyo, hii ni agenda ya Waislam wote na si sera ya chama fulani, kama ni sera ya chama fulani na yenye we imechupia kwenye vitabu vya *Quran*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika itikadi hii Waislam wote hii ni *agenda* yao ya Mahakama ya Kadhi na hata Wakristo wenye kuutakia Uislam ili uendelee kuishi katika hukumu za Kiislam, hii pia wanaweza wakaisemea. Kwa hiyo, hii ni *agenda* ya Waislam wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchangia jambo moja, napenda kuchangia jambo la kuhusiana na hiki kitu wanaita Utawala Bora. Utawala Bora ni utawala wa kisheria lakini pale inapofikia kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu amegusa maeneo ya uchaguzi pale inapofikia nyakati za uchaguzi, Utawala Bora unaenda likizo.

Kwa hiyo, ninaiomba Serikali Utawala Bora usiende likizo wakati wa uchaguzi kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia suala la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2009. Katika chaguzi za Serikali za mitaa tunashuhudia tukiona watu fulani wanapiga kura zaidi ya mitaa miwili, mitatu na watu wengine wakiwasindikiza kwa magari, huu ndio Utawala Bora wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi unakuwa sio wa haki, uchaguzi ume-base kwene upande mmoja, kila mtu ukimuuliza, anasema kwamba uchaguzi ume-base upande fulani. Wale wote wanaosimamia chaguzi hizo, wanateuliwa na Mkurugenzi na Katibu Kata, ni Msaimamizi. Katibu Kata huyo amewekwa na chama fulani, hivi kweli atawatendea haki chama kingine? Ni kwa nini shughuli hizi za uchaguzi, isikabidhiwe moja kwa moja Tume ya Uchaguzi na Tume iliyo huru na haki bila kuegemea upande wowote?

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema kuhusu marekebisho ya Taftari la kudumu. Nasema hili kwa uhakika kwa sababu nimeshuhudia Daftari la Kudumu linafanyiwa marekebisho, cha kustaajabisha watu wanakwenda pale kuijandikisha wanakuta mkanda wa kupiglia picha hakuna, sijui hili daftari linarekebishwa vipi? Sielewi linarekebishwa kwa njia gani kama mkanda wa kupiglia picha unakuwa hakuna. Akifika pale mtu anayeielewa Sheria na akasala, anaambiwa njoo kesho saa nne na akifika saa nne anakuta mkanda upo, sielewi linaboreshwa vipi. Ni lazima Serikali isimamie suala hili kwa sababu Serikali inatumia kodi za wananchi katika kurekebisha daftari hili na kama Serikali inatumia kodi za wananchi ni lazima wananchi wanyonge wa Tanzania watendewe haki si kuangalia kwamba hapa ni chama gani kimeshika nguvu, uwaambie mikanda imekwisha na hapa chama gani ambacho hakijashika nguvu ndiyo uwaambie hapa ndipo mikanda ilipo. Tunauomba uwanja wa siasa uwe wa wazi, huru na wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mimi nadhani watu wanachanganya Katibu Kata na Mtendaji wa Kata, nafikiri mnamaanisha Mtendaji wa Kata siyo Katibu Kata.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERÄ, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Mwongozo, endelea.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERÄ, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Naibu Spika, siku za karibuni, kumekuwa na mazoea ya Waheshimiwa Wabunge, kuleta nyaraka za siri za Serikali na kuzionyeshaonyesha hapa kwene ukumbi. Kuwa na nyaraka za siri, kwa Sheria za Tanzania, ni kosa kubwa la jinai na mtu akipatikana na hatia, kifungu kinakwenda kwene miaka 20 jela na duniani kote, nyaraka hizi hazijadiliwi Bungeni ambapo ni mjadala wa wazi.

Sasa naomba mwongozo wako, kwa vile humu ndani kuna kinga na kwa maeneo yote ya Bunge kuna kinga, hivi siku vyombo vya dola vikiacha kufumbia macho makosa haya ya jinai ya wazi na kuwazuiazuia na kuwapukua Waheshimiwa, itakuwaje?

Sasa, mwongozo wako ni kwamba hawa wenzetu wanaacha nyaraka hizi humu au zinawajia humu kimujiza? Kwa sababu kuzipata kwanza ni kosa la jinai aidha zimeibiwa na kutembea nazo huko mitaani ni kosa la jinai.

Sasa, mwongozo wako ni kwamba hizi nyaraka huwa zinabaki humu au wanakuwa nazo huko mitaani kwa sababu kuna siku inaweza ikaja kutuathiri wote hapa kama vyombo vya dola vikianza kutupekua.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, unajua humu ndani kama mtu anasimama kujadili jambo anakuwa labda na gazeti, inabidi amuombe Spika kwamba naomba kwa ruhusa yako nisome au ninukuu kwenye gazeti hivyo kama kuna kitabu chochote anachotaka kunukuu inabidi aseme kwamba Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruhusa yako, ninukuu kilichopo kwenye kitabu. Ndiyo maana tuna Kanuni ya kutokusoma kitu chochote ila kwa ruhusa ya Spika. Sasa kama unataka nyaraka yako hiyo iweze kutambulika hapa, unatakiwa uiweke Mezani hapo, inakuwa ni nyaraka ya Bunge na Bunge litajua hii nyaraka inatokea wapi au vipi sio unasema kwamba unajua nina nyaraka hii hapa na kadhalika, hapana, hiyo siyo *official* kwetu sisi. Kwa hiyo, ukikutwa na kitu cha namna hiyo mitaani, hiyo ni shauri yako wewe, siyo shauri ya Bunge hili.

Kwa hiyo, unapo *refer* kwenye *document* yoyote ile, lazima utuambie hiyo *document* uliyonayo na unaomba ruhusa kwamba natumia nyaraka fulani. Hata hotuba ya mwenzio au hata hotuba ya Mawaziri, unasema naomba kwa ruhusa yako nisome hotuba ya Waziri kifungu fulani, si ndiyo mnavyosema na ndivyo inavyotakiwa. Sasa unaposema nina kiambatanisho fulani ni lazima kiwekwe Mezani, huo ndio utaratibu wa Bunge hili.

Tunaendelea, anayefuata ni Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, ajiandae.

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii, nikushukuru sanasana kwa kunipa nafasi hii ili niweze na mimi kushiriki katika kutoa maelezo yangu kuhusu hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri na kwa kipimo cha uhakika kabisa, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo K. Pinda, ameanza kazi yake vizuri, tunampongeza sana. Tunaomba aendeleze tabia hii ambayo ameanza nayo ya kushirikiana na kuwa karibu na

Wabunge kwa sababu ni kweli kabisa kuwa Bunge ndiyo wawakilishi wa wananchi na ni sauti ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo agenda yangu ni moja kilimo na ufugaji. Lakini kabla sijasema hiyo, ninapenda tutambue juhudhi kubwa sana ambayo Wabunge wanafanya katika kuongoza Majimbo yao hapa Tanzania. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuwa Waziri wa Serikali za Mitaa, ndiye aliyekuwa anashughulikia suala la kuwawezesha Wabunge kuwa na fedha za maendeleo ya Jimbo. Kwa hiyo, naomba jambo hili lipewe umuhimu kwa sababu hakuna hoja yoyote inayozuia suala hili kutekelezwa. Kama rafiki zetu wanaotupa misaada ndiyo sehemu ya kikwazo, naomba Serikali ikae nao au ikibidi waje hapa sisi wenyewe tuwaeleze, waelewe kwa nini ni muhimu Mbunge kuwa na fedha kwa ajili ya kusaidia nguvu za wananchi katika Jimbo na mambo haya siyo Tanzania peke yake yamefanyika pia mahali pengine. Kwa hiyo, ninaomba kwa kuwa Mheshimiwa Pinda, ni Waziri Mkuu sasa na alikuwa analishughulikia jambo hili basi lipewe umuhimu wa kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kama nilivyosema, leo agenda yangu ni kilimo. Kilimo siyo uti wa mgongo, isipokuwa ni uhai wa Taifa lolote lile. Maendeleo ya nchi zote tunazozisikia zinasifiwa kwa mfano Amerika na Ulaya walianza na kilimo, kilimo ndiyo kimezaa viwanda na maendeleo ambayo tunasikia wenzetu wanazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoona hapa kilimo cha Tanzania hakina mwenyewe na mwenyewe ni *peasant* yaani yule mkulima mdogo kabisa na nchi haiwezi kwenda kwa mkulima yule mdogo ambaye hata jembe la kulimia ni la mkono. Takwimu ambazo zinatolewa kuhusu kilimo, siamini kama ni sahihi. Hizi takwimu za kuelezea kilimo kilivyoendelea na tani zitakazovunwa, zinapatikanaje? Kwa sababu wanaolima ni wale ambaeo hawana mwenyewe! Kwa hiyo, nataka tukubaliane leo kwamba kilimo cha Tanzania mwenyewe awe ni Serikali na Mkulima na ili tufike hapo mimi napendekeza kwamba kuwe na mpango wa kitaifa wa kuendeleza kilimo cha mazao ya chakula na biashara na katika kutekeleza mpango huo, Mikoa yote ya Tanzania, ishirikishwe ili kila Mkoa uweze kueleza namna gani wataendeleza kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano wa dhati ambaeo mimi mwenyewe nina uzoefu nao, labda kabla sijautoa nataka niseme kwamba Benki Kuu waliwahi kutumia fedha, wakaweka kampuni moja inaitwa *HYPER*. Hii kampuni ya *South Africa*, ilitengeneza mpango huu wa maendeleo ya kilimo unaoitwa *feasibility study on the development of agriculture in Tanzania*. Huu mpango ulitengenezwa mwaka 2002 lakini ukawekwa kwenye kabati kwenye Wizara husika na mpaka leo haujatumika. Kwa hiyo, napendekeza kwamba ili hii nchi iweze kuendeleza kutokana na kilimo, tuwe na mpango ili wote tunapokutana hapa tuzungumzie mpango ambaeo pia una *program* za kuutekeleza kwa kila zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja hapa, tunapiga kelele kuhusu *report*, ni kweli kwa sababu hatujui hata hizi takwimu tunazoambiwa mahitaji ya pembejeo ni kiasi hiki, mimi siwezi kusema mia kwa mia kwamba ni hakika kwa sababu hakuna mpango

unaotuonyesha zana za kilimo, washiriki, mazao yatakayolimwa na pembejeo inayotakiwa, kama upo, uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa ambayo imetolewa mwaka huu kwa ajili ya kuendeleza kilimo, itatumika kwa ajili ya semina, mikutano na utawala. Mimi nazungumzia kilimo ambacho fedha inayotengwa itafika kwa wakulima kuongeza uzalishaji wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi, mtu ukijitaja, inaonekana kama ni kasoro lakini duniani kote, mtu anayesema anaweza kuwa na nguvu kama akifanya *reference*, mimi nitafanya *reference* na ushahidi upo, kila mtu anaweza akaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, nilitumia Chuo Kikuu cha Sokoine na Mzumbe, kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Mkoa wa Morogoro na mmoja wa watalamu, alikuwa ni Mheshimiwa Prof. Maghembe, yupo hapa, nilimteua kwenye Kamati ya Wataalamu. Mwingine ni Mheshimiwa Juma Ngasongwa, alikuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Moja ya Masharti, niliwaambia, nendeni mkakutane na wananchi ili mpango uwe shirikishi. Ulipokamilika, nikaalika benki zote za Tanzania, Mwenyekiti wa Benki, aliyeongoza timu hiyo ya Wanabenki, ni Marehemu Garana Nyirabu. Niliwaalika Mkoa wa Morogoro, wakaja, tukajadiliana na tukakubaliana watawakopeshaje wananchi. Leo kuzungumza habari ya Mkoa kusimamia bei na kusimamia kukopesha, ni kama jambo jipya, hili ni jambo ambalo linatokea duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hawa wataalamu wakaja, ule mpango tulipounadi, tukapata fedha, tulipata trekta kutoka FAO, Italy, yalikuja Morogoro moja kwa moja kwa Mkuu wa Mkoa. Yalifanyiwa *assembling* Morogoro na Ofisi yangu ndiyo ilikuwa dhamana ya kudhamini wakulima wa Morogoro wanaokopeshwa matrekta.

NAIBU SPIKA: Na mimi ndiye niliyeyapokea yale matrekta.

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Ahsante sana, kweli wewe ndiye uliyeyapokea matrekta hayo. Sasa mambo haya tunayona kama ya ajabu, mimi niliyafanya miaka 20 iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokwenda Morogoro, Rais alinipa malengo kwamba nenda kaendeleze kilimo cha chakula na biashara, miaka mitatu nilishapandisha uzalishaji wa mazao, ukifika nyumbani kwa mtu anasema sitakupa pa kulala kwa sababu nina wageni na wageni hao ni mpunga na mahindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu wa wakati huo, Mheshimiwa Warioba, alipokuja kutembelea Mkoani kwangu, nilimpeleka kwenye shamba la wakulima wadogo ambao walilima hekta 12,000, wakulima wadogo. Wakati ule nilipokwenda Morogoro, niliambiwa watu wa Morogoro ni wavivu, hakuna mtu mvivu Tanzania, uvivu unatokana na kutokuwa na mipango. Hata viongozi wote wa Serikali wanakuwa wavivu kwa sababu wanakuwa hawana malengo ya kutekeleza. Sasa kipimo kiko wapi, huna mpango wewe

ni mvivu. Hata nyumbani kwako utaamkaje asubuhi na hujui utakwenda wapi, lazima nyumbani kwako uwe na mpango wa jinsi ya kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeondoka Morogoro, nimeacha matrekta zaidi ya 300 na Mkoa ungeruka lakini kwa fitina, watu fulani wakaona mafaniko, wakala njama niondoke na Mkoa ukaporomoka, hakuna aliyeendeleza mambo yale. Ndiyo Tanzania hiyo! Nchi hii, hakuna mtu mzuri, watu wote ni wabaya kwa sababu hatuna vipimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Kigoma wapo hapa, nimekwenda Kigoma, wakasema amepewa adhabu, nikaambiwa watu wa Kigoma wavivu, Masheikh, Waswahili. Nilikaa mwezi mzima, Rais akaniambia utakwenda Kigoma, baada ya mwezi, nikaenda kununua Quran Tukufu, nikaanza kusoma kwa sababu nilijua ninakwenda kule kwa watu waliosoma dini, ukizungumzia waliosomea dini vizuri ya Kiislam, usiiondoe Kigoma. Nikaanza kusoma, nilipofika, nikaanza na Masheikh, tukashikamana, Wabunge wa Kigoma wapo hapa, tukaandaa mpango na aliyeongoza Kamati ya Wataalamu ya kuandaa mpango wa Mkoa wangu, ni Mheshimiwa Dr. Kigoda yupo hapa, nilimuomba Serikalini. Ndugu Ngirwa kutoka Kilimo na Ndugu Mgumia, nikawashirikisha wataalamu wa Mkoa ule tukaandaa mpango na tukauuza kwa wahisani na niilipata fedha kutoka Sweden, Norway na Benki Kuu (*BOT*), tukanunua matrekta zaidi ya 100. Waziri Mkuu, wakati huo, Mheshimiwa Malecela ndiyo aliyeuja kufungua matrekta yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulianzisha mpango wa kulima michikichi, nilikuwa naagiza mbegu kutoka Costa Rica na baadaye nikaanza kuagiza mbegu kutoka Ivory Coast. Nilikwenda mwenyewe mpaka Malaysia nilikutana na Waziri Mkuu wa wakati ule, Ndugu Mahati, mara mbili, alinipokea na gharama yangu yote nililipiwa na Serikali ya Sweden.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulianzisha mpango wa kukopesha wananchi kuvua samaki na tulichagua mahali pa kulima kahawa na michikichi. Tulipeleka Makatibu Tarafa na Mabwana Shamba Ivory Coast kusoma, hayo yamefanywa na Mkuu wa Mkoa! Sasa leo Serikali inashindwaje mambo hayo? Sisemi kwa kujigamba ila nasema kwa kueleza kwa mifano, hakuna kisichowezekana. Tunatumia muda mwingi sana kwa maneno, huwezi kusema kilimo hoyee, mahindi yakaota, yataotaje kwa hoyee? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, usindikaji wa mazao umekuwa wimbo. Aliyekuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi juzi, Mheshimiwa Edward Lowassa, ni shahidi. Sisi tunasema hivi na naiomba Serikali tuelewane, yapo mambo ambayo mkichagua ni lazima muamue kuyasimamia yafanyike. Usindikaji wa mazao ya chakula, ni jambo ambalo lazima lielekezwe na Serikali, nchi hii, tutauza pamba ghafi mpaka lini? Tutaendelea kunywa *juice* za madawa mpaka lini? *Chemicals* ndiyo *juice* tunazokunywa Tanzania na siku moja nilileta Bungeni hapa tomato zinazotoka nje ya Tanzania, lazima sisi tuseme program yetu ya kilimo na usindikaji itakuwa miaka kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa umekuja ugomvi wa kusamehe kodi mafuta ghafi. Wabunge, mimi ni shahidi. Serikali ilituma wataalamu, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda, Katibu Ofisi ya Rais na Fedha kwenda Malaysia wakakuta Kule Malaysia hakuna mafuta ghafi, hii habari ya kusamehe mafuta ghafi, yako wapi mafuta ghafi? Hakuna duniani kote kuna mafuta ambayo ni *semi-refined!*

Mheshimiwa Naibu Spika, ulitokea ugomvi, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, akaumua kati ya watu wadogo na watu wakubwa. Wenye viwanda vyta mafuta, ni wakubwa na ni manyangumi wanaotaka kugandamiza wakulima wadogo na viwanda vidogo vilivyopo. Kazi yetu ni kulinda viwanda vidogo na mkulima mdogo, tunatakaje kuwanufaisha hawa? Wameambiwa waende Kigoma kulima michikichi hawataki, wamejenga matanki sawa na matanki ya kuuzia mafuta ya petroli kwa ajili ya ku-*import* mafuta kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lilishaisha sielewi kwa nini Serikali imerudia tena kulileta humu, lilishaisha (*it no longer an agender*), jambo hilo hilo la mafuta ndilo lililomfukuzisha kazi Waziri Mbilinyi, jamani Wabunge wa zamani tumesahau? Aliwasamehe kodi watu haohao, ikamgharibu hapa ndani. Kwa hiyo, naomba mafuta hayo yatozwe kodi. Malaysia kwa michikichi peke yake, wanaingiza bilioni 4.9 USD, sisi Tanzania tuna nafasi kubwa kuliko Malaysia ya kulima michikichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza, nataka kuwaomba Wabunge, nawaomba radhi, sitaki kum-*offend* mtu lakini nataka kusema kweli kwamba kuongoza ni kuonyesha njia, huwezi kuwa Mbunge wala Kiongozi wa aina ye yote kama wewe mwenyewe huonyeshi njia. Kama wewe ni Mbunge wa wakulima, hebu lima shamba zuri watu walione, fuga ng'ombe mzuri watu wamuone.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, nilikuwa na shamba zuri la michikichi kuliko raia ye yote na nilimuuzia Ndugu yangu Kilontsi. Nilipokuwa Morogoro, eka moja ya mpungu nilikuwa napata gunia 42, wa kwanza katika Mkoa na vyuo wanakuja kujifunza kwangu. Leo, ingawa wengine wanatukejeli, nataka Washimiwa Wabunge mjue kwamba Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa na Tanzania kwa ujumla ukiuliza ng'ombe mzuri, utaambiwa nenda utamkuta kwa Mzindakaya, ng'ombe mzuri. Ukitaka shamba zuri la ngano, nenda kwa Mzindakaya utalikuta kwa sababu mimi ni mkulima, naongoza wakulima. Sasa nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuibane Serikali na agenda yetu iwe moja tu, kuwawezesha wananchi, uwezeshaji!

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunapitisha Bunge hapa trilioni saba kati ya hizo trilioni nne zitakuwa za matumizi na miradi fulani fulani, zote zitakwenda kwa familia tisa tu za Tanzania. Najua familia tisa ndiyo zinamiliki utajiri wa nchi yote hii, sisi Wabunge tunachomana mikuki sisi kwa sisi. Tuombe uwezeshaji, Waheshimiwa Wabunge ndiyo iwe agenda yetu. Undeni makundi ya kudai maendeleo, undeni *club* mionganoni mwetu za kuzungumza maendeleo kuliko kutafutana roho, haitusaidii. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunaanza kupata sifa ya *critics* ambapo tulikuwa na sifa ya kuwa *quite, positive, ukipita* kwenye *corridors* watu wanatetana tu,

haliwezi kuwa Bunge hilo, Waheshimiwa Wabunge siyo kutetana ni kuzungumza maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilihuzunika kidogo, aliposimama Mheshimiwa Dr. Mwakyembe kuzungumza habari ya Richmond. Waheshimiwa Wabunge, nataka niseme ukweli, kwa Kanuni na kwa heshima ya Mabunge, suala lile la *Richmond* lilishaisha na lilishafungwa kwa maana ya Bunge, tunachongoja, ni Serikali kuleta taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati Teule ya Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, haikuwa Kamati yake ilikuwa ni Kamati Teule ya Bunge. Ilipofanya kazi, ikalete Bungeni na Bunge likapitisha, si Mheshimiwa Dr. Mwakyembe na Kamati yake, ni maamuzi na maelekezo ya Bunge. Sasa ili kuonyesha kukomaa, inatakiwa jambo hili tuliache kulijadili hapa Bungeni, tingoje utekelezaji kutoka Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naiomba Serikali itupe taarifa kuhusu mambo yanayoandikwa juu ya Rais Mstaafu, Mheshimiwa William Mkapa. Mheshimiwa Rais Mkapa, ana sifa kubwa sana duniani, ameijengea heshima nchi hii, anaandikwa hovyo tu na Serikali mnanyamaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikutana na watu wa Kimataifa wanasema *you people*, wewe Bwana Mzindakaya, hata mkimtukanaje Mheshimiwa Mkapa, sisi tutaendelea kumtambua. Halafu hapa watu tunapiga kelele, sitaki kuwataja wakubwa ambao wana kampuni zao, wakubwa wote wa Amerika na Ulaya wana makampuni kule Arabuni, yanafanya kazi lakini katika hili, tunataka Serikali itueleze, kwa nini kiongozi wetu wa heshima, aliyeijenga heshima nchi hii, nyumba hii tunayokaa Waheshimiwa Wabunge, ni matunda ya Mheshimiwa Mkapa, Uwanja wa Taifa, ni yeye, kwa nini tunatumia Bunge hili kupakazana matope?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itsaidie kujibu, kutueleza ili tusiendelee kupiga kelele huko na kule. Sifa yetu ni kulinda na kuheshimu viongozi waliotangulia, nchi yetu ina sifa kubwa, aliyetangulia, aliyefuata na leo Rais Kikwete, akitembea popote duniani ana sifa, ukimpinga ni fitina kwako mwenyewe. Lakini ana sifa nzuri, ameanza vizuri, anaiuza nchi duniani, Tanzania inajulikana kupita kiasi, akitoka naye mtaanza kumuandika hivyo hivyo maana mmeanza tabia ya hovyo, hakuna heshima tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamuita Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim ajiandae na Mheshimiwa Halima O. Kimbau pia ajiandae.

MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza namshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa Jumatatu iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwanzo ambalo nataka na hili nataka Mheshimiwa Waziri Mkuu, alijibu mwenyewe siyo ijibu Wizara ambayo inahusika na suala hili, nalo ni kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar, hivi sasa, ni kitendawili. Kwa muda mrefu, inazungumziwa, inapigiwa kelele, yanaulizwa maswali Bungeni lakini taarifa ambazo zinakuja ni zilezile za kila siku kuwa itajengwa. Sasa itaanza lini kujengwa na tutegemee nini kutokana na maandalizi ambayo tayari yameshaandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, imetengewa bilioni 2.9 ambazo zitafanya kazi ya ujenzi lakini kwa kweli fedha hii, ni ndogo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar lakini ni mwanzo mzuri, tuanze, tuone ni wapi itafikia na baada ya hapo tuone hatua zitakazofuatia baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo nataka kujikita sana leo, ni suala la elimu yetu Tanzania. Kwanza nataka kulizungumzia hili ambalo tunalizungumzia kila mwaka ifikapo wakati wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera zetu za elimu Tanzania lazima tuziangalie na tuzifanyie marekebisho. Ukiingalia Sera ya Elimu ya Tanzania Bara na Sera ya Elimu ya Tanzania Zanzibar, ni vitu tofauti lakini tunawatahini wanafunzi ambao wako katika *level* moja. Ukiingalia Sera ya Elimu Tanzania Bara, inazungumzia kuwa watoto wataanza shule kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la saba na ni elimu ya lazima, ukiingalia Tanzania Zanzibar, hivi sasa wanaanza darasa la kwanza mpaka darasa la kumi, hiyo ni tofauti ya mazingira ya jinsi sera zetu zinavyotofautiana. Lakini hata hivyo, sera hizi zinatofautiana katika utoaji wa elimu lakini kuna hatua ambayo wanafikia wanakuwa sawasawa na mitihani yao inakuwa sawasawa vilevile lakini utofauti uko katika kukutana katika elimu ya juu, elimu ya msingi kila mmoja ana sera yake lakini elimu ya juu tuna sera sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo ambalo linatukuta Zanzibar ambalo naona ni chanzo cha kufeli watoto wengi, ni ule mfumo wetu wa elimu ulivyo. Kwa kweli si mfumo ambao unaweza ukasaidia sana wanafunzi wa Zanzibar kufanya vizuri katika mitihani ya Taifa ukilinganisha na Tanzania Bara. Kwa hiyo, elimu ya juu Zanzibar inakabiliwa na matatizo mengi sana, la kama hawataibadilisha, itakuwa na matatizo ambayo huenda ikasababisha watoto wengi kutokuwa na elimu bora. Kwa maana hiyo, sera yetu ya elimu, kwa kweli ni lazima tuifanyie marekebisho na kama hakuna marekebisho kwa kweli tutawasukuma watoto mpaka *Form Four* wakati ambapo hawana elimu bora, vifaa na mambo yanayohitajika katika elimu, ni kitu ambacho kwa kweli kinachangia elimu hiyo iwe siyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa Tanzania Bara, elimu ya msingi hivi sasa ni Darasa la Saba lakini kuna kundi kubwa ambalo wanafeli halina pa kwenda ambalo linamalizia Darasa la Saba, lazima tuitazame hali hii. Hivi sasa mtihani wa Darasa la Nne na mtihani wa Darasa la Kumi tayari umefutwa. Kwa hiyo, ipo haja tuiangalie hali hii kama ipo basi tuikebishe, tuhakikishe kuwa sera zetu zinakwenda sambamba na yale mahitaji ambayo tunaweza kuyahitajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia, ni suala la Chuo cha Mwalimu Nyerere. Chuo cha Mwalimu Nyerere, kwa kweli ni chuo kizuri sana, hivi sasa, kinatoa mafunzo na kinaanza na *degree* mwakani ambayo itasaidia watoto nchini Tanzania lakini chuo hiki kwa kweli kinakabiliwa na matatizo mengi yaliyopo pale. Mwaka jana, kimetengewa bilioni moja kuhakikisha kuwa kinafanyiwa ukarabati na mambo mengine ya maendeleo lakini katika kipindi hiki, hakuna fedha iliyotengwa katika chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo kile kinakabiliwa na matatizo ya ukarabati, kwanza, ni kibovu, hakuna mabweni ya wanafunzi ambayo yanakidhi haja lakini tunaongeza wanafunzi kila siku, kwa kweli hivi sasa ipo haja ya kuyafanyia marekebisho au kuyaongeza ili yaende na wakati tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu wakati huohuo, chuo kile kiko karibu na Bahari, kinaliwa na Bahari kwa hatua kubwa kweli kweli, mmomonyoko wa ardhi unakitafuna kile chuo katika upande mmoja wa Bahari. Ipo haja tukiangalie na tuhakikishe kuwa mmomonyoko ule uliopo unafanyiwa kazi ili kile chuo kisije kikaliwa na Bahari kwa muda mfupi tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalotaka kulizungumzia ni kwamba kile chuo kimetengewa bilioni moja kama nilivyosema mwanzo lakini bilioni moja hiyo hiyo itengeneze na chuo kilichopo Zanzibar na kuanzisha chuo kingine ambacho kitakuwa ni *campus* ya Chuo cha Mwalimu Nyerere lakini bilioni moja iliyotengwa sifikirii kama inaweza ikajenga chuo hicho. Kwa hiyo, nashauri kuwa ipo haja Wizara au Serikali, kuongeza bajeti ya chuo kile ili kuhakikisha kuwa inakidhi haja na kile chuo cha Zanzibar ambacho kinataka kuanzhishwa, ihakikishe kuwa nacho kinaanza mara moja kwa hatua za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia, ni kuhusu Baraza la Mitihani. Kwa kweli Baraza la Mitihani linafanya kazi nzuri sana lakini vilevile linafanya kazi katika mazingira magumu sana. Baraza la Mitihani kwa kweli lina changamoto nyingi sana ambalo linakabiliana nazo likiwemo la wizi wa mitihani tulio nao hivi sasa. Kwa kweli hivi sasa, wizi wa mitihani umeongezeka. Kama hatutafanya bidii kuhakikisha kwamba wizi wa mitihani unadhibitiwa, tutapata wanafunzi ambao hawapo katika kile kiwango kinachokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho kinasikitisha zaidi, tulipouliza swali hapa Bungeni kuhusu wale wanafunzi ambao wanazuiliwa kutoendelea na shule

kwa sababu ya kutokulipa ada au wakati mwingine kutokuwa na *progressive results*, katika suala hili, wanaoadhibiwa, ni wanafunzi ambao hawakufanya vitendo vile, bali vimesababishwa na Walimu Wakuu ambao ndio wanaoshughulika na mambo haya lakini wanasababisha wanafunzi wazuiliwe kufanya mitihani au wazuiliwe matokeo ya mitihani yao badala ya kuadhibiwa wale ambao wanahusika zaidi. Kwa hiyo, ipo haja ya kuliangalia suala hili ili tuhakikishe kuwa hatuwaadhibu wanafunzi ambao wazazi wao wanapata hasara kwa kutoa fedha nyingi lakini mwisho wake hawapati matokeo yao, vitu vinavyosababishwa na walafi wachache au wanaokwenda kinyume na maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia, ni kuhusu mitihani. Katika kuhakikisha kuwa mitihani inafika salama na bila wizi, wanatumika Askari Polisi. Askari Polisi wakati wanatumika, wasiwe ni wasimamizi wa mitihani bali wawe ni wasindikizaji kwa sababu unaweza kuwaathiri watoto kisaikolojia. Suala hili lipo ambapo katika baadhi ya vituo wanatumia Askari Polisi kusimamia mitihani. Naomba Askari Polisi, wailinde mitihani lakini wasiwe wasimamizi. Kwa hiyo, naomba hili suala nalo liangaliwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wanadai kuwa zile posho zao za kulinda hiyo mitihani zinachelewa au hazifiki kabisa. Kwa hiyo, kuna haja ya kurekebisha hiyo hali na kuhakikisha kuwa Askari Polisi ambao wanasimamia au kusindikiza mitihani wanapata posho zao mara tu wanapomaliza kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu Chuo cha *Science Marine* iliyopo Buyu. Hiki ni kilio cha muda mrefu, kilianzia Kaskazini, kikahamishiwa Buyu kwa miaka ambayo hivi sasa inafika ishirini. Kitu ambacho kinasikitisha zaidi katika suala hili kwa kweli na lazima Serikali iwe na uangalifu sana, kama uwezekano upo na uongozi wa Chuo cha Dar es Salaam, kuititia Kitivo cha *Science Marine* ambapo walikuwa na majadiliano mazuri tu na baadhi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Benki ya CRDB, wakafikia muafaka mzuri tu ili kuhakikisha kuwa fedha inayopatikana Sh.6.3m/= iweze kusaidia kile chuo kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, walifanya majadiliano mazuri na walifikia hatua nzuri lakini cha kusikitisha, maamuzi ya Wizara yalikuwa hayapo katika msimamo ambao ulikuwa unaweza kukisaidia kile Chuo kupata mikopo kwenye Mashirika ya Hifadhi ya Jamii au ile Benki kwa sababu ilikuwa tayari wameshafikia makubaliano. Lakini hawakufikia muafaka kwa sababu Wizara ilichelewa kutoa jibu kwa wakati na mpaka leo kile chuo kinasusua na hatujapata ufumbuzi rasmi wa kuhakikisha kuwa chuo cha Buyu kinafanyiwa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia, ni suala la *TCU (Tanzania Commission for University)*. Hii ni Taasisi ambayo inashughulikia mikopo ya wanafunzi. Wakati huo huo, wameiteua *Commission* hii kwa makusudi kabisa ili kushughulikia masuala ya mikopo lakini kuna malalamiko mengi kutoka kwa wanafunzi au wana madai yao lakini hii Tume haishughulikii ipasavyo. Wanafunzi wengi, wanasajiliwa katika Vyuo viwili kwa wakati mmoja na hili ni lalamiko ambalo lipo na ambalo linalalamikiwa kwamba wanafunzi wanajisajili katika chuo kimoja halafu

wanajisajili katika Chuo kingine wakati hii Tume ipo na wakati mwingine inaliona suala hili lakini inalifumbia macho. Kwa hiyo, ipo haja ya kuhakikisha kwamba baadhi ya wanafunzi ambao wanajisajili mara mbili wanachukuliwa hatua inayofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kitu kingine ambacho kinasikitisha, wanasema kuwa suala ambalo lipo katika hii mikopo, wale maskini ambao walilengwa hasa hawaipati ile mikopo wanapata wale ambao hawakulengwa na wanapata mikopo mikubwa na wale maskini wanabakia na umaskini wao uleule. Hili suala lazima liangaliwe ili kuhakikisha kuwa wale wanafunzi ambao wanalengwa kusaidiwa, ili wale maskini na wao waweze kupata elimu ya juu. Hili suala lipo, baadhi ya wanafunzi hawaipati ile mikopo, wanapata wale matajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia suala hili, sasa nazungumzia suala lingine kuhusu kivuko cha Kigamboni. Kwa kweli, ukiangalia kivuko cha Kigamboni kinasikitisha sana, kila siku kipo kwenye vyombo vyahabari kikionyesha jinsi watu wanavyosumbuka pale. Naishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kwa kuhakikisha kuwa kile kivuko kinaweza kufanya kazi hivi karibuni. Kulikuwa na mpango wa kuanza kufanya kazi mwezi wa Tano lakini hivi sasa wanasema kitamalizika mwezi wa Tisa, tunaomba kimalizike ili hili tatizo liondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kudumu au ufumbuzi wa kudumu katika tatizo hili la kivuko cha Kigamboni, si kutafuta kivuko bali kuhakikisha kwamba tunajenga daraja la kudumu, huu ndio utakuwa ufumbuzi wa kudumu. Kwa sababu tukisema tununue kivuko na kivuko hakipumziki, hakina *service*, nacho kwa muda mfupi kitaharibika, lakin tukijenga daraja la kudumu, litaondoa usumbufu wa muda mrefu kwa sababu hivi sasa Kigamboni si kisiwa, ni sehemu ambayo imeendelea sana, Kigamboni ya sasa si ile ya zamani. Kwa hiyo, kama hili daraja likijengwa na Serikali ikijikita katika suala hili, nafikiri mafanikio tutayaona na wananchi watafurahi sana kwa kuona usumbufu huu umeondoka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia, ni hii lugha yetu ya Kiswahili. Kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisema Kiswahili kwa kweli hivi sasa kinakua na kinatanua mipaka yake na ni lugha ya Taifa ya Tanzania na ni lugha rasmi tulioichagua kuhakikisha kwamba tunapata mawasiliano mazuri na ni lugha yetu ya kutumia katika ofisi zetu. Lakini suala ambalo hivi sasa linaudhi na linakera, ni kuwa kile chombo ambacho kinaratibu shughuli za Kiswahili bado kiko nyuma sana. Hawana nyenzo, hawana ofisi, wanatumia kiofisi ambacho hivi sasa kwa kweli hakikidhi haja, hawana nyenzo za utafiti, hawana wataalamu, sifirkii kama hicho Kiswahili kinaweza kukua. Kwa hiyo, ipo haja ya kuliangalia suala hili, kama tunataku kukuza Kiswahili kiwe ni lugha ambayo imeenea na inapanua mipaka yake na hivi vyombo vilivyopo tuhakikishe kuwa vinafanya kazi ipasavyo na kuondoa yale matatizo madogo madogo yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu bila matatizo kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala*, aliényiwezesha kuwa mzima na mwenye afya njema wakati huu nikichangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niende moja kwa moja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 74, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu. Ustawishaji wa Makao Makuu, ni pamoja na kujenga maelewano na ushirikiano ndani ya eneo husika la Dodoma na wakazi wake kwa ujumla. Inasikitisha, inasononesha na inaumiza sana kuona jinsi wananchi, wakazi wa Mji Mwema, Chang'ombe walivyofanyiwa na *CDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa walibomolewa nyumba zao, zaidi ya nyumba mia na hamsini zilibomolewa na baya zaidi wananchi hawa hawakupatiwa mbadala wa kupatiwa nyumba nyingine, wameachwa wakitangatanga kutoka sehemu moja mpaka nyingine na wale walio na huruma basi angalau wanawachukua kuwahifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya *CDA* wanayoisema ni kwamba, hawa ni wavamizi, hili si kweli! Kuna wazee pale mfano Mzee Antene Mbatiani na Mzee Mkuyu Mbatiani, wapo pale hata kabla ya uhuru wakiwa na makazi yao, wakiwa na makaburi yao, nyumba zao za ibada lakini wapo wengine wamejenga pale kabla ya mwaka 1977, *CDA* ilipoanzishwa. Sasa wanaposema kwamba, hawa wamevamia, sisi hatujui uvamizi huo, kama ingekuwa ni magari yamekuja usiku yakafika mia mbili au mia tatu, ungesema wamevamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu na tuwaulize hawa *CDA*, hivi tangu mwanzo ambapo wameanza kutayarisha matofali, *CDA* walikuwa wapi? Walipoanza kuchimba msingi, kujenga hadi kufikia nyumba mia na hamsini, *CDA* walikuwa wapi? Maana uvamizi unatokea pale ambapo asubuhi tu umeamka, unazikuta nyumba lakini huu haukuwa uvamizi. Nafikiri *CDA*, haikuwatendea haki wananchi hawa wa Mji Mwema na Chang'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamevunja maeneo mengine ya Mbwanga Juu, Kizota na nasikia wana mpango wa kuvunja tena maeneo ya Chinyoya, Mbuyuni na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hili ni tatizo hapa Dodoma na ni kero na hawa wananchi ni wakazi wa hapa hata kama wangkuwa ni wakimbizi kuna taratibu zake za kuwahamisha, lazima kuwe na maelewano na ushirikiano, huwezi kusema niwaondoe haraka haraka, kuna siri gani iliyojificha? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema ni lazima tuandae utaratibu ambao kwa njia moja au nyingine, wananchi hawa wafikiriwe angalau kupatiwa sehemu nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baya zaidi wakati zoezi hili likiendelea, Polisi walitumika vibaya. Wananchi walihoji uhalali wa kuondolewa, baadhi ya wananchi katika kuhoji kwao wakati wakihojiwa na walipokuwa wakihoji walipigwa. Hivi jamani, nchi hii mtu anahoji uhalali wa kuondolewa pale alipo, anapigwa!! Utamwondoaje mtu katika eneo lake asikuhoji? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna wengine mbali ya wale ambao walipigwa ambao ni vijana, kuna tendo moja ambalo ni baya zaidi, mama mmoja ambaye alikuwa amejifungua kwa *operation*, ana kichanga cha siku ishirini, yaliyomkuta, anajua Mwenyezi Mungu. Nashangaa sana kama Polisi hawajui kuzaliwa. Kila mtu amezaliwa, anajua umuhimu wa mama. Hivi mtu amejifungua kwa *operation*, akiwa na mshono na kichanga cha siku ishirini, unamfanyia vitendo ambavyo havielekei, hii kweli ni halali jamani? Tatizo hili lililopo hapa Dodoma, linaumiza watu na linasikitisha sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata pale unapoeleza kwamba nahitaji kiwanja, urasimu umekuwa mkubwa. Inavyoolekea utaratibu wa hivi sasa, wanaoondoka ni maskini baada ya muda maeneo haya watapewa wenye nacho. Sasa ikiwa Ustawishaji wa Makao Makuu, ni kwa matajiri, tuambiwe kwamba maskini hawana haki hapa Dodoma. Haiwezekani hata kidogo wananchi wale wanaomba viwanja lakini wanaambiwa subirini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini na wao vilevile *CDA*, wanalamikiwa na wananchi, kuna taarifa ambazo tunataka pia tuzifanyie kazi, wao wanaondolewa lakini wakati huo huo na wao wanamiliki viwanja zaidi ya vitatu, wanalamikiwa na wananchi na wananchi watasema kutokana na hasira zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwanza, Serikali iunde Tume ya kuchunguza kero hizi za bomoa bomoa zinazoendelea hapa Dodoma.

La pili, ninashauri Serikali yale maeneo yote ambayo yamevunjwa basi waliovunjiwa wapewe fidia, wakopeshwe na wapimiwe maeneo yaleyale, wajenge hiso nyumba ambazo *CDA* wanazihitaji kwa sababu na wao wanahitaji kujenga lakini umaskini unawakabili. Hili lilikuwa ni suala langu la kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni maslahi ya wafanyakazi na wastaifu. Maisha yamekuwa magumu, bei za bidhaa zimezidi kupanda, hazishikiki, mchele umekuwa bei ghali, maharage na sukari lakini hata saruji pamoja na mabati, vyote bei ziko juu. Kutokana na hali hii, tunayokwenda nayo, kuna haja ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi wetu pamoja na kwamba hivi karibuni tunaambiwa kwamba mishahara inaongezwa lakini bado kulingana na ukali wa maisha kuna haja ya kuangalia kwa dhati kabisa ni jinsi gani tutaboresha maisha ya wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ni suala zima la wastaafu. Tuliambiwa hivi karibuni kwamba mstaafu analipwa pensheni yake ya kila mwezi Sh.21,600/=. Hizi fedha, ni kidogo ingawa tulipewa matumaini kwamba huenda hizi fedha zikaongezwa. Nataka niseme tu wastaafu wetu wapo katika hali mbaya na ya hatari sana, kuna haja ya kuwafikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo ambalo kidogo lililikuwa linaniumiza, ni majibu ambayo tumeyapata hapa Bungeni hivi karibuni kwamba, kuna wastaafu 6339 waliokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hawajachukua hundi zao. Wakati Serikali ikitujibu, walisema majina haya yapo katika magazeti, ndiko yanakowekwa lakini mwananchi wa kijiji magazeti hayapati. Hivi ni kweli Serikali ndiyo iwe na jibu hilo tu kwamba majina ya wastaafu yako katika magazeti, hiyo itoshe? Naishauri Serikali kwamba, itayarische vitabu maalum ambapo majina yote ya wastaafu wa Afrika Mashariki yatawekwa tugawiwe sisi Wabunge kama watumishi wa wananchi, twende huko tuwasiliane nao. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kuna haja na ni vema kuenzi wastaafu wetu wakati huu wakiwa katika hali ngumu ya maisha. Kumezuka mtindo mara nyingi na kila wakati tunasikia sifa ambazo mstaafu anazipata pale ambapo anafariki dunia. Kumtunza kwa risala nzuri ya kutoa machozi, simanzi na majonzi wakati ameshakufa, huko si kumtunza. Mara ngapi tunasikia, marehemu alikuwa shupavu, hodari, jasiri, mwaminifu na mtiifu, yeye ni mfano wa kuigwa, atakumbukwa, atathaminiwa kwa kazi yake nzuri aliyoifanya, hakuthaminiwa wakati alipokuwa hai ambapo alikuwa akipewa Sh. 21,601/= kama pensheni yake kwa mwezi, wastani wa Sh. 720/=. ni ili anunue pipi? (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sielewi kumtunza kama huku inakuwaje kwa sababu akiwa hai hatukumjali, amefariki unasoma risala ya majonzi wakati ameshakuwa kaburini, mtu akiwa kaburini hasikii lolote. Tunasubiri mtu afe ili tuandae mazingira ya kumsifu, mambo haya, tunayo Tanzania. Nafikiri kuna haja ya kwenda sambamba na wale waimbaji waliosema ‘mpende bado yuko hai, usimpende akiwa kaburini, ukimpenda akiwa kaburini...’nawaachia wenyewe Serikali mmalizie. (*Makofit/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dhana nyingine ambayo kidogo haipendezi, mara nyingi tunapajaribu kuwatetea wafanyakazi, Serikali imekuwa na majibu mazuri ya haraka haraka hapa Bungeni. Jana nilikuwa nikisikiliza sana jinsi ambavyo Mawaziri walikuwa wakijibu maswali, ni majibu ya matumaini na wananchi wamekuwa wakituambia kwamba ni kweli tuna matumaini makubwa. Mara nyingi tunasikia hapa Bungeni tukijibiwa, Serikali ni sikivu, imesikia kilio cha Mheshimiwa Mbunge, nia ni njema, mipango kabambe iko mbioni, Mheshimiwa Mbunge avute subira hadi mchakato utakapokamilika, haya ni majibu tuliyoyazoea hapa Bungeni. Nafikiri kwa vyovyote iwavyo, hii mikakati itoshe, tuangalie namna gani ya kuweza kuboresha maslahi ya wafanyakazi wetu pamoja na wastaafu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2007, kwa

upande wa wastaafu, inatisha. Katika majalada 7014 yaliyokaguliwa, majalada 514 yamelipwa pungufu kwa Sh. 416m/=, ina maana hata Serikalini nako wataalamu wa kutosha hawapo, huo ni mwaka mmoja tu wa 2006/2007. Wastaaafu 514 wangelipwa pungufu Sh. 416m/=. Kinachonipa tabu, ni kimoja tu, ina maana hiyo dosari imekutwa ndani ya mwaka huo mmoja je, mwaka 2005 mpaka 1980 ni kiasi gani wastaafu wamepunjwa? Ushauri wangu kwa Serikali, ihakiki majalada yote ya wastaafu kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 1980, yaani kwa ushahidi huu, ina maana wastaafu wengi wamepunjwa. Hii ni hatari na sijui kama ni kweli tuna wataalamu wa kutosha au kunakuwa na makusudi, sielewi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, katika kuwaenzi wafanyakazi wetu, tumekuwa tukipiga kelele sana hapa Bungeni kwamba kulingana na hali ya ujambazi ilivyo, kuna haja ya kuwalinda Askari wetu, wapate vifaa vile vya *bullet proof vest* lakini cha kushangaza, tumekuwa tukipiga kelele mara nyingi lakini hili bado halifanyiwi kazi. Tumekuwa tukisema mara nyingi kwamba angalau maeneo ambayo ni nyeti wakati wa doria za usiku na katika mabenki, ni hivi karibuni tu, tumeshuhudia au kusikia katika vyombo vya habari, Askari anapigwa risasi, mbwa anapigwa na mwaka jana Mwanga kule *NMB*, nako alipigwa risasi, lakini tumesubiri mpaka amepigwa risasi afe, tuandae risala ya kumuenzi, atakumbukwa daima milele, kwa kweli kuna haja ya kuwafikiria sana askari wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije katika suala zima la matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, za mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, kuna mishahara ambayo haikulipwa na haikurudishwa Hazina, kwenye Halmashauri ishirini na nane, fedha zenye jumla ya Sh. 482,703,896/=, huu ni msiba mkubwa. Huu ni ujisadi na hawa ni mafisadi. Huu ni ujisadi kwa sababu ikiwa Halmashauri 28 hizi na tumekuwa tukisema sana hapa Bungeni, hivi kuna hatua gani zinazochukuliwa kwa hawa Watendaji wa Halmashauri wanaotumia vibaya fedha za Serikali? Lakini mara nyingi tunaambiwa vuteni subira mambo yako mbioni. Labda niseme tu kuna haja ya kuangalia kwa makini sana tatizo hili la matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kwa haraka haraka, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanaotetea sana Walimu. Walimu wana kazi ngumu na hasa Walimu ambao wanapelekwa katika maeneo ambayo yako katika hali ngumu kama Mikoa ya Mara, Kigoma na Rukwa, mara nyingi tunasikia walimu hawataki. Kazi hii ni ngumu na wale ambao wanawalalamikia Walimu, waelewe neno lenyewe la Ualimu ni ugumu. Neno lenyewe *U* ni usumbufu, *A-* maana yake ni kazi ya adha, *L-* maana yake ni kazi ya lawama, *I-* ni Inda na Ikirari, *M-* ni kazi ya mahangaiko na masumbuko, *U* ya mwisho ni uvumilivu ndiyo maana ya kazi ya wito. Sasa wale ambao wanaona Walimu wanapata mafao makubwa zaidi, neno lenyewe tafsiri yake ni ugumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wale wote ambao kwa njia moja au nyingine, wanatetea sana Walimu. Naomba niseme tu, katika hali hii tunayokwenda nayo, kuna haja ya kuhakikisha

tunawaenzi na kuwatuunza Walimu wetu vizuri ili na wao wajisikie kwamba wanafanya kazi katika hali iliyo nzuri na wajue kwamba hatima yao ni njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache niliyosema, nafikiri Serikali imesikia kilio na machozi yangu, nina imani wakati Waziri Mkuu akifanya majumuisho, atayafuta, nashukuru sana. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Kuhusu utaratibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1)(a), sikupenda kuingilia mtiririko wa mjadala wa Mheshimiwa Mbunge lakini sasa nataka kusema kwamba alitoa tuhuma nzito sana dhidi ya Askari Polisi waliokuwa wakisimamia shughuli za ubomoaji uliokuwa unalenga kusaidia ramani kabambe ya Mji wa Dodoma isiharibike na Kanuni hiyo inasema kwamba:-

“Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli”.

Alisema kwamba Askari Polisi waliwanyanyasa raia ikiwa ni pamoja na mzazi aliyekuwa na kichanga cha siku ishirini. Taarifa tulizonazo sisi ni kwamba, Askari Polisi walikuwepo wakati wa zoezi hili lakini hawakugusa raia yeyote. Sasa tunaomba angalau atupe jina la huyo mama ambaye alikuwa na mtoto wa siku ishirini na yeyote yule ambaye amenyanyaswa, taarifa tulizonazo ni kwamba Polisi hawakumgusa raia yeyote, la sivyo afute usemi wake ule.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, dawa nzuri ni kuleta haya majina unayoyafahamu kusudi waweze kupata ushahidi unaostahili kwa sababu tukisema jumla jumla hivi watakapoanza kutafuta majibu, watashindwa kujibu. Kwa hiyo, tukiwa na majina rasmi, ni nani, binti nani, lini, ilikuwa wakati gani, itakuwa vizuri kwa wao kuweza kujibu.

Mheshimiwa Mbunge, nadhani utafanya hivyo mchana wa leo kwa sababu kesho wanaanza kujibu. Kwa hiyo, kesho utatoa majina ya hao watu unaosema ili kusudi kesho Mheshimiwa Waziri Mkuu, aweze kulifanyia kazi suala hili. Nadhani kulikuwa na majina, alete tu majina kwa Waziri wa Nchi, kusudi atakapotafuta majibu, wapate maelezo haya, utawapa wakati unaofaa.

Tunaendelea Mheshimiwa Halima Omari Kimbau.

MHE. HALIMA O. KIMBAU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nipate nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu aliye niwezesha leo kusimama tena hapa ndani ya Bunge ili kuweza kuchangia baada ya kupata matatizo katika Bunge letu la mwezi wa Pili.

Pia napenda kuchukua nafasi hii, kuwashukuru wale wote ambao kwa njia moja au nyingine, walichukua nafasi yao kunihudumia kuanzia hapa Dodoma mpaka Dar es Salaam, mpaka leo hii ambapo bado naendelea na matibabu ninayoendelea nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kuishukuru familia yangu, akiwemo mume wangu na watoto wangu ambao kwa kweli walipata tabu sana wakiniona katika hali niliyokuwa na leo wanashukuru na wanawashukuru wale wote waliokuwa pamoja na mimi kwa kuwasaidia kumweka mama yao katika hali iliyosababisha niwepo hapa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri walio chini ya Wizara yake, Manaibu Waziri, kwa hotuba yao nzuri ambayo nami leo napata nafasi ya kuichangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote mazuri na naiunga mkono mia kwa mia, ninayo mambo machache ya kutaka kuongelea juu ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitaanza kwenye suala la kilimo. Tunaishukuru Serikali kwa kutambua umuhimu wa kilimo na kuiongezea bajeti na hii siyo mara ya kwanza kutambua kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa nchi yetu. Lakini naomba sana hebu turudi, tuangalie huko nyuma, tangu tumeanza siasa ni kilimo, tumekuja na mengi mengi hapo katikati lakini tukifanya tathmini tumepiga hatua kweli ya kutosha kwenye suala zima la kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuangalia hiyo, ninashauri, tunazo kambi za JKT ambazo sasa hivi wengi wao, ukiondolea mbali elimu wanayopewa ya Kijeshi, lakini pia wanalima na kufuga. Tukiacha kambi hizo, hivi kama tukishirikiana kama tulivyoshirikiana kwenye elimu kuanzia kwa wananchi wenyewe, Halmashauri zetu, Serikali za Mikoa, Serikali Kuu, tunashindwa kuanzisha kambi za kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema kambi za kilimo, nina maana gani? Tunajua kwamba tuna vijana wetu wengi tu ambao hawana kazi na ni wakulima na wana nguvu lakini waanzie wapi? Unawachukua vijana unawarudisha Mbeya, nimesikia kuna wazururaji 76,000 Mbeya, nasema hawa si wazururaji *in such* lakini hawajui cha kufanya, nguvu wanazo, uwezo wa kuanza shughuli hawana!

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi tunayo safi tu, nina hakika wataalamu wetu wa udongo wanajua wapi tunaweza tukapanda nini. Sasa hebu tujaribu basi, tujaribu tukishirikiana na wote kama nilivyo sema kuandaa kambi za kilimo, tuwawezeshe vijana wetu hao, tuwaweke pamoja kama tunavyofanya watoto wetu kwenda shule za msingi na kwenye shule za sekondari, tuchukue vijana angalau wa mfano. Tuanze kwa mfano,

mimi ninajitolea na naamini Mkuu wangu wa Mkaoa Mheshimiwa Dr. Ishengoma, akiwa ni mtaalamu wa kilimo, atakubaliana nami, ndani ya Mkao wetu wa Rufiji, tunayo ardhi. Hebu tupatiensi idadi kadhaa ya vijana, tuwawezeshe kwa mambo matatu. Kwanza, mahali pa kuishi, hata ma-*dormitory* tu kama vile tunavyowawezesha watoto wa sekondari, tuwape chakula kama tunavyowawezesha watoto wa shule, tuwape nyenzo, kwa maana ya pembejeo zote za kilimo, tuwape na utalaam na tuwasimamie, tuone matokeo yake yatakuwa ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tusiishie hapo tu, nashauri pia yale maeneo ambayo watayatumia, kila mmoja agawiwe la kwake na hatimaye amilikishwe ili baadaye awe na maisha mazuri yale tunayoyaongea ‘Maisha Bora kwa kila Mtanzania’. Najua inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa kuna mikopo, tunashukuru tuna Wahisani mbalimbali na nina hakika watakuwa tayari kutusaidia kwenye hili. Mimi naomba sana hebu tujaribu, inawezekana kabisa tukajikomboa sisi kwa upande wa chakula na kiuchumi, lakini pia tukawasaidia vijana wetu kupata ajira ya kudumu na maisha bora ambayo kila mmoja anatakiwa kuyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hao vijana wakikopeshwa, nina uhakika wakisimamiwa vizuri na wakipatiwa vifaa, wataweze kurejesha mikopo hiyo na nina uhakika kwa hali ya sasa hivi ya mahitaji ya chakula, wanaweza wakauza na wakapata fedha na wakawenza kulipa madeni na hatimaye na wenyewe wakapata fedha za kuweza kuwafanya kuishi. Kwa hilo, naona niliachie hapo. Ninaamini, Serikali ni sikiu inaweza ikafanya jambo hili kwa majoribio. Nina uhakika, Mkao wa Pwani, tutakuwa tayari kujitolea eneo na vijana kuja kuanza kufanya hiyo shughuli kwa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nataka kuongelea suala la elimu. Tunaipongeza sana Serikali, wananchi na Halmashauri zetu kwa kufanya kazi nzuri kabisa ya kuandaa shule za msingi na shule za sekondari. Tatizo ambalo sasa hivi bado linatukumba na jitihada ya Serikali bado halijalifikia ni kuweza kupata Walimu wa kutosha, kwa kweli hili ni tatizo. Sasa mimi nimekuwa nikijiuliza, hivi kweli kama tunapata misaada ya mambo mbalimbali, kama tunaweza tukaajiri watu kwenye fani mbalimbali, nitatoa mfano wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, leo ukienda hospitali ya Mkao wa Dodoma kuna Wachina, ukienda wapi sijui, utakuta kuna Wa-Cuba, ukienda kwingine, utakuta kuna Waarabu, wote wanakuja kutusaidia katika masuala ya afya, hivi Serikali kuititia Wizara zinazohusiana na masuala hayo, tunashindwa sisi kupata msaada wa Walimu kwa njia yoyote ile wa kuja kutufundisha watoto wetu wakati sisi wenyewe tukiwa tunaendelea kuijandaa kukamilisha lengo la kupata Walimu wa kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale wenzangu ambao tulisoma wote, ninakumbuka tukiwa Tabora, tulikuwa na Walimu kutoka Marekani, nawakumbuka wawili tu Isramack, na baadaye akaja Miss Jego, hao watu walitufundisha sisi, sasa leo wako wapi? Au kuna kigugumizi gani cha kuwaomba hata majirani zetu Kenya na Uganda ambao nina uhakika wana Walimu wa kutosha na wazuri tu, kwa haya haya masomo matatu ambapo ni tatizo kuwapata Walimu? Tukawaajiri hata kwa mikataba ya

miaka miwili, mitatu, ili watoto wetu waweze kupata elimu bora si kwenda kukua shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi utakuta mtoto amemaliza Kidato cha Nne hajui kitu, anajua kusoma na kuandika, *well and good* lakini ukimwambia akuandikie barua ya maombi ya kazi, utashangaa. Ni wachache sana ambao wanaweza kujieleza kwa ufasaha kabisa kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaiomba sana Serikali, irudi kuangalia siku zilizopita, kwenye mafaili yetu, ni nchi gani marafiki ambazo zinaweza zikatusaidia Walimu na ni nchi gani marafiki wanaweza wakatupa Walimu tukawaajiri kwa gharama nafuu na kwa mikataba ambayo ni laini ili na sisi watoto wetu waweze kupata elimu ambayo ni bora wawapo shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano wa shule moja mzuri sana. Kwa wale ambao wamekuja Mafia na wakafika katika kijiji cha Bweni, kuna shule ya sekondari ya *standard* ya Kimataifa na ninawashukuru wale wote waliochangia kutuwezesha kupata aina ya shule hiyo ndani ya Wilaya ya Mafia lakini utashangaa Walimu hawatoshi. Hali ya shule, ni nzuri tu, lakini bado Walimu wa kutosha kuweza kufundisha watoto wale, hakuna. Taarifa za haraka haraka nilizonazo, wanasema hata hivi sasa baadhi ya wanafunzi wanaanza kuihama shule hiyo. Sasa hebu angalia jitihada zote za wenzetu waliotuchangia kuanzisha shule nzuri, yenyе *standard* nzuri, inaishia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tena sana pamoja na ujenzi huo wa shule unaoendelea, hebu na wenzetu watutafutie Walimu popote pale waje wa-*cover* hizo nafasi kwa muda, siyo kwa maisha yote, ni kwa muda mpaka hapo sisi wenyewe tutakapokuwa na Walimu wa kutosha, kama tunavyofanya kwenye Idara na Wizara zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya matatizo mawili kwenye suala la elimu na kilimo, ni kutokana na wingi wa watu tunavyoongezeka Tanzania. Ukichukua mwaka 1961 baada ya kupata uhuru, tulikuwa milioni tisa, leo tupo milioni thelathini na kitu. Tunazaliana kwa kuwa tunapata huduma safi, watoto wanaishi wengi kwa pamoja na kutokana na kwamba uzazi unakuwa kidogo na matatizo, tunapoteza wajawazito na watoto lakini bado tunaongezeka kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala la uzazi wa mpango, ninaiomba pia Serikali ilichukulie suala hili kwamba ni suala zito, tusilionelee tu kijuujuu, uzazi wa mpango, nyota ya kijani. Jana nilimsikia Mheshimiwa Mbunge mmoja akisema wengine wanasema hawaijui nyota ya kijani, wanaijua nyota nyeupe. Sasa hebu tufike mahali tuichukulie hii nyota ya kijani, ni jambo ambalo inabidi sisi tulihamashe kama tunavyohamasisha kuhusu UKIMWI. UKIMWI unatuua lakini uzazi usiokuwa na mpango unatupa matatizo ya elimu, ya kilimo, ya afya na ya chakula na mambo mengine mengi. Sasa tufanye zoezi maalum la kuwahamasisha watu kujua suala la uzazi wa mpango ambao utawafanya wazae kwa wastani ili waweze kuwatanza watoto vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nitakuwa sijatenda haki, kama sitaongelea suala zima la uvuvi. Bahati nzuri pamoja na uwakilishi wa Wanawake, lakini ninaishi Mafia kwenye Kisiwa ambacho moja ya kazi ambayo tunaifanya, ni uvuvi. Bahati nzuri tunaishukuru Serikali yetu kutulinda kwa kutuvekea mambo mawili mazito. Kwanza, suala la *Marine Park* ambayo ipo Mafia lakini pia suala la kutunga sheria kuacha kutumia nyavu ndogo. Kwa kweli, ninaishukuru mno Serikali kwa hayo mambo mawili ambayo yametusaidia sana Mafia kuweza kupata samaki waliotulia na samaki ambao wanahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nashindwa kuelewa nini tatizo kati ya Wizara, Idara ya Uvuvi Mafia, Mkurugenzi mwenyewe wa Mafia, Madiwani kwa maana nikiwemo na mimi mwenyewe na wananchi wa Mafia, kwa nini mpaka sasa hivi hatufikii muafaka? Sheria imesema mwisho wa ukubwa wa nyavu za kuvulia samaki, ni inchi mbili *unless* ni uvuvi maalum lakini bado Mafia unakuta wananchi mpaka leo wanaendelea kuvua samaki kwa kutumia nyavu za inchi moja na nusu, kwa kibali cha nani, hatujui!

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukirudi nyuma, tulipata Waraka kutoka Wizarani kwamba leseni zote zilizokatwa ambazo wanavua samaki kwa nyavu za chini ya inchi mbili zilirudishwe na kuanzia sasa wasizitumie lakini bado unakuja kupata maelezo mengi, wanasema Mkurugenzi amewaruhusu wavue mpaka mwezi Juni, 2008 kwa kutumia nyavu hizo za inchi moja na nusu. Mara tena unasikia Mkurugenzi ameomba kwa maandishi waongezewe muda mpaka mwezi Desemba, 2008, waendelee kuvua samaki kwa nyavu ambazo si sahihi. Sasa *which is which?* Sheria au Mkuu wa Idara kwenye Wizara au Mkurugenzi wa Halmashauri au Baraza la Madiwani au wananchi ambao wanatakiwa kuitekeleza hiyo sheria? Mwenye kosa ni nani? Baadhi ya wananchi, tumewaadhibu wameacha kuvua samaki kabisa, lakini baadhi ya wananchi Mafia wanavua samaki kwa nyavu ambazo zipo nje ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi wanasiaya tunapata tabu sana jinsi ya kujibu maswali. Tunakaa kwenye Baraza la Madiwani, tunaagiza Halmashauri ichukue hatua mara moja, Mwanasheria wa Halmashauri anaeleza vyake, Mkuu wa Idara ya Uvuvi ndani ya Halmashauri anaeleza vyake, hatimaye Mkurugenzi anaandika barua ya kuomba muda kuongezwa ili watu waendelee kuvua samaki kwa nyavu ambazo haziruhusiwi, hivi tunafanya nini? Mimi kwenye suala zima la uvuvi Mafia, sielewi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho, kwenye suala la uvuvi, bado ninaiomba Serikali yetu, iwaangalie wavuvi kwa jicho la huruma. Mpaka sasa hivi wanapoambiwa wavuvi wasivue samaki kwa nyavu hizo, hizo nyavu nyingine zinazotakiwa zipo wapi za kutosheleza mahitaji hasa? Kwa sababu leo ukienda Mafia, utakuta watu wamezagazagaa tu. Tunaishukuru Rumaki na Maseko wamewasaidia wavuvi, lakini hata kwenye kuwasaidia huko, kuna baadhi ya nyavu zilizonunuliwa kupitia msaada wa Rumaki, ni nyavu ambazo hazifai. Sasa hizo nyavu za ukweli kama wanavyopewa mbolea ya ruzuku na wanavyopelekewa majembe na matrekta na

kadhalika, je, hawa wakulima wa baharini, mimi siku zote nasema ni wakulima wa baharini, ambao ni wavuvi, wanasaidiwa kwa kiasi gani? Ninaomba wavuvi waangaliwe kwa sababu leo Mafia ukiondoa uvuvi, kilimo si kilimo, hakuna kilimo cha kuweza kutosheleza kusema Mafia watalima, Mafia kama Kisiwa, tunavua samaki.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. HALIMA O. KIMBAU: Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni kengele ya pili, narudia kusema naunga mkono hoja hii, naamini haya niliyoyaongea, yatatiliwa maanani wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anahitimisha hoja ya Wizara yake, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima Kimbau, ahsante.

Sasa nitamwita Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud na Mheshimiwa Abdul Marombwa, ajiandae na Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu pia ajiandae.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 99 kwa sababu zikiwa 100 haina faida ya kusimama hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa TAMISEMI, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzia kilimo. Kilimo tunasema ni uti wa mgongo wa nchi yetu lakini bado tunawazungumzia wakulima wadogo wadogo. Ukweli nchi inayotoa kipaumbele kwenye kilimo, inakuwa na wakulima wakubwa, sasa sijui lini tutakuwa na wakulima wakubwa ili waweze kutupeleka huko tunakotaka kwenda kwa sababu azma hii tunayo muda mrefu, wakulima tunao muda mrefu, lakini hatujawawezesha wakawa wakulima wakubwa. Ukweli, kilimo ni kazi kama kazi nyingine, inatakiwa ithaminiwe, itukuzwe ili iweze kuleta tija nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuamua kutenga baadhi ya Mikoa isiyopungua nane kwa kuipa kipaumbele katika kilimo. Sasa ninashauri kipaumbele hiki kiwe na manufaa. Kama tunatoa kipaumbele basi kiwe na manufaa ili uwe mfano kwa Mikoa mingine itakapopewa kipaumbele hicho ili ifanye zaidi ya Mikoa hii nane iliyotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kinalingana na mifugo. Tukiangalia mifugo, utakuta mifugo tunayo, lakini tija yake siyo kubwa kama inavyofikiriwa. Kwa baadhi ya makabila, mifugo ni kitu kikubwa sana. Huwezi kutambuliwa, kama mtu huna mifugo, huwezi kupewa mke kama huna mifugo, huwezi kupata lolote kama huna mifugo lakini tunavyoichukulia sisi mifugo kama ni kitu cha kawaida tu ambacho nikimnukuu

Mheshimiwa Rais alisema mchungaji anakonda, mifugo inakonda, hujui hata tija yake inayopatikana katika mifugo. Sasa ningeshauri tunapajaribu kutoa vipaumbele, tujaribu kutoa vitu ambavyo vitawasaidia walio wengi na tuondokane na kila siku kusema tuna wafugaji wadogo, tuna wakulima wadogo, hawa wanataka kuwezeshwa ili wawe wakubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kila baada ya muda, hutoa matangazo kuwaasa wakulima wasiuze mazao yao yakiwa shambani. Ukweli uamuzi huo ni vizuri lakini sisi Waswahili tunasema kimfaacho mtu chake, shida walizonazo, inabidi wafanye mambo ambayo hayastahiki na wanaamua kuza mazao yao yakiwa machanga. Sasa tuwawezeshe, tuwasaidie ili hao wadogo wadogo, wanawarubuni huku chini waachane nao lakini anapokuwa na shida, hana cha kumsaidia, anatokea mtu kumwambia nikatie eka moja, nitakulipa kiasi Fulani, anauza wakati bado mazao machanga, hata faida haipati lakini tatizo lake anakuwa amelitanzua. Sasa kwa hili, ninaomba tuwasaidie wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar ni kisiwa na visiwa vingi vinajientesha kwa viwanda, utalii na biashara. Katika hili, ninaomba sana Serikali ya Zanzibar ijitahidi sana kutaka kutafuta njia za kujikwamua kutokana na matatizo ya kiuchumi yaliyopo. Lazima tukubali, hata sasa hivi ninavyozungumza, hali ya uchumi wa Zanzibar siyo nzuri. Sisi wawakilishi wa watu, macho yetu yanaona mbali zaidi kwa sababu kila kukicha unakumbana na matatizo ya kimaisha. Sisi ndio watanzuaji wa matatizo ya kimaisha zaidi ya kimaendeleo katika Majimbo yetu, kutokana na umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hali ya uchumi siyo nzuri, Zanzibar walijaribu kutafuta njia za kujiondoa na umaskini uliokithiri, walitaka bandari huru, utalii, *Alhamdulilah*, inatusaidia, *EPZ* tunakwenda nayo hivyo hivyo lakini kulikuwa na jambo ambalo lilizungumzwa karibu miaka 10 au 12 iliyopita, ni suala la *OIC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili, lilipoletwa Serikali ya Muungano, ililitafakari kwa upana zaidi na ikaona faida zilizopo kwa kuingia katika mikopo ya *OIC*. Ukweli ni Taasisi ya Kiislam lakini haikopeshi Waislam tu na hata riba haina. Taasisi hii ina wanachama karibu 57. Katika wanachama 57 basi wanachama 20 ni nchi ambazo si Kiislam kama nchi yetu, naweza kukutajia mbili/tatu zilizopo karibu tu kuna Mozambique, Uganda, Mali, Benin, Chad, Cameroon, Burkinafaso na nyingine nyingi. Ukweli wanafaidika na mikopo ya benki hii ambayo wanaitumia bila ya kuwa na riba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachotaka kukizungumza pamoja na mawazo mazuri na kulikubali suala hili, Serikali ya Muungano iliwalishwa Serikali ya Zanzibar kwa sababu Zanzibar siyo nchi, hili halina ubishi wala halikataliki, mikataba mikubwa kama hii iingie Tanzania kama nchi. Sasa nilipenda njue pamoja na hayo yote, pamoja na hii faida ambayo ni mikopo iliyokuwa haina riba, Tanzania tumefikia wapi kujiunga na *OIC*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uboreshaji ya Jiji la Dar es Salaam, nashukuru kwamba viongozi wakuu wameuona Mji wa Dar es Salaam kwamba hali yake ni mbaya na Serikali imeamua kufanya marekebisho kwa Jiji la Dar es Salaam. Mimi nasema, ni wazo zuri, tuendelee nalo kwa sababu miundombinu ya Dar es Salaam, yote ni mibovu. Ukweli ikiwa kama kitovu cha nchi yetu pamoja na kuwa Dodoma ndiyo Makao Makuu ya nchi, lakini pale ni kitovu cha nchi yetu, ninaomba tuchukue hatua za haraka kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna masuala ya kutia aibu, haya masuala ya bomoabomoa, hivi ndio tuseme hii Miji yetu, haina Mipango Miji? Leo utasikia kumebomolewa huku, kesho huku, mfukuzano tu, watu wanalala nje, matokeo yake watu wanakwenda kulipwa fedha za walipa kodi, tunakwenda kuzilipa kwa watu ambao wamebomolewa lakini hatua zilizochukuliwa kwa waliofanya vitendo hivyo, hatuzipati, ziko vipi? Tunaomba hao waliosababisha hizo bomoabomoa ambazo hazina mpango, basi angalau tujue hatua walizochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, safari hii katamka na kuwatambua Madiwani kimaslahi, siyo kama hawatambuliwi lakini pamoja na haya ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, amshauri Waziri Kiongozi wa SMZ, salamu hizi zifike na Zanzibar ili Madiwani walioko Zanzibar, wanufaike kama Madiwani walioko Tanzania Bara. Wajihisi na wao wapo Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tusiseme Madiwani walioko Zanzibar, watashughulikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini hebu kaeni Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi kulitatua suala hilo. Ukweli wana matatizo na wanahitaji kupatiwa ufumbuzi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka sana, nataka nizungumzie feri ya Kigamboni. Feri ya Kigamboni inataka iangaliwe kwa jicho la huruma. Lakini pamoja na hiyo, kuna wafanyakazi pale Kigamboni ambao wanafanya kazi na Wizara ya Miundombinu wanaofungua mageti, wanaochana tiketi, wengi wao hawaaja jiriwa mpaka leo hii. Wako pale wana miaka sita mpaka miaka saba, hata kama ni majaribio, basi miaka saba bado hujamwajiri tu? Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba uliangalie suala hilo. Kama wanawahitaji basi wawaajiri kama hawawahitaji, wawaambie kwa sababu hakuna utu wa binadamu kama kujijua mimi nina kazi ya maana siyo *daily payed*. Sasa wale wako pale wamekuwa kama hawana kazi ya maana lakini kazi yao ni kubwa. Naomba Mheshimiwa Waziri hilo alitupie jicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nitawahi wenzangu wamezungumzia suala la Kadhi Mkuu. Ukweli Mahakama ya Kadhi, imefika wakati Tanzania iwepo. Hii itamhusu yule Muislam ambaye anadai haki zake zilizoko kwenye *Quran* kwa sababu masuala ya mirathi na mambo mengine, yote yameandikwa kwenye Kitabu Kitukufu cha *Quran* hukumu zake, haziko sambamba na Mahakama nyingine. Sasa suala hili tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, nalo aliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wengi wamezungumza suala *CDF*, naamini wote ni mashahidi...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, ile asilimia moja, sijui ilikuwa ya nini?

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza, nianze kwa kuunga mkono hoja halafu nianze kwa kuchangia kwa sababu ninayo mengi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie kwa upande wa elimu. Katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, alitangaza rasmi hapa kwamba mitihani ya Darasa la Nne na ile Mitihani ya Kidato cha Pili, Serikali imeiondoa lakini wanafunzi wale watafanya mitihani, pamoja na kufanya mitihani watakaofaulu, wakifeli wataendelea mbele tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi, ilinipa *shock* na mara baada ya Waziri kutangaza, alipotoka nje, mimi nilimfuata nikamwambia kweli Mheshimiwa Waziri uliyotangaza, ndiyo hayo? Akasema ni kweli. Nikamuuliza kuna utafiti wowote ambao ulifanyika kwamba ile mitihani ya Darasa la Nne na ya *Form Two*, haina maana? Akasema ni kweli mitihani hiyo tumeifanyia utafiti tumeona haina maana, bora tuiondoe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema nilipata *shock* kwa sababu kama wewe ni Mwalimu, mimi ni mwalimu, madhumuni ya mitihani siku zote, mojawapo ni kuwapanga wanafunzi kwenye madaraja. Hilo ndiyo lengo la mitihani. Kuna wanafunzi wanaelewa sana, kuna wanafunzi wanaelewa kiasi na kuna wanafunzi ambao *totally* hawana uwezo wa kuelewa, wanahitaji nguvu za ziada kuweza kuwaelimisha. Sasa unapoiondoa mitihani ile kwamba hata kama wakifanya wale wanafunzi ili mradi tu wamalize darasa la saba wamalize na ili mradi wamalize darasa la 12, basi wamalize lile darasa la 12 bila kuwafanya mitihani, ndipo hapo ambapo mimi nimepata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *syllabus* ya darasa la kwanza mpaka la nne, lengo lake kubwa ni moja tu, kumwezesha mwanafunzi aweze kujua kusoma na kuandika na kwa upande wa masomo yale, mwanafunzi huyu anatakiwa ajue matendo manne yale kujumlisha, kutoa, kugawanya na kuzidisha, basi. Sasa akimaliza kuyaelewa matendo yale, anafanyiwa tathmini na tathmini hiyo ndiyo mtihani. Anapofanyiwa tathmini ile, yule ambaye ana uwezo wa kujua kusoma na kuandika, yule ambaye matendo yale yote manne anayaelewa vizuri, basi anaendelea na masomo yale, yule ambaye hana uwezo anarudishwa pale nyuma.

Kulikuwa na kasoro katika mitihani ile, wote tunajua kwamba ili mtoto wa darasa la nne aweze kufaulu kwa wakati ule, ilibidi afaulu kwa alama 15 kati ya alama 50 kwa kila somo. Jumla ya masomo yalikuwa ni matano na masomo yale alitakiwa apate alama 75, lakini kasoro iliyokuwepo kwa wakati ule ni kwamba kama mtoto akipata alama 15, 15 masomo manne au angalau masomo matano, akipata alama 15, akipata zile alama 75 mtoto huyu amefaulu. Lakini yule mtoto ambaye alipata somo moja 50 kwa 50, somo la pili akapata 50 kwa 50, somo la tatu 50 kwa 50, somo la nne akapata 50 kwa 50. Somo la tano akipata alama 14 kwa 50, amefeli.

Hivyo ndivyo ilivyokuwa mitihani kwa wakati ule, kwamba ni lazima apate masomo yote yale matano. Lakini somo moja akifeli basi yule mtoto amefeli mtihani ule anatakiwa arudie tena mwaka darasa lile la 4.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiyo ilikuwa ni kasoro kwamba ni lazima afaulu masomo yote, lakini uwezo wa watoto unatofautiana. Mwingine anaweza kuwa mzuri kwenye masomo ya hisabati na mwingine akawa mzuri kwenye masomo ya Kiswahili. Masomo ya hisabati akifaalu vizuri yale masomo ya Kiswahili anaweza kufeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naiomba Wizara iliangularie tena upya suala hili, kwa sababu huyu mtoto ambaye anapelekwa bila ya kumfanyia tathmini katika mitihani ya darasa la nne, kama nilivyosema, anapofika darasa la nne, ule mtihani una lengo kwa matendo hayo tu. Lakini kuanzia darasa la tano, huyu mtoto anakwenda kwenye *applications* za masomo mbalimbali. Huyu mtoto sasa hivi anatakiwa ajue kipeuo cha pili cha namba.

Huyu mtoto sasa hivi anatakiwa ajue kutafuta eneo la pembe tatu. Mambo mengi sana kuanzia pale darasa la tano, kunakuwa na masomo magumu zaidi. Kama mtoto hajui kusoma, wala kuandika wala kuhesabu, hivi unampeleka darasa la tano anakwenda kufanya nini? Hajui kusoma, hajui kuandika, hajui kuhesabu, eti kwa sababu tu kuna baadhi ya maeneo fulani wanafunzi wale wanaorudia darasa la nne, hawaendelei na masomo, kweli? Ni sababu hiyo tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, napata matatizo sana kwa hili. Lakini hebu tuangularie wanafunzi wetu. Nilikuwa nachukua hiki kitabu cha takwimu za orodha ya majedwali ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ametupatia. Takwimu zilizokuwemo kwenye kile kitabu, zinatisha sana. Ukiangalia mtihani wa mwaka jana, pamoja na hawa wanafunzi kufanyiwa *screening* kwenye mtihani wa darasa la nne, wengi hawakumaliza darasa la

saba, kwa sababu walipofanya mtihani wa darasa la nne, wakachujwa wakapelekwa mbele. Hawa ndiyo wazuri, ambao walipata hizo alama 15. Tuuchukulie Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Shinyanga baada ya *screening* hiyo ya Wizara, wanafunzi waliofaulu kati ya wanafunzi 64,564 waliofanya mtihani ule ni wanafunzi 21,708 waliofaulu. Mkoa mzima wa Shinyanga asilimia 34. Hawa wamefanyiwa *screening* na wakati huo huo Serikali yetu inasema kwamba ifikapo mwaka 2010 nadhani, tunataka karibuni asilimia 80 ya wanafunzi wanaomaliza shule ya msingi wawe wanafaulu kwenda sekondari. Hivi hawa waliofanyiwa *screening* wamepata asilimia 34 wale ambao hawakufanyiwa *screening* ambao wataanza mwaka huu hivi watakaofaulu kama hawa wanafunzi 64,000 waliofanya mtihani si wanawenza kuwa wanafunzi 10,000 tu, waliofanyiwa *screening* asilimia 34 wasiofanyiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli suala hili mimi binafsi linaniuma. Nasema tena, naiomba Serikali iliangalie upya. Kwa mfano, hivi tumejiandaa kwa hili? Wanadai kwamba kutakuwa *remedial teaching* kwa wale wanafunzi ambao uwezo wao ni mdogo watapatiwa masomo ya ziada. Juzi alipokuwa anajibu swali Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mkoa wa Mtwara peke yake ulikuwa na upungufu wa walimu 2,400, mkoja! Mkoja wa Pwani, usiseme! Mkoja wa Ruvuma usiseme! Huko tena ndiyo mbaya zaidi. Huu upungufu huu wa walimu uliokuwepo, uwingi wa wanafunzi waliokuwepo madarasani mwetu, kuna upungufu. Hivi huyu mwalimu atapata nafasi gani? Shule ina wanafunzi watatu aende akafanye *remedial teaching*. Nafasi hiyo ataipata wapi? Tunajiongopea? Atafundisha namna gani huyu mwalimu wakati darasani mwake ana wanafunzi 100, ana wanafunzi 200 na kwa upungufu wao wote wanaingizwa madarasani kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, hapo hapo tena, tunayo madarasa ya kutosha katika shule zetu za Msingi kwamba wanafunzi kweli wanaingia madarasani. Ukienda katika shule zetu zote, majengo ya madarasa yaliyokuwepo ni machache sana, tunayo hayo mpaka tufikie maamuzi. Lakini la tatu, kama tukiondoa, kweli tunayo elimu ya awali katika nchi yetu kwamba kuna wanafunzi ambao kabla hawajaanza elimu ya msingi tunawapatia ile elimu ya awali.

Lakini hebu atuambie Mheshimiwa Waziri, hivi ni Wilaya gani ina shule za awali zinazolingana na shule za msingi? Wilaya ya Rufiji, shule za awali zilizokuwepo kati ya shule za msingi zaidi ya 108 lakini shule za awali zilizopo zimezidi sana shule 15 katika maeneo yale ya mjini, lakini shule zile za vijijini kule hakuna elimu ya awali, hakuna walimu. Sasa elimu ya awali inawaandaa. Elimu ya awali ina lengo la kuwaandaa watoto wetu hawa waweze kupata masomo mazuri. Akiingia darasa la kwanza, huyu awe anajua kusoma na kuandika, lakini tunao wa kutosha? Hivi kuna Wilaya ambayo madarasa ya elimu ya Msingi na elimu ya awali yapo yanalingana? Ombi langu, Wizara ya Elimu ikae itafakari, suala hili ni suala la kisera. Iwaone watu, washauriane tutoe maamuzi ya uhakika kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la kilimo. Wenzangu wengi wamezungumza kwa uzuri tu na kwa ufasaha mkubwa. Lakini nilikuwa nataka kusema kwamba, hivi tunatoa fedha nyingi sana za kujenga uwezo kule Wilayani, tunapotoa fedha hizi za kujenga uwezo Wilayani, hawa wakulima wenyewe wameandaliwa? Vifaa vya kulimia wanavyo? Unapopeleka fedha, zinamalizika kwa ajili ya semina tu. Mwaka huu kuna pesa ambazo zimekwenda chini ya mradi *DADPs*. Katika fedha zile ambazo zimepelekwa, kuna fedha ambazo wakulima wametakiwa wafungue akaunti ili ziwasaidie wale wakulima katika kuimarisha mazao.

Sisi kule kwetu Rufiji wakati mzuri wa kilimo ni kuanzia mwezi wa Kwanza, fedha zinapelekwa mwezi wa Sita wakati watu wanavuna. Lakini zinatakiwa zitumike kabla ya tarehe 30 mwezi wa Sita. Fedha hizi zinawasaidia nini? Tuweze kuolea wake wa pili! Kwa sababu kilimo chenyewe kimepita. Zina kazi gani?

Nafikiri fedha hizi ambazo zinawasaidia wakulima, ziende kwa wakati muafaka, wakulima wanapotaka kulima, basi na hizi fedha zisaidie kwenye kilimo chao. Sio zinapelekwa mwezi wa Sita, zitawaisaidia nini? Au kwa kilimo kinachokuja? Kwa hiyo, nilikuwa naomba suala hilo nalo lizingatiwe. Hilo la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Wizara ya Kilimo ni matrekta. Ili watu waweze kulima ni lazima wawe na matrekta. Tulifanya mkutano wa *RCC* pale Pwani, Wilaya nzima ya Rufiji matrekta yaliyokuwepo ambayo ni ya watu binafsi na makampuni mbalimbali yaliyokuwepo kule ni 15 tu. Unakwenda Tarafa nyingine, Tarafa mbili unatafuta trekta moja huwezi kulipata.

Hivi Serikali inapohimiza kilimo, haioni kwamba ina jukumu la kununua matrekta? Pamoja na kwamba jukumu la kununua trekta mnasema ni suala la watu binafsi, lakini hizi fedha za *DADPs*, mimi namshukuru sana Mheshimiwa Hawa Ghasia, alikwenda kule kwake akahamasisha fedha hizi za *capacity building* sijui ndiyo hizo au nyingine, lakini walikubaliana kwamba katika kuunda vikundi vile wao wakaamua kununua matrekta. Wamenunua matrekta manne yanasakiadnia kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na ombi katika maeneo yetu ambayo matrekta hayapo, basi Serikali itoe, waangalie kama kuna uwezekano wa fedha zile kuweza kununua matrekta, watupatie mwongozo tununulie matrekta. Lengo kubwa ni matrekta ndipo kilimo kinaweza kuendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu nilizungumzia siku moja kuhusiana na Kituo cha Afya Mbwera na upatikanaji wa boti katika maeneo ya Tarafa ya Mbwera. Serikali ikajibu ni jukumu la Serikali kuweza kupatiwa maboti Mbwera. Ni *sympathy*. Sio haki! *It is just a sympathy!* Nilipata uchungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nampongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, akisaidiwa na Mheshimiwa Waziri, dada yetu Kombani na akisaidiwa na Naibu Waziri, ndugu yetu Mheshimiwa Mwanri.

NAIBU SPIKA: Yupo na Waziri wa Nchi mwingine. Umemsahau?

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo nakuja. Pia Waziri wa Sera - Mheshimiwa Marmo na kwa kweli leo amenifurahisha, lakini hili na mimi mara kwa mara nilikuwa namwambia kwenye Kamati, suala la nyaraka alilozungumzia, lakini sasa tunaomba basi utekelezaji. Maana yake zimekuwa nyingi kweli! Utakuta mtu ana nyaraka zinazostahili kuweko kwa Mzee Kandoro Dar es Salaam anatembea nayo na sisi kama Serikali tunamtazama. Lakini madhara yake mbele kwa kweli yatatugharimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze tena hotuba ya Waziri Mkuu, kwanza kubwa ni lile ambalo karibu Wabunge wengi tulichangia bajeti iliyopita kuhusu suala la Madiwani. Kwa kweli tunapongeza sana hilo. Lakini haitoshi, nafikiri mwakani tujaribu kuangalia pia uwezekano wa Wenyeviti wetu wa Mitaa, nao wanafanya kazi kubwa na ngumu sana.

Lakini pia nitumie nafasi hii kuwaomba Wenyeviti wa Mitaa na hasa Dar es Salaam na Tanzania nzima, sasa hivi tumekuwa na tatizo kubwa sana, wala siilaumu Serikali, ni letu wenyewe wananchi. Tumekuwa na tatizo kubwa sana la wizi wa mafuta ya *transformer*. Dar es Salaam leo mnawenza mkalala wiki mbili, tatu hamna umeme. Siyo shida umeme hakuna, lakini watu wameiba mafuta ya *transformer*. Kwa hiyo, ndugu zetu Wenyeviti wa Mitaa, naomba tushirikiane tuhakikishe hilo tunalitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia nianze na maeneo ya Temeke. Pale Temeke tunalo eneo la Kurasini, Serikali imepanga eneo lile tupanue bandari na wananchi wa Temeke wamelipokea kwa furaha na malipo kwa baadhi yao yametoka. Lakini kulikuwa na ziada kwa wananchi wengine wa Zamu-Cargo na Rungwe. Kwa hiyo, naomba Serikali ifanye jitihada ili wananchi wale waweze kupata malipo yao. Lakini haitoshi, namshukuru sana Waziri aliyepita maana yake tulikawia kuwalipa wale wengine, lakini kwenye kikao kama hiki nikamwambia kwamba wako watu ambao wanawenza kununua vile viwanja ambavyo viko tayari ili tuweze kuwalipa. Alinikubalia na nilipeleka watu tena watu karibu sita, viwanja viwili vikanunuliwa, kimoja mia sita na kitu na kingine milioni 700 na kitu tukalipa watu.

Sasa najua Serikali ina nia nzuri na tuna viwanja pale 2001, 2005 na 2007 tulivitangaza, lakini bahati mbaya wale ambao waliotenda karibu wote hawakujitokeza ila kiwanja kimoja tu Mheshimiwa Waziri ameniambia kile cha mwaka 2005 ambacho ametokeza yule mtu wa nne kwenye tenda. Sasa namwomba tena Mheshimiwa Waziri vile viwanja viwili vilivyobaki tunaweza tukafanya utaratibu watu wakaja wakavilipia kwa tathmini ya Wizara ili tuweze kuwaondoa wananchi wale bila matatizo. Ombi langu kwa kweli kubwa ni hilo, tuwaondoe wale wananchi na kama tatizo ni viwanja viwili

vilivyobaki Mheshimiwa Waziri tuwasiliane ili tukamilishe mipango wananchi walipwe, watu wapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali sana. nina kilio kikubwa cha Yombo Vituka watu hao hao walihamishwa kutoka Kurasini, wakahamia Yombo Vituka zikawepo ahadi nyingi za barabara na zahanati, lakini barabara haikuwepo kipindi chote cha wenzangu. Lakini nashukuru mwaka jana kwenye bajeti hii tulipata kilomita moja na nusu lakini tatizo lilitokea na hili namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi wa Serikali waliangalie.

Tatizo lilitokea, mkandarasi aliyepewa pale Bwana Rukoro kwa kiwango cha lami mpaka leo ni tatizo. Sasa tuangalie kwa sababu tunaweza tukaacha makandarasi wazuri kwa taratibu zetu ambazo tumejifunga tukaweka makandarasi wabovu, kazi yetu ikawa haiendi. Yuko mkandarasi pale *EXIM* yule mkandarasi ambaye sasa hivi anatengeneza Kawe alianzia Temeke Stereo, anatengeneza barabara vizuri kabisa. Nina uhakika kama ile tenda ingelikuwa amepewa yeche kwa kweli ingekuwa sasa hivi imekwisha kwa kiwango cha lami.

Naishukuru Serikali kwa nini, iliniahidi kwamba bajeti hii itatupatia pesa nyingine kwa barabara ile. Nashukuru mwelekeo unaonyesha kuna kilomita nyingine nne na ndugu zangu wa Yombo Vituka, Makangarawe, Serikali yenu inawapenda na kilomita nne zinakuja. Nina uhakika kero ya mabasi mabovu kuja huko, kero ya nauki kuwa kubwa itakwisha, na niliwaahidi kwamba barabara nitaweka lami, sikuweka lami sichukui fomu 2010 pamoja bado ni kijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko tatizo lakini nataka kuuliza kama swalii. Temeke tumebahatika ni makao makuu ya TAZARA hili Shirika la Reli la Tanzania na Zambia. Lakini ajabu iliyotokea kwa miaka mingi sana pale Temeke tuna kijiji cha wavuvi ambacho kuna nyumba karibu 145. Lakini ndugu zetu wa TAZARA wameuza eneo lote mpaka njia za kupitia maji katika kile kijiji cha wavuvi. Matokeo yake maji yakija yanabomoa kwa watu nyumba 5zimeshaondoka za wananchi. Wananchi wale hata hamu ya kukaa pale hawana wameomba nije niwaombee kama Serikali inaweza ikanunue na zile nyumba zote ili waondoke. Lakini cha ajabu hata kiwanja cha michezo imeuziwa shule moja ya Indiana. Sasa nilikuwa nauiliza hili Shirika la TAZARA bado na sisi tunahusika? Katika uuzaji huu Serikali inajua?

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana sana nyumba za Jeshi la Polisi zinazojengwa Kurasini. Nipongeze sana Shirika la NSSF kwa kutoa pesa kuweza kujengwa nyumba hizo. Ila ombi langu kwa sababu ile *show* pale zilipojengwa zile nyumba nyingine zilizobaki zisipojengwa *show* ya pale itaharibika kutohakana na ile barabara mpya. Niombe Wizara ihakikishe ikishirikiana na NSSF tunamalizia na zile nyumba nyingine.

Daraja la Kigamboni limezungumzwa na mimi ninalizungumza kwa sababu linapitia Kurasini. Nalizungumza kwa sababu ndiyo Mwenyekiti wa Wabunge Mkoa wa Dar es Salaam na nafikiri kaka yangu yuko tena amepata *promotion*, sasa Naibu Waziri,

Wizara ya Fedha, Bajeti iliyokwisha aliniahidi hapa katika Bunge hili barabara, daraja litajengwa na aliahidi kwamba litaanza kujengwa mwaka 2008/2009. Kwa hiyo, tutataka tu kusikia kauli kama ile. Najua unakumbuka kaka yangu Mheshimiwa Sumari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napongeza sana Shirika la Nyumba la Taifa. Hali ya Dar es Salaam mjini inabadilika na nyumba zao wanazojenga ni za viwango, tofauti na nyumba ambazo zinajengwa kama hizo zinazoanguka. Nyumba zao zinazojengwa zina *parking*. Mimi naomba kwa kweli tuwape nguvu waendelee na zoezi hilo. Lakini ombi langu lingine, tuna nyumba pale Chang'ombe, Keko na Tandika Maghorofani. Wenzao wote wa chini nyumba zile wamezinunua, kasoro wao wa maghorofani. Kipindi kilichopita kaka yangu Magufuli aliniambia ooh, zile hatuwezi kuuza, sasa ni sababu gani kama za chini tumeweza kuuza, hizi nyingine kwa nini tushindwe kuuza?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba hilo tupate jibu lake. Wananchi wale nao wana hamu ya kununua kama wenzao walivyouziwa. Nije katika miundombinu ya Dar es Salaam. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameliona na ameunda Kamati. Lakini niwaombe Wabunge wote kwamba naamini wengi wenu mkistaafu mtaishi Dar es Salaam, pamoja na sasa tunahimiza tuhamie Dodoma, lakini Dar es Salaam bado ni mji wa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba kwa kweli katika suala la Dar es Salaam ndugu zangu tuweke mkazo tupate barabara nzuri, tupate mifereji ya uhakika. Mnaona wenyewe kuna wakati ule Wabunge pale mvua zilinyesha siku mbili kutoka katikati ya mji mpaka ufike kwako unatumia masaa matatu, manne.

Kwa hiyo, naomba kabisa na kwa kweli nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, bila kificho anafanya kazi usiku na mchana na nyinyi mnawoma kwenye TV kazi anayofanya. Nampongeza sana na ma-*DC* wake na hasa Kanali pale Temeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze dada yangu Waziri, lakini nmwomba kwa Jiji la Dar es Salaam, ameanza na nikiwa Mwenyekiti wa Wabunge, tunamuunga mkono, atusafishie Dar es Salaam kwa nia nzuri, atupatie viongozi wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono asilia mia kwa mia. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri jinsi alivyoialishe, lakini nawapongeza Waziri, Naibu Waziri katika Wizara hiyo, katika Ofisi yake pamoja na Watendaji kwa jinsi ambavyo

wameitayarisha hotuba hii. Imekidhi na kwa kweli imelenga kabisa katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005/2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiwe mchoyo wa shukrani na naomba kwa dhati kabisa nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa jitihada anazozifanya kupambana na ufisadi na rushwa hapa nchini. Kwa kweli amefanya mambo makubwa sana katika kupambana. Aliahidi na kwa kweli ameonyesha. Sio rahisi kuvunja Baraza la Mawaziri ukawaondoa viongozi wakuu kabisa kwa sababu tu ya kuwajibika kwa suala hilo, lakini amelifanya. Ni jinsi gani inaonyesha anapambana kwa dhati kabisa na ufisadi ambao upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpe pole pia kwa sababu pamoja na yote anayoyafanya mazuri, lakini bado kumekuwa na maelezo, maandiko mengi, kila siku kukicha, suala la *EPA*, *BOT*, *import support* na mambo mengine yanajitokeza. Lakini niseme ye ye mwenyewe ameamua kuyafanya, suala la *EPA* tunajua, ameshaunda na Tume inafanya kazi. Lakini utakuta maneno ni mengi, aliipa miezi sita na nina hakika baada ya miezi hiyo tutapata taarifa nzuri sana juu ya suala hilo. (*Makofi*)

Ameunda Tume ya Viongozi Mahiri, Watendaji wachapakazi ambao wako makini kabisa wakiongozwa na Mheshimiwa Mwanyika - Mwanasheria wetu Mkuu, Ndugu Hosea - Mkurugenzi wa *TAKUKURU*, pamoja na *IGP*. Ni watu makini, nina hakika taarifa itakuwa nzuri sana. Kwa hiyo, niseme tu kwamba katika jitihada anazozichukua, basi ni vyema tukampa moyo ili aweze kuendelea na hilo. Isiwe wengine wanarukia tu hoja, *import support*, *EPA* kana kwamba labda wao ndiyo wamelizua, kumbe ni jambo ambalo tayari linafanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wetu Chama cha Mapinduzi ni ile Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2005-2010 ndiyo mkataba wetu na wananchi na itakapotekelezwa ile ndiyo tutakuwa tumekidhi yale ambayo tumeyaainisha katika Ilani yetu. Sasa tusiache hilo tukaendelea sasa na mambo ambayo yanazushwa tu watu wengine wakati tayari Serikali inachukua hatua. Ni vyema tukajiekeleza huko na nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yako imelenga na niombe sasa tuisimamie hiyo ili ule mkataba wetu na wananchi tuutekeleze kwa vitendo. Maisha bora kwa kila Mtanzania inawezekana na kweli inawezekana kama wote tutaamua kufanya kazi ya kutekeleza Ilani yetu ya Uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo katika Jiji letu la Dar es Salaam, wenzangu wameyazungumza. Ningependa nichukue nafasi hii na mimi niyaseme na inawezekana Halmashauri zetu zinatakiwa ziyatekeleze. Lakini ama kwa uzembe ama kwa kutowajibika, mambo yale yanakuwa hayatekelezwi. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Kiongozi Mkuu wa hawa ambao nawasema na nina hakika anaweza akachukua hatua juu yao.

Tunalo tatizo katika Jimbo langu la Kinondoni. Matatizo ya barabara tumeyazungumza, lakini nina tatizo kubwa sana la miundombinu ya majitaka na maji ya

mvua na bahati nzuri niliuliza swali lilikuwa la kwanza kabisa hapa, majibu yalikuwa mazuri sana. Halmashauri imetenga Shilingi milioni 491 kwa ajili ya kupambana na tatizo hilo. Lakini tatizo ni kubwa mno. Pesa hizi ambazo zimetengwa hazikidhi, haziwezi kuondoa hata lile tatizo ambalo lipo pale Msisiri ‘A’ ama kule Bwawani Mwananyamala. Ukiachilia mbali yale maeneo mengine ambayo yapo Bonde la Mpunga na kadhalika. Kwa hiyo, tuiombe Serikali kwa kuititia Halmashauri yetu ijaribu kuongeza nguvu ili tuweze kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo tatizo la maji. Pamoja na jitihada ambazo zinafanya, lakini bado yapo maeneo ambayo maji hayapatikani. Ndungumbi Mpakani, Magomeni Makanya na kadhalika, ni maeneo ambayo maji huyapati. Lakini bomba kubwa limepita na lile bomba lina maji. Lakini ukiwaambia *DAWASA*, *DAWASCO* waunganishe inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri Mkuu na hili nalo tulione ili tuone nio hatua gani tutachukua kuhakikisha wananchi wetu wanaishi katika maisha ambayo yanastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo ambalo limejitokeza Kigogo Sambusa. Kigogo Sambusa ni eneo ambalo liko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Ilala, lakini linapakana na Kinondoni. Kuna mtu amejenga ukuta mkubwa mno, ukuta ule umefika mpaka katikati ya Mto Msimbazi kiasi kwamba mafuriko, ama mvua kubwa ikinyesha, yale maji yataingia kwa wananchi wangu wa Kigogo ndio watakaoathirika na wala sio Ilala.

Kwa hiyo, naomba hili tuliangalie kwa sababu huyu aliyepewa kiwanja kile amepewa mita 198 urefu. Mita 198 ukizipima na hana hati zinafika mpaka katikati ya daraja katikati ya mto, sasa kweli tukitaka mito tunaigawa viwanja. Huyu mtu hakujenga kufika kule, lakini huwezi kujua baada ya muda atasema kuwa lile ni eneo lake. Kwa hiyo, naomba hili tuliangalie ili tuweze kuondoa hili tatizo. Kwa sababu athari itakayotokea pale itawakumba wananchi wangu wa Jimbo la Kinondoni maeneo ya Kigogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalo tatizo lingine la Dampo. Pale Kigogo tunalo dampo wananchi wa Kigogo waliamua kwa ridhaa yao kwamba pale liwekwe dampo kwa maana ya kujaza shimo kubwa ambalo lilikuwepo. Tukakubaliana na Halmashauri kwamba watajaza kwa maana ya kumwaga takataka, kumwaga kifusi, kuweka dawa pamoja na kutengeneza barabara inayokwenda kule.

Lakini kwa kweli hivi sasa ni kitu cha ajabu sana, hata ukienda mwisho, wananchi wataamua kwamba iko siku watalala barabarani kuzuia magari yasiende kumwaga takataka kwa sababu hizi huduma zote hazipatikani sasa. Pamoja na ahadi ambayo imetolewa, hakuna dawa inayomwagwa pale, hakuna kifusi kinachowekwa, waliahidi kutengeneza barabara, haijatengenezwa mpaka leo ni mbovu. Kwa hiyo, wananchi wameshaanza kupiga kelele.

Bahati mbaya ikitokea wananchi wakigoma tusimwage takataka pale, basi Kinondoni yote kama sio Dar es Slaam, itanuka na hakuna mahali pa kumwaga takataka.

Magari yanayomwaga takataka Dar es Salaam yote ni mabovu. Ukiyaambia yaende yakamwage takataka Pugu Kinyerezi yakiondoka leo yatarudi kesho kutwa. Kwa hiyo, mji utazidi kuwa mchafu. Naomba Wizara iliangularie hili kwa maana ya kuongea na hawa watendaji wetu amba mara nyingine unaona kama ni wabishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo lingine ambalo limejitokeza, tulikuwa tunahitaji kujenga Shule ya Sekondari katika Kata ya Ndugumbi. Bahati nzuri, eneo lile lilikuwa linakaliwa na vijana wanaotengeneza magari kwa maana ya gereji. Tuliongea nao na wakakubali kuondoka kupisha eneo lile lijengwe Sekondari ili wao watafutiwe eneo lingine. Lakini sasa ni mwaka wa pili eneo lile hawajapewa mpaka hivi leo vijana wale zaidi ya 3000 wanashindwa mahali pa kufanya kazi, matokeo yake wanarudi katika shule ile ile kutengeneza magari ya eneo la shule. Hii ni hatari kwa sababu hata wanafunzi wanaosoma pale kwao inakuwa ni kero huku unasoma nje vyuma vinagongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kupertia Wizara hii kupertia Mheshimiwa Waziri Mkuu ajaribu kulifuatilia hili ili hawa vijana amba wameondolewa pale wapewe maeneo kama walivyoahidiwa ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu Sheria ya Mipangomiji, sheria ambayo inataka vikao vikae baada ya miezi mitatu, kikao cha Mipangomiji kikae baada ya miezi mitatu. Ni sheria nzuri, lakini kweli Dar es Salaam ama Kinondoni mahali ambapo watu kila siku wanajenga aombe kibali cha ujenzi, leo akae miezi mitatu asubirie kupata hicho kibali ndiyo maana kuna ujenzi holela. Hebu tuliangalie hili, kama kuna uwezekano kwa maeneo maalum, kama Kinondoni au kama Dar es Salaam vikao hivi vifupishwe ili kushughulikia maombi mengi ya hawa amba wanaomba kujenga majengo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie Hospitali ya Mwananyamala. Hospitali ya Mwananyamala ni hospitali hivi sasa ni kubwa kwa sababu inahudumia wagonjwa wengi. Wagonjwa zaidi ya 1,100 kwa siku ukiachilia mbali uwezo wake amba ulikuwa labda ni wagonjwa 200 kwa siku. Lakini huduma ambazo zinatolewa pale hazikidhi kwa sababu watu ama wagonjwa ni wengi na wengi wanaokuja pale ni wale wa vipato vyaa chini. Dawa hakuna, huduma mbovu, wengine wanakufa ovyo. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aiangularie kwa makini sana hospitali hii. Ama kuongezewa madawa, vitendea kazi na wataalam kwa sababu inahudumia wagonjwa wengi mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nzungumzie suala ambalo wenzangu jana walilizungumza. Mheshimiwa Simbachawene alilizungumzia na Mheshimiwa Grace Kiwelu alilizungumza na napenda sana jinsi ambavyo alivyolisema kuhusu watendaji kwenye Halmashauri zetu. Wapo watendaji amba ni wabovu mpaka unajiuliza: “*Hivi huyu aliajiriwa kwa sababu gani? Ama kwa hisani! Ama kwa sababu ya uwezo?*” Kwa sababu wengine unakuta hawana uwezo kabisa.

Kwa hiyo, naomba kabisa hili tuliangalie kwa makini, watendaji amba wako kwenye Halmashauri kwa kweli ni bomu, wengi wao ni mabomu hawafanyi kazi vizuri.

Tuangalie na ikiwezekana anapoonekana ni mbovu, basi afukuzwe kazi na sio kuhamishwa kupelekwa kwenye Manispaa nyingine. Tunao wanafunzi wengi ambao wamemaliza Chuo Kikuu kwenye mashule, hivi sasa wanahitaji kazi. Hao ambao wanazichezea kazi hatuna sababu ya kuwabembeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kama Waziri Mkuu anajua kwamba Dar es Salaam Mkuu wa Mkoa hana Ofisi! Pale anapokaa ni Ofisi ya Wilaya. Amejaribu kuomba, ana majukumu mengi anayofanya, alikuja Dar es Salaam ana mvi chache, unazihesabu kichwani. Lakini leo ukimwangalia Mkuu wangu wa Mkoa Mheshimiwa Kandoro, mvi zimejaa kichwani kwa matatizo yanayomwandama Dar es Salaam mpaka hata Ofisi anaomba viwanja, anashindwa kupewa mahali pa kujenga. Fedha anazo za kujenga, lakini eneo hapati. Kila anapokwenda, akienda Ilala anapigwa danadana, Kinondoni akienda danadana, Temeke akienda danadana. Hebu Mheshimiwa Waziri Mkuu tumsaidie ili aweze kupata Ofisi ambayo itakuwa ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa sababu muda umekwenda, kuna wanamichezo ambao wamekamatwa Mauritius kwa madawa ya kulevyta na inawezekana wamepitita Dar es Salaam sijui wamepitapita pitaje? Kwa sababu madawa ambayo wamekamatwa nayo tunavyosoma kwenye vyombo vya habari ni mengi sana, sidhani kama waliyaweka tumboni ama walikuwa nayo kwenye viroba. Inaonekana katika uwanja wetu wa ndege wa Dar es Salaam hauko makini.

Pamoja na uchunguzi ambao unafanywa na Serikali hivi sasa, basi ni vyema na hilo wakaliangalia kwa makini walipitaje pale Dar es Salaam na kama walipita nayo pale, basi wahusika ambao walikuwepo siku ile ya zamu kwa sababu najua vikosi vyote viro, wachukuliwe hatua kwa sababu hawa ni wachache, inawezekana wako wengi sana wanapita pale. Madawa ya kulevyta imekuwa ni athari kubwa sana kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Kinondoni mateja wako kibao, vijana wetu wameharibika, Serikali inapiga vita jitihada za Mheshimiwa Rais ni kubwa sana kupambana na madawa ya kulevyta, lakini inaonekana jitihada zake zinashindwa kwa sababu wenzetu baadhi ya vyombo vya usalama wanashindwa kulisimamia vizuri hili.

Kwa hiyo, pamoja na taarifa itakayokuja, basi ni vyema tukaambiwa na hatua ambazo zitachukuliwa kwa hawa ambao waliruhusu hawa wakapita na madawa yale. Kama mitambo haipo ya kujuwa, maana wengine wanakuja wanakamatwa hawa walipitaje? Lakini kama mitambo haipo, sasa tufanyeje? Tunashindwa kweli kuleta mitambo ya kugundua wanaoingiza madawa ya kulevyta au tuweke waganga wa kienyeji wapige ramli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia. Kwanza kabisa, naomba kama kawaida nimshukuru *Allah sub-hanah-wataala jalajalaluu* kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya

uzima wa afya na naomba sana kwa niaba ya wananchi wa Mafia haya nitakayoyasema Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba uyapokee kwa huruma ili uweze kufahamu kwamba watu wa Mafia tuna asili ya kukaa Kisiwani na hatuhami.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale inapotokea dharura ya mafuriko au mvua nyingi, barabara inapotokea bahati mbaya kukatika, basi mara nyingi tunawasikia Waheshimiwa Wabunge wakisema kwa vilio vikubwa kwamba barabara ile inatufanya sisi tuwe kisiwani. Sasa sisi ni *originally* wakazi wa Visiwani, hatuhami tena. Ujue kwamba adha tunayoipata ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, naomba pia na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kukupongeza sana Mheshimiwa Pinda - Waziri Mkuu wetu na *inshallah* Mwenyezi Mungu atakupa hekima kubwa, uwezo na akujalie akupe afya njema uweze kutuongoza katika Serikali hii ambayo naamini ndiyo mwelekeo na itakayoweza kutuletea heshima katika dunia hii tuliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nawapongeza Mawaziri wote, Manaibu Waziri, sitaacha kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoja -Mama Christine Ishengoma, yuko pembe ya chaki amekaa na naomba tena nimpongeze DC wangu, Mkurugenzi wa Halmashauri, Watendaji wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa jitihada kubwa wanazoonyesha katika kuhakikisha kwamba wamekuja kutusaidia sisi watu wa Mafia. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, suala la kwanza, natoa tena shukrani kwa Serikali, hasa baada ya kuona kwamba ujenzi wa Mafia wa Uwanja wa ndege umetengewa fedha. Tunaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zilizotengwa, sijui ni kiasi gani au kupitia *MCC* tumetengewa kiasi gani, lakini nitakuwa na hamu kubwa sitasita Wizara ya Elimu kuchangia, kueleza tena mawazo yangu na kuweza kuambiwa kwamba uwanja huu wa ndege kupitia *MCC* tumetengewa kiasi gani: Je, zitaweza kutosheleza ujenzi mpaka ukamilike wa uwanja ule pamoja na *apron tax way* na eneo la majengo yale pamoja na taa kama ahadi ilivyotolewa na wataalamu wetu kwa kauli ya Mheshimiwa Rais aliooisema pia, hilo nitataka kulifahamu baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, baada ya kupekua vitabu vyote, naiweka tahadhari tu, Wizara ya Miundombinu gati ambalo ndio asilimia 85 ya wakazi ambaa hali zao sisi wenyewe tunajijua tunavyoishi ndio tuliokuwa tuna nia ya kutaka kulitumia. Nini hatma ya gati katika Wilaya ya Mafia? Sio masihara kwamba labda tunavyokuja hapa tunafanya *jokes* kwamba nilitaka kugoma kula nikapata fedha za uwanja wa ndege, lakini mwaka huu nitasema nini kwa sababu tunaoadhirika ni sisi watu wa Mafia, tunaopata adhabu ni sisi watu wa Mafia na kila aina ya shida tunaipata sisi watu wa Mafia.

Nyinyi wenyewe mashahidi tu, hivi karibuni kuna meli ndogo ndogo zilizama zilikuwa zikipeleka mafuta, lakini kama kungekuwa na gati ingekuwepo meli kubwa na

vyombo vizuri vyenye usalama wa kuwafikisha watu wa Mafia na kuwarejesha. Sio watu wa Mafia tu kwa sababu sasa dunia imekuwa kama kiganja, watu wengi sasa wanapenda kuja Mafia, lakini hali ya usafiri imekuwa ngumu. Namwoba Mheshimwa Waziri Mkuu - Kiongozi wetu wa Serikali hapa Bungeni aielekeze mamlaka yake ya miundombinu kuhakikisha kwamba gati la Mafia lijengwe na fedha itoke mwaka huu bila ya hivyo kimbembe! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tat,u naomba sana tulizungumzie kupitia Wizara yako kwa kuwa mambo yote ya afya, kilimo fedha zote zinaelekezwa TAMISEMI. Mafia kama nilivyosema, kwa kuwa ni Kisiwa adhabu yetu ni kubwa tunayoipata. Tuna tatizo la upande wa Idara ya Afya, hali ni mbaya sana. Pale tulipo linapotokea tatizo lolote tu kijijini, basi kama usiku mgonjwa yule kama sio rehema za Mungu kupona, basi lazima afe. Hivyo kweli Serikali hii *ambulance* moja tu, Wilaya ngapi zilizokuwepo hivi karibuni zimepata *ambulance* kuipa *ambulance* moja Mafia, imekuwa ni mzigoto mzito wa Serikali hii. Tunaomba sana TAMISEMI, mwaka huu itakuwa ni aibu kwenu nyinyi kutamka kwamba mtapeleka sijui *ambulance* katika Halmashauri nyingi Mafia tukikosa. Hakika itakuwa aibu kwenu nyinyi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upande huo wa afya tuna tatizo la wataalam. Wataalamu wetu wachache, kwa hiyo, tunaomba mtumie jitihada zenu hata kwa mafungu tofauti kuhakikisha kwamba basi tupatiwe angalau Madaktari Bingwa wa kuweza kuja Mafia japo mwezi mara moja kama ile hali ya kuweza kukaa pale itakuwa nzito. Tusaidieni waweze kuja kusitirika ndugu zenu Watanzania wenzenu wa Mafia. Hili mkilifanya hakika na Mwenyezi Mungu atakusaidieni nyinyi katika nafasi zenu. Tuna matatizo katika Mafia, kuna kisiwa kikubwa, lakini kuna visiwa vidogo vidogo, tuna zahanati zetu tumejenga. Tunaomba mtusajilie safari hii. Barua tumeleta ziwemo katika programu ya usajili. Zahanati ya Kijiji cha Juani ambayo ni kisiwa na zahanati ya kijiji cha Jojo ambacho pia ni kisiwa, tunaomba mtusajilie hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo pale. Linapotokea tatizo, mgonjwa ameshindikana kutibiwa Mafia anapata rufaa ya kuja ama Muhimbili au Kibaha Mkoani. Ngoma katika usafiri. Hali zetu tunajijua sisi wenyewe! Kwa hiyo, naomba sana ama kama ni Serikali itusaidie kutupa mafungu au Waziri atamke watendaji wetu wasikie kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mafia katika moja ya fedha zake zitengwe kwa ajili ya kusafirisha watu hawa. Hali ni mbaya, mizigo tunaibeba sisi Wabunge wawili. Tunabeba mizigo hiyo wakati mwingine tunashindwa, kama hatupo watu wanaadhirkira, watu wanakufa, viungo vinaoza, matokeo yake yule mwenye uwezo atapanda ndege, lakini yule asiyekuwa na uwezo kupita baharini wakati mwingine siku tatu ziko boti zinazokwenda.

Lakini hebu angalia mtu umevunjika mkono, mtoto mdogo au wewe mwenyewe unapita baharini unakwenda Nyamisati, kutoka Nyamisati mpaka Dar es Salaam karibu kilomita 150 barabara ni mbaya! Hebu tuambie hali inakuwaje ya mgonjwa yule? Tusaidieni watu wa pale! Tusaidieni programu hii iwepo ianzishwe kama ilivyokuwa zamani, wagonjwa wanapopata *referral*, basi zitumie *government warrant* kwa maana kusafirisha wagonjwa liwe jukumu la Serikali, sio Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wenyewe umekuwa mzito naomba nizungumzie suala la uvuvi. Mheshimiwa Mama Kimbau amezungumza mama yangu na amejitahidi sana katika kuelezea. Jana Mheshimiwa Shoka amelizungumza, ni kweli anatoka katika chama ambacho sio chama changu mimi ninachotoka, lakini ndiyo hali halisi ilivyokuwa. Mafia sasa hivi Benki imezuia kutoa mikopo, inauza majumba ya watu hakuna mzunguko wa fedha, wizi mdogo mdogo upo umezidi kwa sababu hakuna kazi wavuvi wamezuiliwa. Sasa tunaomba kabla ya Wizara ya Uvuvi hajaleta bajeti yake tunakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu mwombe Mheshimiwa Waziri au Naibu wake aende Mafia akazungumze na wavuvi halafu aone hali halisi ilivyo ya njaa iliyokuwepo pale Mafia. Naomba sana sitasema mengi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mradi wa Masemu ninachotaka kuzungumzia mradi huu wakati Waziri atakapokuja atuhakikishie mambo madogo tu mawili. Atuambie kila Wilaya itatengewa kiasi gani? Maana yake mradi huu unatembea ukanda mzima ule wa Pwani. Lakini pia na kila Wilaya jinsi ya kuandaa miradi yake wasiachiwe wananchi na sisi tushirikishwe. Mimi ni mvuvi asilia, nafahamu hali halisi ya baharini. Kwa hiyo, viwango vile vinavyoletwa ukiangalia taarifa zote hizi za mipango mizima ya Halmashauri ya Wilaya ya Mafia fedha za Masemu zaidi ya milioni 300 zinakwenda kwenye doria. Sasa kweli hapo zimelenga kumsaidia huyu mtu au zinakwenda kufanya nini?

Kwa hiyo, tunaomba doria tunayohitaji kwa wavuvi haramu, lakini pia tunahitaji fedha zile sasa ziwaende wananchi moja kwa moja waweze kufaidika. Naamini kwa dola milioni 60 zilizokuwepo naamini ukanda wa Pwani wote kuanzia Tanga mpaka Mtwara na Unguja na Pemba kutakuwa hakuna maskini na hakuna mtu atakayeambiwa mvivu ukanda wa Pwani pesa hizi zitamsaidia na zitakuwa ni ukombozi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mawazo yetu sisi yatasikilizwa, wataalamu wakikaa nayo basi na sisi wachambue mawazo yetu. Bila ya hivyo fedha zitaliwa na taarifa hizi zipo na hakuna chochote kitakachoonekana katika mradi huu na fedha hizi ni fedha za wananchi walipa kodi, sio watu wa Mafia peke yao au watu wa Ukanda wa Pwani, sisi wote jamii nzima ya Watanzania ni fedha za mkopo ziende manthari zimetulenga, sisi basi zitusaidie na wananchi wale waweze kuonekana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni dogo. Nilikuwa naomba katika Wilaya ya Mafia tuna Kata moja inaitwa Kata ya Baleni, tunaomba igawanywe. Hali ni mbaya, Kata kubwa! Najua Wilaya yenyewe ya Mafia huwezi kushindanisha na Tarafa moja ya Bara, lakini kulingana na mazingira ya Kiwilaya tunaomba Kata hii igawanywe na barua ipo kwa Katibu Mkuu TAMISEMI, tunaomba hilo Mheshimiwa Waziri atusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho kabisa, nizungumzie suala la maji. Naomba Wizara ya Maji itakapokuwa imekaa, naomba na yeze Mheshimiwa Waziri aende Mafia aje kuangalia hali ya wananchi wa Kijiji cha Juani Kisiwani. Hali ya wananchi wa Kijiji cha Jibondo na hali ya baadhi ya visiwa vidogo vidogo watu

wanaadhirika na kufa na kuacha kufanya kazi za maendeleo kwa ajili ya kutafuta maji. Wanasaferi baharini masaa matano mpaka au wakati mwingine siku nzima kwenda kutafuta ndoo mbili au tatu.

Mashua inapotoka Jibondo kuja kisiwa kikubwa wakati mwingine inachukua masaa maana hawezi kwenda mtu mmoja huwa wanachukua majirani na kadhalika. Kwa hiyo, kila mtu anapata ndoo mbili au tatu, watu hawafanyi kazi. Tunaomba mtusaidie mitambo ya maji iliyochimbwa Kigamboni, hivi ni kwa nini na sisi watu wa Mafia kwenye visiwa vile angalau viwili vilivyokuwa mbali wasipelekewe na tukaenda kuchimbiwa. Kwa hiyo, naomba Waziri Mkuu Wizara ya Maji isaidie katika kuchimba visima hivi katika maeneo niliyoyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na nawatakia kila la kheri.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge najua dakika zilizobaki kwa msemaji mwingine ni 10 tu sasa nitaongeza dakika tano kusudi angalau apatikane huyu mtu.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunihurumia. Kwanza naunga mkono hoja na nampongeza Waziri Mkuu na timu yake yote kwa kazi nzuri ambayo waliyoifanya katika Wizara hizi. Nina machache ya kuongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri ahadi za viongozi hazitekelezwi. Ahadi ya Rais Mstaafu Mkapa aliahidi kuhusu kugawa Kata katika Jimbo langu la Uchaguzi. Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati huo alikuwa Naibu Waziri, akaja akawa Waziri, sasa Waziri Mkuu. Mimi nafikiri anionee aibu kama dada yake mwaka wa tatu huu Mheshimiwa ndugu yangu Pinda unafahamu matatizo ya Igalula. Kata ya Kigwe kila nikikuona unasema dada usiwe na wasiwasi mambo yanakwenda. Kawiakawia utamkuta mtoto sio wako. Tunavyozidi kukawia mambo ndivyo yanavyozidi kuharibika.

Kata ya Kigwe ni muhimu sana katika jimbo langu la uchaguzi. Ni kura ya CCM. Kama nikiendelea kupiga danadana kwamba inashughulikiwa 2010 kura zitapungua. Bado wakati ule niliomba Rais Mkapa alikubali kugawa kupata Tarafa ya Kizengi na yenye pia mpaka leo inasuasua. Matamko niliyoyapata kwenye Serikali ni kwamba Kata nyingi zimeombwa, lakini hili lilikuwa ni tamko la Rais. Labda kama matamko ya viongozi hayathaminiwi, labda nielezwe leo ili wananchi wangu wafahamu. Kwa kweli wanashangaa kama Rais anaweza kutamka: Je, akienda Waziri akatamka atasikilizwa? Mimi Mbunge wao nikieleza si ndio kabisa!

Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu Pinda lione hili kwa macho ya huruma angalau katika kumaliza kwako kesho unitamkie dada wewe nenda kwa usalama na wananchi wako wa Igalula Kata imekwishatengewa fedha zake na Tarafa imeshatengewa fedha zake. La sivyo, ndugu yangu hata ukija kule kama hii Kata hajatamkwa, labda uamue usije mpaka Kata hapo itakapotamkwa, lakini watakuuliza. Watakuonyeshea na mimi sitaki uonyeshwe kidole. Wewe mtoto mzuri, halafu mtiifu, nakuomba sana. Alikuwa Waziri – Mheshimiwa Celina Kombani pale, walimfurahia kweli kwa mambo

aliyokuwa anayazungumza, lakini leo akirudi tena watamwuliza hii Kata, yatakuwa ni yale yale nakuomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni ujenzi wa barabara ya Itigi. Inazungumzwa sana. Mimi nasema hivi, ukiahidiwa kitu, basi tekeleza. Leo mnatuambia barabara ya Itigi haimo katika bajeti humu, lakini kwamba Rais ameahidi na nimemsikia mwenyewe Rais kwenye Kampeni, amekuja Tabora akatamka tena anasema barabara ya Itigi itajengwa wananchi msiwe na wasiwasi. Jamani hatma itakuwa mbaya sana mwaka 2010 ikiwa barabara ya Dodoma mpaka Manyoni imechukua miaka mitatu haijamalizika na kilomita chache leo kutoka mpakani mwa Itigi mpaka Tabora ni kilomita zaidi ya 210 na kitu, kama haikuanza katika kipindi hiki itaanza lini? Naomba angalau muanze tutakuwa na la kuzungumza, lakini kama isipoanza ianze mwaka kesho itachukua kilomita ngapi kutengenezwa barabara ya Itigi - Tabora ? Itakuwa ndogo barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni reli. Reli wamezungumza sana wenzangu, lakini reli hii tusiwalaumu hawa Wahindi ambao tumewakodisha kwa sababu Wahindi wana asilimia zao na Serikali ina asilimia zao. Sasa wote tunawalaumu. Wapiga kura wangu wa Jimbo la Igalula ndio watumiaji wakubwa wa reli hii baada ya kushindikana hiyo barabara. Sasa mwaka juzi Rais alikwenda Amerika akaahidiwa kusaidiwa na Mfuko wa *IFC* mnaufahamu kukopeshwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli hiyo, lakini Serikali ikaambiwa kwamba ifanye haya, haya halafu watapata mkopo ule.

Tangu Septemba mwaka jana Serikali haikufanya chochote mpaka Mei mwaka 2008 fedha mtazipata upesi kweli! Hii reli itatengemaa! Bado Rais amekwenda India miezi miwili iliyopita akaahidiwa na Serikali ya India, Waziri Mkuu wa India, akaahidi kutukopesha dola milioni 47 kwa ajili ya ujenzi wa hii reli lakini nendeni basi mkanianidikie haya na haya mlete *application* mpaka leo hii nasema Serikali bado hamjafanya kitu. Sasa hii mtawalaumu namna gani? Ikiwa sisi wenyewe hatutekelezi wajibu wetu hawa Wahindi watatekeleza? Ina maana watu wa Tabora tutaendelea kufa hatuna usafiri wa reli wala barabara! Tusiwasiliane na Makao Makuu ya Dodoma, tusiwasiliane na Mkoa wa Dar es Salaam, sasa tukae kwenye kisiwa mpaka lini usafiri haupo? Labda ndege sijui itakuja lini?

Naomba sana hawa wawekezaji ambao wapo walihidi mwezi Aprili kwamba behewa wataleta, injini wataleta, lakini hawajaleta mpaka hii leo. Jana nilikuwa *Railway Station*, bahati mbaya nikawakuta huyo Mkurugenzi wao kutoka India na Mkurugenzi ambaye yuko hapa. Bahati nzuri alikuwa na watendaji wa Reli. Nikaona nashangaa pale wakamwuliza huyu ni nani. Waliposema *Madam, how are you?* Nikawaambia niwaulize nyie, kwa sababu kuweko kwangu hapa natazama nyie tazameni treni ilivyojaa *mail train*. Mizigo iko kwenye maungio, iko juu wananchi wanaanza kupigwa na askari wamening'inia kule *second class* watu 15 badala ya watu sita. *First class* watu nane badala ya watu wawili. *Third*, ndiyo kama mihogo. Mihogo imetoka Morogoro inakwenda zake Tabora. Magunia ya uweli na mtama yanatoka Dodoma yanakwenda Tabora. Nikawaambia wale Wahindi mmeona hali ilivyo, wakanitazama. Wakasema je, ndivyo mlivyofanya? Kumbe wanasema wakatieni tiketi tu waingie, waingie vipi?

Wamepunguza mabehewa badala ya treni moja mabehewa 20 wameweka 16. Wanasema tutategemea mwezi wa Nane tukileta mabehewa kutoka India tutaongeza.

Treni ziliwa tatu, lakini siku zile za kawaida ziliwa karibu nne zinaweza zikapungua tatu, walipokuwa wanaendesha Waswahili wetu. Leo wamekuja wao kutusaidia treni mbili. Mnategemea Mikoa ya Magharibi watakwenda na usafiri gani? Ndege nani anaweza ku-*afford*? Robo tatu asilimia 99 ya wakazi wa Magharibi wengi hawana fedha za kutosha kununua tiketi ya ndege na ndege zenyewe hazipo na viwanja vyenyewe havipo, watatoa wapi? Tabora ndege ikienda safari nyingine inazama wakati wa masika kutokana na kiwanja kilivyo.

Sasa nasema hivi, kweli mnawatachia heri hawa watu au mnawatachia wakati wa uchaguzi tu? Hawa watu wanatachia wakati wa uchaguzi watupe kura hatuwapi miundombinu ili na wao wakajikomboa katika umaskini uliopo.

Mimi naomba sana kwa kweli, jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa anapita pale treni ikasimama. Mimi kidogo niseme hapana, hebu asimame yeze aone. Nikawaambia pale, jamani, hebu acheni, usalama upo, asimame aone jinsi watu walivyojifinga. Pale huwezi kuona ndani giza ilivyokuwa katika *third class*. Mama mmoja amejifungulia ndani ya treni wiki iliyopita alivyominywa. Chooni watu wanaka, hakuna cha *first*, *second* wala *third*. Mtu mmoja pia amekufa anaelekea Dar es Salaam kutoka Dodoma alivyominywa akashindwa kupumua. Mimi naomba Serikali kwa heshima zote simamisheni treni, watu wanakufa!

Mheshimiwa Naibu Spika, jana treni imeondoka kufika Makutopora, inapanda mlipa injini zikafeli. Watu wakatachia kuruka wakaambwa hapana tulieni ikabidi arudi *reverse* mpaka Makutopora kutoka mlipa wa Saranda kuja kusubiri injini kutoka Dodoma. Watu kidogo waruke Mheshimiwa Waziri Mkuu na wewe pia mtu wa huku, wewe unatumia gari, lakini watu wako wanatumia treni mpaka Mpanda kule kwenye Jimbo lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu afanye ziara ya treni kwa kipindi hiki aone watakaokaa *third*, atashindwa kutazama, Atalia! Sasa huyu amekufa, huyu amejifungua anahudumiwa na wanaume, hakuna usiri tena wa wanawake wakati wa uzazi, lakini yuko kwenye treni.

Sasa naona kwamba wakati muafaka hawa watu sasa wasimamishe mpaka mtakayoyipanga. Tumevumilia miaka yote, tutaendelea kuvumilia, lakini sio kuwachukua watu wakafia kwenye treni eti kwa sababu mnatachia kuwafurahisha waliokodisha na sisi wenye Serikali tuna mipango chungu nzima lakini mipango yenye isiyotkelezeka. Naomba sana hili Shirika la Reli kuanzia sasa toa amri lisimame. Likianguka hili treni watakuwa maelefu. Jana nimewaambia wakifa watu hapa nyinyi mtaishia Ukonga msiwaabudu India. Kwa sababu mna-zooret *human rights* mnakubali wapakiliwe tu hapa kwa sababu ni Waswahili, kwani tumekuwa India hapa!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie tatizo la ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya yetu ya Iyui. Ni kweli sisi wenyewe tuliamua kisiasa kwamba Makao Makuu yawe Isikiza. Lakini kulitamkwa mwaka huo wa 2002 au 2003 nimesahau kidogo kama Wilaya nne, Wilaya mojawapo ni Wilaya ya Hai. Nenda kaone Wilaya ya Hai inavyoendelea katika majengo halafu uone inavyosota kuendelezwa Makao Makuu ya Wilaya yetu. Eneo lenyewe tulilochagua *not viable* kwa muda huu. Nasikitika sana kusema na mimi nilikuwa mmojawapo katika kupiga kura, lakini maamuzi ya kisiasa wataalamu wapo mje kutushauri. Mmetushauri kuhusu Nanga ya Igunga wanasiwa walipiga kura wakasema kwamba Nanga iwe Makao Makuu, lakini baada ya kuona matatizo yaliyojitokeza, afadhali wakaamua wakarudi kule kule na sisi tusione aibu kurudi. Kwa sababu juzi alipokwenda Waziri kwenda kutazama hali halisi Waziri Kombani akaambiwa kupeleka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda umefika kengele ya pili.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono, aah nimeunga mkono tangu zamani. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nashukuru sana kwa dakika tano mlizotupa kwa sababu idadi yetu ya kuzungumza asubuhi inakuwa 11 jioni, kwa hiyo, tusingefanya hivyo tungekuwa tumepungukiwa na nafasi moja.

Tukirudi mchana Waheshimiwa Wabunge wafuatao wajiandae: Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Haroub Masoud, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Eng. Laus Mhina, Mheshimiwa Alyoce Bent Kimaro nategemea na Mheshimiwa Meryce Emmanuel atafikiwa.

Baada ya kusema hivyo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 07.05 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa mwanzo leo hii atakuwa Mheshimiwa Issa Kassim Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Guido Sigonda na Mheshimiwa Steven Galinoma ajandae.

MHE. ISSA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii leo ikiwa ni mtu wa kwanza kwa jioni ya leo, jambo la kwanza namshukuru Waziri Mkuu kwa kuwasilisha vyema bajeti katika Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nitakaloanza kuongea kwa siku ya leo ni suala la *EWURA*-umeme. Suala la umeme kwa sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sehemu ya Zanzibar imeanza kutuletea mashaka makubwa kutohana na Bunge lako Tukufu kuwapa meno *EWURA* na tumekubaliana sote, *EWURA* wamepandisha umeme kwa Bara asilimia 21.7 kwa Zanzibar wamepandisha umeme kwa asilimia 168. Je, umeme huu wanawauzia Zimbabwe, Zambia, au katika Jamhuri ya Muungano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkoo ana kazi kubwa sana. Sasa hivi mnaanza kutengeneza jibu lingine la kero za Muungano, Waziri Kiongozi, Waziri Mkoo aliyeondoka, aliystaafu, walikaa kikao na Zanzibar ikakubali kulipa kama wanavyolipishwa Tanzania Bara. Je, kuna kitu gani hata ifike Zanzibar wauziwe umeme kwa asilimia 168, uchumi wa Zanzibar ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waziri Mkoo unapokaa na ndugu yako ukihitaji kumsaidia kumpa ninyi huku mnaita *dinner* na *lunch*, umsaidie kwa dhati umpe mtaji ajiongoze, tumefika mahali pabaya kama tuna Muungano tuwe na Muungano ndani ya moyo, siyo Muungano wa kubabaisha kwenye mdomo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni la kusikitisha mno. Joto tulilolipata kwa muda wa mwezi mmoja zanzibar haina umeme. Dokta Idrisa ameniandikia kwamba shirika la umeme Zanzibar watakata umeme leo; anatutakia mema? Mkae mtanabahi, watendaji ni lazima wajue kwamba ile ni sehemu ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme huu ulikuwa ni mradi wa Zanzibar kutoka Tegeta, Kiromoni, Fumba mpaka Zanzibar. Zanzibar imetoa mchango wake wenye kutaka umeme, leo umeme huu mnaupandisha namna hii, mnawaweka vipi wananchi wa Zanzibar? Uchumi tuliokuwanao, tunalia na wanyonge wa Zanzibar, hali zao za kimaisha ni ngumu, hili tutake tusitake lipo, watu wa Zanzibar tusionbe tu kila siku, mkae mtanabahi upendo unakwenda ndani ya moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu huyu hapa Mheshimiwa Yahya, sio kama hatukosani, tunakaa tunakosoana pamoja, ninyi Bunge zima mnasema mnapendana, lakini tunakaa pamoja panapokuwa na athari na panapokuwa na tatizo.

Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkoo, kama ikibidi wamepunguza bei, basi Zanzibar hawajawapelekea taarifa au *TANESCO* hawajawaeleza Wazanzibar kwamba wameshakubaliana bei yake na ya Bara iwe hiyo hiyo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkoo awaeleze na litoke tamko rasmi kwamba umeme ni bei moja kwa Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, Zanzibar inalipa umeme shilingi bilioni 1.2, msifikirie kwamba wale wateja ndiyo wanaolipa zile pesa, ni Serikali ndiyo inachangia kuwasaidia wananchi wa Zanzibar, ni lazima mlielewe hili! Sasa mnaitwisha mzigo vilevile Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar, wapunguzieni, wana mambo mengi ya kufanya kutimiza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mandhali hili Waziri Mkuu kwa usikivu wake namwona anaandika, leo au kesho utakapokuja kutoa tamko, nina uhakika atatoa maelezo ya kina na ya matumaini kwa wananchi wa Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nitakaloliongelea ni mchango unaotolewa wa 4.5, wazee wangu tangu hatujaanza kutambaa mpaka tumetambaa, mpaka tumeingia kwenye Bunge Tukufu hili, Zanzibar inapata asilimia 4.5. Tulipokuwa tukisoma shule sisi darasa moja watoto 15, sasa hivi wanafunzi wanaosoma darasa moja ni kati ya 50 na 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muelewe kuwa watu kule wanazaa mambo, yanakua na mambo yanaongezeka na ilani ya Chama cha Mapinduzi inataka kuendelezwa ingawa kuna jamaa zetu wanaona hawafanyiwi kitu, lakini Pemba kuzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Dr. Amani Karume* nina uhakika ameshakuwa *Doctor*, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni *Doctor* anakamilisha ilani ya Chama ya Mapinduzi na anaisimamia kweli kweli. Lakini mhakikishe uchumi wa Zanzibar, muda wa mwezi mmoja umeme hakuna, wanapata kitu gani mnafikiri? Kipi kilichopatikana na kipi kilichokwenda? Nataka mkae, Kamati imeundwa na Mzee wetu Shelukindo na mapendekezo ameleta na sasa hivi ni miaka miwili, mnakuwa na kigugumizi cha nini? Msioamua kitu cha kufanya na yametoka mapendekezo angalau asilimia 10 mpaka 15 ,tatizo liko wapi kumpa ndugu yako akajiendesha? Sisi ni ndugu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mke wangu ni wa Kigoma na Tabora na nimeshazaa naye. Mke wangu ni mmanyema wa Tabora na nilishazaa naye, tatizo liko wapi? Hatuwezi kuvunja undugu, tunahitaji kuimarisha Muungano wetu kwa kukaa kwa kusikilizana, Komredi Mwanri unanisikia! Tunahitaji kukaa pamoja kuondoa matatizo, umeeleza kwenye kitabu hiki ukurasa wa nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu atavalia njuga matatizo ya Muungano na yasiyokuwa ya Muungano. Tunataka kuona cheche zake. Wananchi wa Zanzibar walishachoka kulalamika. Wale Wapinzani husema sisi tuko kikeni na ninyi kuumeni ni lugha kubwa sana hiyo na mmeiweka kwenye mabano, ukaambiwa kwamba uko Kuumeni na Kikeni ni lugha nzito wamefika hadi wapinzani kusema kama umeme tuna uhakika hauwaki Zanzibar na ukiwaka mje mtunyoe ndevu, allah! Msifanye mchezo! Siyo masihara, sisi tuna upinzani wa hali ya juu ni lazima myajue hayo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais – Mheshimiwa Dr. Karume ana kazi nzito nchi ile, msiwaone wanasimama hapa tu, wana ajenda zao za siri hawa wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *OIC (Organisation of Islamic Conference)*, mimi kabla sijawa Mbunge mmekaa katika Bunge hili, mmezungumza na aliyekuwa Waziri Mkuu Mzee Malecela akasema bayana kuwa Zanzibar wana nia nzuri sana, mishtuke kwamba mna kitu *Islamic* humu. Zanzibar inataka kujikomboa isaidiwe, leo tatizo la umeme kama halikuwepo katika shirika hili tusingelipigia kelele namna hii.

Lengo lake ni zuri, hii haimgusi mtu yeote mwenye dini, kila mmoja na dini yake Tanzania. Nchi yetu ya Tanzania haina dini, lakini wananchi wake ndiyo wanadini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiingia katika umoja huu, tutafaidika sote Watanzania na inaonekana dhahiri kwamba Zanzibar ilikuwa na nia njema ikapigwa bao la kisigino ikaambiwa itashughulikiwa, mpaka leo ni miaka tisa, tunakwenda wapi jamani? Nchi ni moja, tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zinazojiunga na *OIC* siyo lazima wawe Waislam, naongeza tena.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Issa Kassim Issa, naomba uunge mkono hoja.

MHE. ISSA KASSIM ISSA: Nimeshamaliza?

MWENYEKITI: Ndiyo muda wako umekamilika.

MHE. ISSA KASSIM ISSA: Naunga Mkono hoja, Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naona tumeanza vizuri na sasa naomba nimwite Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda na atafuatiwa na Mheshimiwa Steven Galinoma na Mheshimiwa Dr. Philemon Sarungi ajiandae.

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kama mzungumzaji wa pili kwa jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo kwa kweli lengo lake kubwa ni kujaribu kuleta mapinduzi ya kimaendeleo hasa vijijini na zaidi jinsi alivyoisoma ile hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namwangalia toka alipoanza kuisoma kwa muda zaidi wa saa moja, hakuweza hata kutetereka wakati aliposimama na hasa kitu ambacho nilitegemea kwamba angekunywa maji, lakini hakufanya hivyo. Nampongeza sana na hii inaashiria kwamba bado ana uwezo wa kiafya na ndiyo hiyo inanipelekea kwamba yale yote yaliyoandikwa nina imani kwamba yatakekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu hiyo inatokana na zile ahadi ambazo tayari ofisi yake ilikwishaanza kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipoingia kwenye Bunge hili, ombi langu la kwanza kabisa lilikuwa ni elimu. Mwaka 2006 katika Jimbo langu la Songwe, tulikuwa na shule moja tu ya Sekondari ya Serikali, naomba niishukuru Serikali kwa jinsi ilivyonisaidia na hadi sasa hivi tuna shule nane za sekondari. Hizo zinatokana na jitihada

za Serikali za kujaribu kutatua matatizo ambayo Waheshimiwa Wabunge kwa kupitia Bunge tunawakilisha wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niandelea kuishukuru Serikali kwa kuwa nilikuwa nimeomba tusaidiwe Miundombinu ya barabara ya kutoka Mbalizi, Mkwajuni hadi Makongorosi, ikaniahidi. Miaka miwili iliyopita tulikuwa tunatumia *pick up* na malori, lakini sasa hivi tuna mabasi ambayo yanapita katika hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kwamba ni mafanikio kutokana na jitihada ya Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, yapo mambo mengi ambayo Serikali imeyafanya katika Jimbo langu, lakini tatizo kubwa ambalo ni kipingamizi cha kuendeleza yale maeneo ni ukubwa wa eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chunya ni nusu ya Mkoa wa Mbeya, ukubwa wake na bahati mbaya katika kilio changu ambacho nilianza nacho wakati naingia kwenye Bunge hili ni kuwaomba viongozi angalau watembelee katika eneo hili wakaone wao wenyewe hali halisi ya maendeleo. Nimepiga kelele kwa muda wa miaka miwili iliyopita, naishukuru Serikali kwamba sasa hivi wameanza kuja, ni hatua mojawapo ambayo ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vibaya kuelezea kwamba Serikali tangu tumepata uhuru ni Rais mmoja tu ndiye ambaye ametembelea katika Wilaya Chunya, kuna nini? Tuna matatizo gani? Hivi Wilaya ya Chunya siyo mionganoni mwa Wilaya nyingine za Tanzania!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni jinsi ya kutembelea ile Wilaya, Mheshimiwa Rais anaweza akawa ana mawazo na dhamira nzuri tu, lakini hali ya Wilaya ile ndiyo inayofanya hata viongozi wa Wilaya na Mkoa wakashindwa namna ya kumfikisha katika yale maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa sasa hivi kwa sababu ni miaka miwili na nusu ya awamu hii ya nne, naomba kwamba yale maombi yetu ya kuigawanya Wilaya ya Chunya, nafikiri ndiyo wakati wake. Bahati nzuri haya maombi Mheshimiwa Waziri Mkuu tayari anayo, ni jirani yetu, tunapakana naye. Kwa hiyo, sidhani kwamba itakuwa ni dhambi ikiwa kama ile Wilaya itagawanywa na kuwa Wilaya mbili, itasaidia kuongeza maendeleo ambayo sasa hivi yameshaanza kujitokeza .

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala mengine ambayo ni madogo madogo ambayo bado ni kero kabisa katika Wilaya ya Chunya. Kuna tatizo la mirathi, mirathi ambazo zinaombwa ili kusudi angalau zitekelezwe. Nasikitika tangu nimeingia kwenye Bunge hili, mirathi yote ambayo nimeipeleka Serikalini ili kusudi ishughulikiwe, mpaka hivi sasa haijashughulikiwa. Naomba Serikali ifikirie namna ya kuishughulikia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni malipo ya Bima, hasa kwa Walimu ambao tunajua kabisa matatizo yao jinsi yalivyo. Bima katika Wilaya ya Chunya zimeiva na zimeshapita wakati wake. Bima nyingine zilikuwa zilipwe mwaka 2005, lakini mpaka hivi sasa hazijalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kwenda kwenye Wizara inayohusika, wanani pa matumaini tu, sasa huyo mtu anayeitwa Matumaini, mimi nilifikiri angalau sasa hivi aanze kufikiria kwamba zile ni fedha za watu, fedha ambazo Serikali iliingia mkataba na hawa wafanyakazi, kwa hiyo, ninaomba itekeleze yale masharti ya mkataba kwamba walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la ujasiriamali. Wenzangu wamelizungumza, lakini mimi kwa uchungu kabisa, kitu kilicho jitokeza ni hizi fedha za JK katika Wilaya yangu na hasa Jimboni kwangu, kwa kweli ni habari za kusikitisha sana. Fedha zilizotolewa Jimboni kwangu hakuna hata mmoja aliyweweza kupata. Mimi nikashangaa na kujiuliza kuna nini? Hela zimeletwa Wilayani kwa ajili ya Majimbo yote mawili, lakini Jimbo langu halikupata, hivi kweli Serikali ilikuwa haijui kwamba kuna Jimbo la Songwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza kwa uchungu na bahati nzuri, aliye kuwa Waziri katika nafasi hiyo nilimwendea na ye ye mwenyewe alishangaa na akania hidhi kwamba basi awamu ya pili Jimbo la Songwe litaanza kushughulikiwa. Awamu ya pili imeshaanza kushughulikiwa, hakuna dalili hata kidogo za kuonyesha kwamba Jimbo la Songwe litapata huo mkopo kwa wale wote waliokuwa wameomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niikumbushe Serikali kwamba Jimbo la Songwe ni mionganoni mwa Majimbo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la mifugo. Naipongeza Serikali kwa kutekeleza ile azma yake ya kujaribu kulifanya Bonde la Songwe liwe bonde la hifadhi ya maliasili. Baadhi ya mifugo iliyotoka Ihefu, imeletwa kwenye Jimbo la Songwe, kwa hiyo, ule unafuu tuliuopata Ihefu ambao sasa hivi tunajivunia, Songwe ndiyo imehamishiwa matatizo, siyo kusema kwamba haikuwa uamuzi usiokuwa na busara, hapana. Tuna maeneo mazuri tu ya ufugaji kule, lakini ahadi ya Serikali ilikuwa katika maeneo yale iwekwe miundombinu itakayoifanya ile mifugo iendelee kuishi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliahidiwa Malambo, tuliahidiwa Majosho, lakini mpaka hivi sasa hakuna kinachofanyika, matokeo yake ni kwamba wafugaji wanafuata mahali ambapo kuna huduma hizo na sehemu ambayo ni kubwa zaidi, wanakokwenda ni kwenye bonde ambako ndiko kunakofanyika kilimo cha kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kwamba wakati Serikali inapoamua kutekeleza azma yake, basi itekeleze itatusaidia sana sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi dakika tano zilizobakia kuna mambo ambayo kwa kweli mimi bado yananitia shaka huko tunapokwenda. Tumeendelea na suala la ufisadi, Meremeta, Kiwira na suala la *Richmond*. Mimi mpaka hivi sasa nashangaa kwa sababu yote haya tumekwishayazungumza na yametolewa uamuzi. Kitu kinachonishangaza ni kule kuendeleza haya maneno, tena hatuendelezi sijui sehemu gani, ni humu humu ndani ya Bunge ambapo ndipo chanzo chake kilipoanzia.

Mimi nilikuwa nafikiri kwamba suala ambalo tayari limekwishaamuliwa, basi turejee hizo hatua ambazo zitachukuliwa ili kusudi tusitoe kwa maadui wetu. Haya masuala ya ufisadi ni masuala ya kiusalama na maadui tunao wengi wanaotafuta mwanya wa kuweza kupenyeza ili kusudi wavuruge mwelekeo wa nchi yetu.

Mimi nilikuwa nafikiri kwamba ifike mahali tuamini kwamba yatashughulikiwa, itatusaidia sana, na ninazungumza hivyo kwa sababu mambo ya usalama, mimi ni mwanausalama, najua matatizo ambayo yanaweza yakatutokea na sasa hivi yameshaanza kutokea. Wengine wanazomewa wanapopita barabarani, sasa wewe mtu tu wa kawaida unakwenda kumzomea kiongozi, maana yake ni nini? Ile *integrity* ya Serikali ipo wapi? Ni kwa sababu tunayaaendeleza humu ndani! Kuna mjumbe mmoja amesema kwamba hivi Viti vya Bunge visingekuwa na nati tungeweza tukagongana hapa. Maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana na ninaunga mkono hoja hii.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na papo hapo ili nisije nikachanganyikiwa mbele, napenda nitamke mara moja kwamba naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu. Vilevile natamka kwamba naunga mkono mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati ya Kanuni, Katiba Sheria na utawala ambayo mimi pia ni Mjumbe wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo ni fasaha, nzuri sana, yenye kina na kwa kweli inaashiria maendeleo mema katika miezi 12 ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu pia ziwaendee Mawaziri pia walioko chini yake, Mheshimiwa Marmo, Mheshimiwa Kombani bila kuwasahau Makatibu Wakuu, Ndugu yangu Vicent Mrisho na Mama yangu Tarishi

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia mambo yanayohusu Serikali za Mitaa kwanza, halafu baadaye kama muda utaruhusu, nitazungumzia mambo ya jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo ningependa kwanza nianze na suala la maslahi ya Madiwani ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana. Mimi ningependa Ofisi ya Waziri Mkuu, itufafanulie suala la posho. Hakikutajwa kiwango na mimi ninahisi kwamba huenda kinazungumzwa kiwango kile cha Sh. 60,000/= ambacho kilikwishaongezwa tangu mwaka jana. Kama hivyo ndivyo, nadhani bado ipo kazi, wanapaswa kuzidi kulitazama kwa lengo la kuboresha maslahi ya hao ndugu zetu.

Mimi sioni mantiki ya kusema hao Madiwani wasilipwe mshahara walipwe posho tu. Sisi Waheshimiwa Wabunge tunalipwa mshahara, tunalipwa posho na hao Madiwani ni Wabunge wadogo katika maeneo yao. Sioni kwa nini wao wasilipwe mshahara. Isitoshe kama tunazungumzia shilingi 60,000/= kwa mwezi kwa kweli ni kuwadharau. Kwa sababu hata kima cha chini cha mshahara katika nchi hii ni kiko zaidi ya hapo.

Nadhani kama sikosei ni shilingi 100,000/=. Sasa huyo Diwani ambaye tunampa shilingi 60,000/= kwa kweli tunamlipa sawa labda na mtumishi wa nyumbani au *bar made* hivi, kwa sababu nao wanalipwa kiwango hicho hicho. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa pia napenda nihoji uhuru wa Serikali za Mitaa. Napenda ifahamike kwamba Serikali za Mitaa ni mkono au uwakala wa Serikali Kuu. Kwa nini basi Serikali za Mitaa ziwe zinabanwa kama ilivyo hivi sasa. Vyanzo vyote vya mapato vikubwa imehodhi Serikali, na sisi kwenye Serikali za Mitaa tumepewa mapato madogo madogo tu, tunashindwa kujitegemea. Na kama mtakumbuka Hayati Julius Kambarage Nyerere alisema waziwazi kwamba Serikali Kuu ni Serikali *it is own right* vilevile Serikali za Mitaa nayo ni huru na ina huru kamili wa kuendesha mambo yake. Ni kweli kwamba hatuna uwezo huo, lakini mimi nadhani ni suala tu la kuwajengea uwezo na watakuwa huru zaidi kuliko hivi sasa tunawawekea mipaka kwa kila kitu.

Mimi nafikiri tungewapa huru na kulegeza ule udhibiti wetu wa viwango vya mapato ili kusudi waweze kuendelea. Serikali ingekuwa kazi yake ni kuweka *guidelines* wasivuke mipaka fulani. Mimi nadhani inabidi tuachane na mazoea ya kuzitazama Serikali za Mitaa kama ni watoto wadogo au kuzitazama kama omba omba hivi. Kwa sababu peke yao hawawezi. Hata zile ruzuku zinazotolewa bado zinatumika zile za viwango vya mwaka 2002 wakati tulipofuta kodi ya maendeleo. Mimi sielewi kwa nini? Hatujali kwamba toka wakati ule kumekuwana kuanguka au kushuka kwa sarafu yetu ya fedha, kumekuwa na mfumuko wa bei na mambo kama hayo. Kwa hiyo, mimi sioni kwa nini tunafumba macho kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulizungumza hilo yaani nataka kusema kwamba suala hili kama tunazungumzia ile shilingi 60,000/= wajitahidi kuona kwamba kama wanaweza kuwaongeza zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie katika suala la umwagiliaji. Kwanza, hapa napenda nitoe shukrani zangu nyingi sana kwa Serikali, imeweza kutoa kama shilingi milioni 650 kwa ajili ya miradi mitatu Kiwele, Cherehani mpaka Mkonga na vilevile mradi wa Tanangozi *Drip Irrigation*. Hata hivyo, nafikiri ni wakati muafaka Serikali itusaidie katika Wilaya yangu, waandae mpango au programu ya muda mrefu ili zinapopatikana fedha au fursa, tuwe tunajua mara moja ni nini cha kufanya kuliko kutumia utaratibu wa zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni juu ya hospitali ya Wilaya ya Iringa. Napenda niishukuru Serikali na Kanisa Katoliki la Iringa. Kanisa Katoliki la Iringa kwa kutoa hospitali waliokuwa wameanzisha na kuiendesha kwa miaka mingi ili itumiwe na Serikali kama hospitali ya Wilaya. Hospitali hiyo ni ya Ipamba, Misheni ya Tosamaganga. Napenda kwa niaba ya wananchi wa kule, niseme ahsante sana kwa pamoja, uongozi wa Kanisa hilo na vilevile Serikali. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisemee habari ya barabara. Halmashauri ya Iringa *TANROADS* na *TASAF* wametengeneza barabara zilizo nyingi katika Wilaya na kwa hiyo, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kabisa. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna barabara mbili au tatu zinatupa taabu. Barabara ya kwanza ni barabara ya Iringa-Msembe, hii barabara ni ya Mkoa japokuwa huwa inatengenezwa. Kwa kawaida, inapaswa iwe ya lami kwa sababu ya umuhimu wake. Barabara hii ndiyo inayokwenda *Ruaha National Park* na kama inavyojulikana, tukiiza utalii barabara hii itakuwa na umuhimu mkubwa siyo tu kwa eneo letu, lakini pia kwa Taifa kwa kuongeza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ni ile barabara kuu ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya kupidia Morogoro sehemu kadhaa hasa sehemu za Mafinga, Ruaha Mbuyuni kuelekea Mikumi zimeharibika, zinahitaji matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa kuhusu uanzishwaji wa Kata mpya katika Jimbo langu. Mwaka 2004 tuliomba Kata mbili mpya, Kata iitwayo Luota itokane na Kata ya sasa inaitwa Magulilwa na Kata ya pili mpya inaitwa Lwamgungwe, itokane na Kata ya sasa ya Mgama. Mchakato huo ulikwishaanza na ninachoomba hapa ni kwamba ukamilishwe ili kusudi Kata hizo mpya zianzishwe kabla ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mfupi uliobaki nizungumzie juu ya barabara ya lami Iringa-Dodoma na nimekuwa nikizungumzia barabara hii kwa muda mrefu sana. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana, upembuzi yakinifu umekuwa ukifanyika mara nyingi katika kipindi cha miaka 12 iliyopita, lakini hatuendi popote na mara ya mwisho ni mwaka huu wa fedha zilitengwa Shilingi milioni 950 kwa ajili hiyo hiyo. Nilitegemea mwaka huu wa fedha basi tungkuwa tumetengewa fedha ya kutosha kuweza kupiga hatua zaidi. Lakini cha kushangaza ni kwamba zimetengwa Shilingi milioni 574 tu kwa mwaka ujao wa fedha kwa upembuzi yakinifu, yaani huwa tunapiga hatua moja mbele halafu hatua mbili nyuma. Kwa maana hiyo, hatujaweza kupiga hatua na kwa mtindo huu nina hakika hatutafika popote. Sitaki nisisitize kwa sababu inajulikana umuhimu wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachoshangaa sasa ni kwamba, inaelekeea kuna aina fulani ya upendeleo. Kwa sababu hapa katikati kumekuwa na barabara nyingi sana ambazo zimetengenezwa, nyingine za vichochoroni majina hatukuyajua, fedha zimepatikana. Lakini barabara hii ambayo tumeanza kuipigia kelele kwa muda mrefu haitengenezwi. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati tuweze kupiga hatua juu ya suala hili. Loh! itabidi niruke ruke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii, kule kwetu tuna hifadhi kama tatu, *National Parks Ruaha*, Kitulo, Udzungwa na vivutio vingi tu vya kihistoria na utamaduni. Lakini kwa sababu ya upendeleo wa miaka mingi, eneo letu la Kusini halikuweza kustawisha utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza juu ya barabara ya Msembe kwa ajili hiyo na pia tuna kiwanja cha ndege kizuri tu ambacho kimejengwa tangu wakati wa ukoloni, lakini hakitumiki ipasavyo. Ninaomba Serikali, kwa sababu za kihistoria ni vizuri sasa Serikali itambue umuhimu wa kutusaidia sisi watu wa Mkoa ule ili tuweze kuanzisha utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kitu kinaitwa *Southern Tourist Circuit* ambayo Wizara husika inafahamu. Ninaomba sana Wizara hiyo itume watalaan wake waje wakae nasi kule Iringa tuweze kuzungumza na kuafikiana vipaumbele na namna tunavyoweza kulishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda uliobaki ni mdogo sana na nilikuwa nataka kuzungumzia na mambo ya utawala, sitaweza kufafanua kila kitu. Kwa hiyo, niseme tu yale ambayo ninafikiri inafaa Ofisi hii ya Waziri Mkuu iyatazame. Kwanza kabisa, nina hakika kwamba bado hatujafaulu kuviwezesha vijiji vyetu kupanga maendeleo yake kama *D by D* inavyotaka.

Pili, vilevile sioni mantiki ya kuwa na Serikali mbili, yaani Serikali Kuu na Serikali ya Mitaa, ngazi ya chini ya Wilaya.

Tatu, mfumo uliopo sasa wa washauri kule Mkoani siyo mzuri na kwa kweli kwa maoni yangu ni mzigo kwa sababu tumelundika wataalam kule ambao hawana *linkage* na Wilaya zetu ambapo ningetegemea wawe wanasediwa. Lakini kwa uwezo wangu wa miaka mingi, nimeanza kazi toka mwaka 1951 katika Utawala, kwa hiyo, ninavyojuu mimi, hakuna *linkage* na kwa hiyo, hao ndugu zetu wanaelea tu pale. Halafu wamenyang'anya hata vyeo vyao kama ni *Regional Heads, Regional Education Officer, livestock* sijui kitu gani, sasa wanaelea tu. Hawana *job descriptions*, hata kazi wanazofanya hazina *legal authority*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Galinoma naomba uunge mkono hoja.

MHE. STEPHEN J GALINOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Yaliyobaki nitayawasilisha kwa maandishi. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Galinoma ahsante sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Mosses Mlata na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ajiandae.

MHE. PROF. PHILLEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii adimu ili niweze kuchangia hotuba iliyo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja hii. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake ambao ni Mawaziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara kwa hotuba iliyoandaliwa vizuri kitaalam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie hotuba hii ya Waziri Mkuu katika maeneo mawili yafuatayo: Kwanza, ulinzi na usalama. Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba kwa ujumla mipaka ya nchi yetu ni shwari. Hata hivyo mipaka ya nchi yetu katika baadhi ya Mikoa siyo shwari hasa Mkoa wa Mara, Kigoma kwa watani wangu, Kagera na Rukwa. Katika Mikoa hiyo wananchi kwa miaka mingi wamedhalilishwa, wameuawa, mali zao zimeporwa na majambazi kutoka nchi jirani. Hivi Tanzania hatuna ulinzi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchungu na masikitiko, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2006 hadi Juni mwaka huu katika Wilaya yangu, majambazi kutoka nchi jirani wameiba ng'ombe 1700 na kuua watu watano na kujeruhi wawili. Tukio la juzi katika Kijiji cha Buganja, Kata ya Buko, Tarafa ya Gilangololi, majambazi hawa walikuja zaidi ya 10 na silaha za kisasa *SMG*, wamepora ng'ombe na kuua watu wawili na kujeruhi wawili. Sasa wananchi wangu wamenituma nifikishe ujumbe na maombi yao kwa Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Pinda, ambaye pia na yeche na Mwanarorya na ni mwenzetu, siwezi kueleza kwa sababu ni mwana Mwanarorya. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kusaidiwa katika mambo yafuatayo: Kwanza, Wilaya ya Rorya. eneo la Rorya litangazwe kwamba ni eneo la maafa na hatari. Pili, wanaomba viwekwe vikosi vyetu vya *FFU*, *STPU*, *JWTZ* Wilayani Rorya na ng'ombe walioibwa na kupelekwa nchi jirani wasakwe na warejeshwe mara moja. Kinyume cha hapa, sisi tutafuata wenyewe wananchi wa Rorya. Pia fidia ilipwe kwa mambo yalioyotoka. Watu waliouawa, waliojeruhiwa na ng'ombe.

Tatu, Kamati ya Ulinzi ya Mkoa chini ya Luteni Kanali MsaaFu, mpiganaji hodari sana, ndugu Machibya iwezeshwe. Hana silaha za kutosha, hana polisi wa kutosha na magari hayapo. Pia vituo vya Polisi vya mpakani Utigi, Sota, Nyang'ombe, King'esi, Kokojya, Vanyakoi, Shirati na Kilongo vipatiwe pipikipiki, magari na silaha. Wanamgambo tunao wengi wanaomba silaha. Tunataka kulinda mipaka yetu. Mtu huwezi kwenda nyumbani kwa mtu unaingia tu kama mwenyewe hayupo halafu unatoka bila kuadhibiwa. Ebo! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaomba vituo vipyta vya Polisi viongezwe vya Bukwe na Eraguro. Wanaomba kwamba lifanyike zoezi la kuwasaka hawa majambazi na silaha ndani ya nchi yetu na nje ya nchi wanakotokea. Wakipatikana kwa kushirikiana na nchi hiyo, siyo kwamba tutavamia nchi hiyo, uwezo wa kuingia tunao, lakini hatutaki. Wakipatikana waadhibiwe. Wanaomba kwamba dhana ya ujirani mwema hawataunga mkono. Huwezi kusema huyu jirani mwema na mwenzako hataki kuwa jirani mwema, wewe ndiyo uwe jirani mwema, inawezekana wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, wananchi wa Rorya wana imani na Rais wetu - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na wana imani na Serikali yake inayoongozwa na ndugu yetu mwadilifu, mimi nimemfahamu Pinda nilipokuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Muhimbili yeche alikuwa Ikulu. Wanaomba na natoa shukurani hizo. Wanashukuru, lakini wanampongeza

pia kwamba aliwaahidi kuwapatia Wilaya na aliwapatia, baada ya mwaka mmoja akawa hapa, lakini tatizo hawana Mkuu wao wa Wilaya. Bado hajateuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa ateuliwe aje Rarya, aongeze nguvu kwa sababu Mkuu wa Wilaya mmoja wa Tarime ndiye anaunganisha hata na Wilaya ya Rarya. Hatuwezi kuchezewa kama watoto wadogo. Sisi wanatujuja jirani zetu, juzi wameiba ng'ombe sehemu fulani huko Tarime wananchi walifuata ng'ombe wakarejesha. Laiti tungekuwa na silaha hawangetuchazea hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Rarya walioathiriwa, napenda kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - kijana wangu Mheshimiwa Masha, Naibu wake, mjukuu wangu, Balozi Kagasheki, *IGP*, Mkuu wa Mkoa kwa kuchukua hatua za haraka nilipowaeleza tu.

Kwanza, nilimweleza huyo anayefuata anashindana na mimi mwenye upara, huyo Mheshimiwa Kagasheki. Nilipomweleza tu, hakusita, aliwaarifu wakubwa wake na kesho yake wakatuma Maafisa wa ngazi za juu kwenda kuchunguza hali halisi.

Lakini zaidi nampongeza Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya jinsi walivyoshughulikia hali hiyo. Hata hivyo naomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kijana wangu twende naye Rarya, ili aweze kutoa kauli ya Serikali kuhusu janga hili na kuwafariji wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara, sisomi, si unaniona na wewe! Barabara ni uhai wa Taifa katika kukuza uchumi. Katika ukurasa wa saba zimetajwa barabara zote, lakini barabara ya kutoka Butiama, Nyamuswe, Bunda, Mgumu hata mto wa Mbu hakuna na barabara hii ilishafanyiwa upembuzi yakinifu, kulikoni? Naomba kauli ya Serikali kuhusu barabara hii katika Mkoa wa Mara.

Lakini ili tuweze kuimarisha ulinzi katika Wilaya ya Rarya, naomba Serikali ipandishe barabara hii ambayo inatuunganisha na Wilaya ya Tarime na Nchi jirani ya Kenya katika kwa kiwango cha lami. Barabara hiyo ni kutoka Kuruya, Utegi, Mika, Shirati, Sota, Sota, Kilongwe na Silai. Tukitekeleza hayo, kazi itakuwa rahisi kwa Mkuu wa Mkoa na Ulinzi wetu. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa la Manchila, ni zaidi ya miaka nenda rudi, kulikoni? Miaka 31 jamani, hivi hawa watu wa Serengeti siyo Watanzania? Naomba hayo niliyoyasema hasa kilio cha wananchi yatekelezwe na ng'ombe warejeshwe fidia zilipwe. Kama Serikali haitasikia, sisi tutachukua hatua ya kurejesha ng'ombe zetu walizoiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofifi*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa, napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya siku ya leo na kuweza kupata nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii. Pia, ninakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida, ninapenda kutoa

shukrani zangu na pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo aliitoa yenyе matumaini na yenyе kujaa neema kwa ajili ya Watanzania.

Hotuba hii nasema kwamba imejaa matumaini yenyе kujaa neema pale tu endapo watumishi wetu na watendaji maofisini watazingatia yale yote ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyaainisha katika hotuba yake wakayatendea kazi kwa uaminifu, nchi yetu itapata baraka na itazidi kuinua uchumi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba nikwambie kwamba mimi ni Mbunge wa Mkoa mzima wa Singida. Hivyo basi, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida naungana pia na Wabunge wote wanaotoka Mkoa wa Singida kupitia Bunge lako Tukufu niweze kutoa shukrani zetu za dhati kabisa, tena kwa moyo mkunjufu kwa Mkuu wetu wa Mkoa ambaye amekuwa ni Mkuu wa Mkoa wa kwanza kuupenda Mkoa wetu wa Singida. Kwa mapenzi mema anautumikia na kuhakikisha Mkoa ule unaondokana katika dhana ya kuonekana Mkoa ule ni wa mwisho. Hivyo, napenda kutoa shukrani hizi za pekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wetu wa Mkoa kwa kushirikiana na watendaji wote na wananchi wa Mkoa wa Singida wamejitahidi sana katika kujenga kiwanja cha Ndege pale Singida. Kiwanja kile kimekamilika. Hii yote ni katika harakati za kuhakikisha Mkoa wetu unapata miundombinu iliyо bora kwa ajili ya kuwawezesha wawekezaji kuweza kufika katika Mkoa ule ili kuinua Mkoa wetu wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo kubwa tulilonalo uwanja ule, kama Serikali haitachukua hatua madhubuti na za haraka, mvua zitakapofika uwanja ule na fedha zile zitakuwa zimeteketea kama hautawekwa lami. Hivyo ninaomba Serikali ichukue hatua madhubuti kutoa fedha za kuweka lami katika uwanja ule na isiwe kidogo kidogo, itoe fedha, lami iwekwe uwanja mzima.

Lakini pia napenda kuishukuru Serikali kwa ajili ya barabara. Barabara ya kutoka Dodoma mpaka Shelei, ninaishukuru sana Serikali kwa sababu sasa hivi barabara ni nzuri. Lakini tatizo bado liko kuanzia Chikuyu mpaka Isuna. Hivyo, ninaomba Serikali isije ikaanza tena kusuasua na mwaka huu barabara ile ikashindwa kumaliziwa. Kwa sababu hicho ndiyo kichocheo kikubwa cha maendeleo katika mkoa ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida ni Mkoa kame, hivyo basi hivi karibuni niliuliza swali la nyongeza na Mheshimiwa Naibu Waziri, yaani mtaalam wa umwagiliaji, Mheshimiwa Eng. Chiza alijibu kwamba kuna utaratibu ambao umewekwa na Waziri atakuja kutolea tamko juu ya gawio kwa ajili ya miradi ya maji. Hivyo basi, ninaomba sana Mkoa wetu wa Singida ukumbukwe. Kama nilivyosema, kuna vijiji vingine vinapata shida ya maji, watoto na akina mama kama walivyozungumza wazungumzaji waliotangulia. Tafadhali sana ninaomba mtusaidie suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la afya. Afya kwa akina mama, uzazi salama, ninaomba niulize Serikali: Je, tangu imeanza kuweka mikakati ya

kupunguza vifo vya akina mama na watoto ama baada ya kujifungua au kabla ya kujifungua imefanikiwa kwa kiwango gani? Kwa sababu bado tatizo hili ni kubwa sana.

Kuna wakati ambapo bajeti inapoletwa fedha zinakuwa zimetengwa, lakini zinakuwa hazifiki mahali husika. Tatizo wakati mwingine wanasema kwamba vituo vingine havina wahudumu. Fedha zinatumika kidogo, nyingine zinarudi Hazina. Sasa mimi ninasema kwa nini fedha hizi zirudi Hazina? Kwa nini zisiende kufanya mikakati mingine ya kuondoa yale matatizo ambayo wale wahudumu hawawezi kufika kwa ajili ya mazingira magumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana tuwahurumie akina mama, hasa walioko vijijini, wanapata tabu; kuna mzungumzaji mmoja alisema kwamba, wagonjwa wanabebwa kwenye matenga; unafikiri ni akina nani? Ni akina mama wanaokwenda kujifungua. Kwa hiyo, tafadhali sana, ninaomba sekta hii itiliwe mkazo ili kupunguza vifo vya akina mama. Hivi kuna ubaya gani, pesa ambazo zinakuwa zinatengwa kama hazijatumika; kwa nini zisinunuliwe hata *pick-up*, kwa sababu kuna wakati niliwhi kuzungumza, si lazima tununue *ambulance*, bei ni kubwa? *Pick-up* zitasaidia akina mama na zitaokoa watu wengi. Mama anabebwa kwenye kitanda au kwenye baiskeli kupelekwa hospitali, haiwezekani; huu ni udhalilishaji na ni unyanyasaji.

Ninasema ni udhalilishaji na ni unyanyasaji, kama ni ufisadi huo ndio ufisadi. Mwanamke kufa njiani eti kwa sababu ameshindwa kufika hospitali; vituo vya afya vimejengwa havina wauguzi; kama siyo ufisadi ni ufisadi gani mwingine wa kuacha akina mama wafe njiani eti kwa sababu tunasubiri *ambulance*, pesa zinarudi Hazina? Kwa hiyo, ninaomba sana fungu linapotengwa litumike barabara, litatue tatizo moja baada ya lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Sheria ya Ndoa, itawagusa wengi lakini huo ndiyo ukweli. Ninaiomba Serikali inieleze imeitekeleza vipi Sheria ya Ndoa iliojiwekea na kwa kiwango gani, kwa sababu akina mama wengi wamekuwa wakidhalilika kutokana na Serikali kutokutimiza na kutekeleza Sheria ya Ndoa? Mama anapofiya anafukuzwa kama alivyokuja; je, huo si ufisadi? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mungu amekuweka katika nafasi hiyo. Tafadhali ninakuomba utetee akina mama. Akina mama wanapoachika kwa waume zao, wanaondoka kama walivyokuja. Kesi zikienda Mahakamani, haziishi miaka nenda rudi. Mheshimiwa Waziri, Mungu amekuweka utetee wanawake. (*Makofi*)

Ninataka kusema kwamba, kuna wengine wananiuliza je, wanaume? Ninataka kuwaambia, Mungu atakaposhuka kuingilia kati suala la Sheria ya Ndoa ni hakika kawaaulizeni wanaume wanaoishi Uingereza na katika mataifa mengine. Hii ni kwa sababu, sheria zilipowekwa wa kwanza ni mtoto anafuata mwanamke; anafuata paka na mbwa halafu ndiyo mwanaume. Kwa hiyo, ninaomba Sheria ya Ndoa inayowalinda wanawake na haki zao. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde.

MWENYEKITI: Ongea na Mwenyekiti Mheshimiwa Mlata.

MHE. MARTHA M. MLATA: Nilijua itawagusa wengi. Huo ndio ukweli, kina mama wananyanyasika sana kwa sababu hata Mahakamani wanaume walio wengi ndio wamekalia zile sheria, ndio maana wanawake wanapata matatizo. Ndiyo maana vilevile hata watu wamekuwa wakipiga kelele kuhusu Mahakama; *is it Kadhi?* Ndiyo Mahakama ya Kadhi. Hili lote ni kwa ajili ya kutaka kumtetea mwanamke, hakuna kitu kingine na mnalijua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Sheria ya Ndoa, ichukue mkondo wake au irekebishwe. Wanaume andikeni wosia; watoto wenu wanapata matatizo pale mnapoondoka duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia kuhusu suala la elimu. Bajeti iliyotengwa ni kubwa sana, tumesema tumeweka kipaumbele kwa ajili ya elimu.

MHE. MOHAMED RAJAB SOUD: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Kanuni?

MHE. MOHAMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(b): “Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo haliko kwenye mjadala.” Anamfananisha mbwa kwamba, ni mzuri zaidi kuliko hata wanaume, naomba asawazishe kauli yake. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante. Nadhani alivyokusudia Mheshimiwa Mlata ni kwamba, Uingereza Sheria ipo hivyo. Alikuwa anafafanua Sheria ya Uingereza, siyo Tanzania. Kwa hiyo, nafikiri hakuna tatizo, mwache aendelee kumalizia tu. (*Makofi*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Naomba muda wangu ulindwe, pamoja na hayo basi, ninaomba radhi kwa kufananisha hivyo, lakini ni Sheria iliyoko Uingereza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia elimu kwamba, bajeti iliyotengwa tunaiona ni kubwa sana. Je, hii Wizara ilikuwa ni Wizara iliyounaganishwa; Elimu ya Juu, pamoja na iliyokuwa Wizara ya Elimu? Je, hizi pesa Wizara au Serikali ina uhakika kwamba zitatosheleza mahitaji yote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu suala la Waandishi wa Habari. Hapa nchini kuna chuo kimoja tu ambacho kinatoa Shahada ya Uandishi wa Habari. Waandishi hawa wanahitaji kuijiendeze ili waweze kufanya kazi yao kwa umakini zaidi. Wanapotaka kuchukua Shahada ya Pili, inabidi waende nje ya nchi. Je, Serikali haioni kwamba Waandishi hawa wa Habari hawawezi kumudu kujigharamia

kwenda kusoma *Masters* huko nje ya nchi? Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kutenga fungu la kwenda kuwasomesha waandishi wetu ili tuweze kupata wahariri wazuri, ambao watafanya kazi kwa maslahi ya nchi yetu na Taifa letu? (*Makofi*)

Waandishi wa Habari pia wamekuwa wakiandika habari nyingi sana za mijini. Hii ni kutokana na kwamba, huenda wanakosa zana au nyenzo za kufanya kazi kwenda vijijini. Serikali ina mikakati gani ya kuwawezesha hawa kwenda vijijini kuibua maendeleo yaliyoko kule na mambo yaliyoko kule, hawawezi kufika kwa sababu hawana vitendea kazi?

Siku moja nilikuwa nasoma kwenye *blog* ya Michuzi, nikaona picha ya mwanamke amebebwa kwenye tenga anapelekwa hospitali, anasema hizi ndiyo *ambulance* za vijijini. Hilo limewekwa hata mtu anapoliona anapata hisia ya kutaka kufanya maendeleo mahali kule kwa sababu aliwezeshehwa akafika. Kwa hiyo, tuwawezeshe Waandishi wetu wa Habari. Serikali iweke mikakati mizuri ili kuweza kushirikiana nao, kwa faida ya nchi yetu na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie Lugha ya Kiswahili; nikiongea haraka haraka, Kiswahili tumesema kwamba ni Lugha ya Afrika, lakini bado sisi wenyewe tumekuwa hatuitumii. Ulifanyika mkutano mkubwa wa *Sullivan* hapa Tanzania; vyombo vyote vya habari vilionyesha, ule mkutano mzima uliendeshwa kwa Kiingereza. Watanzania wengi walitaka kuangalia na kufuatilia, lakini kwa sababu sisi wenyewe hatujajifunza Kiingereza tangu tukiwa wadogo na hakuna mtu aliyeona faida ya kuendelea kufuatilia ule mjadala; kwa nini sisi hatukutaka kui-*promote* lugha yetu? Watu wamekuja hapa, kwa nini wasiwekwe wakalimani tukatumia Lugha yetu ya Kiswahili? Kwa hiyo, niliona nilzungumze hilo ili Serikali ionyeshe mfano wa kutaka kui-*promote* Lugha yetu ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mlata. Waheshimiwa Wabunge, wenzetu Ulaya ndoa ni pamoja na kutambua Sheria za Ndoa na ndoa za jinsia moja, ambayo Tanzania tupo tofauti. Hivyo, kule Ulaya familia ni pamoja na paka na mbwa. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Mlata alipokuwa akifafanua hilo, liliwashtua kidogo baadhi ya Wabunge.

Tuendeleee, sasa namwita Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, atafuatiwa na Mheshimiwa Haroub Said Masoud na Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami ajiandae.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, naona jina langu linakupa tabu sana, lakini ortalizoea taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Pinda, kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu. Naomba nimpongeze kwa hotuba yake nzuri, pamoja na Mheshimiwa Celina Kombani na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Katibu Mkuu

na Ofisi yao yote. Hakika wamekuwa msaada mkubwa, hususan kwa Wananchi wa Kilindi. (*Makofî*)

Aidha, natoa shukrani zangu za awali; jana nilipata fursa ya kuhudhuria Kamati ya Fedha Wilayani Kilindi, ambapo niliwapa taarifa ya kuchangia kwangu, wakanituma salamu na shukrani kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali, kwa huduma mbalimbali ambazo wamekuwa wakipatiwa. (*Makofî*)

Wameshukuru kupitia hotuba yako na taarifa za awali, kuhusu umeme ambao wameahidiwa kupatiwa hadi kufika Makao Makuu ya Wilaya na sisi tutafanana angalau kidogo na wengine. Vilevile, wameshukuru sana kwa fedha za barabara, kwa mara ya kwanza katika historia; Makao Makuu ya Wilaya ya Songe yamefikika hata wakati wa masika. Hii inaonyesha jinsi ambavyo tumeweza kusaidiwa. (*Makofî*)

Vilevile nitakuwa mnyimi wa shukrani kama sitamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu; binafsi napeleka shukrani zangu pia kwa Waziri Mkuu wa awali, ambaye alistaafu muda mfupi uliopita, kwa kupendekeza kuunda Kamati ya Kusuluhiha Mgogoro wa Ardhi ambao ulisababisha mauaji ndani ya Wilaya ya Kilindi na Kiteto. Walituma Kamati, Mheshimiwa Pinda aliweza kuvisimamia kwa kasi na imefanya kazi yake, tunashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina vipengele vichache lakini nitaenda haraka haraka, mtaniwia radhi lakini naona sote huwa tunaelewa hata ninapoongea haraka haraka. Katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri Mkuu umezungumza vizuri, lakini nilikuwa naona kwamba, kwa sababu mimi naamini sana kwenye kumbukumbu, kwa vizazi vijavyo; nilidhani labda kwenye hotuba yako hii, kulitokea mabadiliko makubwa sana ya uongozi ndani ya Serikali yetu kwa sababu mbalimbali. Nilidhani ni muhimu likawa *documented* katika *speech* yako ili hata siku za mbele ambazo sisi hatupo, liweze kusomeka kwamba, mabadiliko makubwa ya Serikali kabla ya wakati wake. Hilo lilitakiwa lioneokane. Vile vile nilidhani pia, heshima kubwa tuliyopewa ya Rais wetu kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika ni jambo kubwa sana, ambalo ni la kihistoria na lilitakiwa liwekwe ndani ya hotuba hii. (*Makofî*)

Aidha, niseme awali kabisa, katika jedwali lako hili kuna masahihisho kidogo, ambayo nimeyaona. Baadhi ya takwimu za Kilindi, nitawasiliana na Ofisi yako ili niweze kuzipata. Moja kubwa, ambalo jana lilijitokeza hata kwenye kikao ni idadi ya Vituo vya Afya na Zahanati. Tusije tukanyimwa fedha, tunavyo vituo viwili vya afya ambavyo havikuonekana. Vilevile nasema kwamba, kuna tathmini ambayo imefanyika ndani ya Wilaya ya Kilindi, nadhani na Wilaya nyingine nyingi, ambayo ni upimaji wa kuiwezesha Halmashauri kupata ruzuku ya maendeleo, ambayo ilikuwa inaangalia miaka ya 2006/2007. Katika Wilaya ya Kilindi, nasikitika kusema kwamba, sisi tumepelekea hiyo tathmini kwamba tukose fedha hizo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ndio ulikuwa Waziri wakati huo wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Unaelewa wazi kabisa, katika kipindi hicho tulikuwa hatuna watumishi ndio kwanza Halmashauri imeanza. Vilevile tulikuwa hatuna vitendea kazi na

Ofisi ndiyo kwanza ilikuwa inaanza. Sanjari na hiyo, tukaambiwa kwamba, pia hatuna Wakuu wa Idara. Ombi la Wakuu wa Idara lipo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, linasubiri uamuzi. Leo kwa sababu ya tathmini, tunaambiwa kwamba hatuna sifa. Tumekosa sifa ya kupata ruzuku hiyo. Wilaya changa kama ile kukosa ruzuku kwa sababu ambazo zipo nje ya uwezo wetu na ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu unafahamu kwamba, tulikuwa hatuna watu hao kwa wakati huo, naona kama kidogo hatujatendewa haki. Ninaomba sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu, uangalie tuweze kupata fedha hizo. Naamini kwamba, hilo linawezekana kwa kuzingatia hali halisi.

Naomba mnapokuwa mnafanya maamuzi katika Wilaya changa kama hizi na maeneo mbalimbali, muangalie aina ya maeneo, mazingira ya kijiografia na sababu mbalimbali zinazopelekea matatizo, kabla ya kufanya maamuzi kwa sababu tunatofautiana sana. Huwezi ku-*compare* Kilindi na baadhi ya Wilaya nyingi. Vilevile tunapata tatizo, baadhi ya huduma zinatoka *direct* Wizarani mpaka kwenye Idara. Kwa mfano, jana lilijitokeza wazi tatizo la dawa za mifugo. Unakuta Wizara ina-*deal direct* na Idara. Tunapomhoji Mkurugenzi, anakuwa hana taarifa inabidi yule Afisa aeleze. Kulikuwa na tatizo kubwa ambalo lilijitokeza la ugonjwa wa kichaa cha mbwa, ile dawa haitoshi, watu wanaathirika na wengine kufa.

Sasa tukajaribu kuuliza, lakini Mkurugenzi hana taarifa. Hii ni kutokana na taratibu ambazo zinatumika kwamba, kuna baadhi ya huduma zinatoka kwenye Wizara husika kwenda moja kwa moja kwenye Idara. Sasa ikiwa Halmashauri, yaani nikimaanisha Madiwani na Baraza lao, ndiyo wanaosimamia *oversight function* kule kwenye Halmashauri. Tutafanyaje wakati hatujui na Mkurugenzi ambaye tunastahili kumuuliza hajui? Ninaomba sana hizi huduma ikiwa tumeamua ku-decentralize, basi na mambo yote yatolewe taarifa tu angalau waweze kufahamu.

Vilevile kuna matatizo ya masharti mengine ya huduma mbalimbali ambayo ni magumu. Nitolee tu mfano, tulipewa shillingi milioni 70 kwa ajili ya ununuzi wa gari la kwanza la Mkurugenzi. Tukaambiwa kwamba, fedha hizo lazima zipitie Wizara ya Miundombinu, wao ndio wanaoagiza. Zoezi hilo limechukua muda mrefu kweli, lakini baada ya kufanikiwa tukaambiwa hapana mmechelewa, bei imepanda imekuwa shilingi milioni 117. Sasa tunatakiwa tuongeze shilingi milioni 45 hatuna. Shilingi milioni 70 tayari tumesha-*deposit* kwa *dealers*, hatuna hizo fedha. Ninaomba kwa ridhaa yako na uwezo wako, hizo shilingi milioni 45 tupatiwe katika mwaka huu wa fedha ili tuweze kupata hilo gari la kwanza.

Ukurasa wa 50 wa hotuba yako umesema Sheria ya Madini itafanyiwa mapitio katika mwaka huu. Wananchi wa Kilindi wanasubiri sana. Kama unavyojua mwenyewe, kule madini ndiyo msingi ambaa ni mkubwa sana na watu wengi wanategemea madini. Wachimbaji wadogo wadogo wanahitaji elimu na elimu hii ni ya Sheria ya Madini. Naomba uangalie sana, wameathirika kwa kiasi kikubwa, hivi ninavyoongea, kuna msafara wa wachimbaji wadogo umefika leo ukitaka kumwona Mkuu wa Mkoa na kupata usuluuhishi wa matatizo yao. Najua wanamsumbuu Mkuu wa Mkoa kwa sababu atakuwa hana jibu, Sheria ndiyo mbovu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, lingine ni kwamba, kumeundwa Kamati za Ukaguzi za Halmashauri. Hili nimeliona jana, pengine Wabunge wengi hawajui. Kamati hizi zina jukumu kama Kamati za Ukaguzi katika Wizara na Idara ambazo zinajitegemea, lakini siwezi kusemea sana kwa sababu ya muda. Huu uamuzi ulikuwa ni wa Agizo la Rais. Uamuzi ni mzuri, lakini ukiangalia Muundo wa Kamati na majukumu yake halitekelezeki. Hili nalisema sasa ni vema likaangaliwa mapema kabla shughuli hazijaendelea ili liweze kutekelezeka.

Kuhusu benki, mpaka leo Mheshimiwa Waziri Mkuu hatuna benki. Mahakama, Kituo cha Polisi ndiyo ile *post* tunaitumia, pamoja na kuwa na *OCD* na watu wote, lakini haya nitayagusia pia kwenye sekta husika nimeyaleta kwako kwa taarifa tu. Mara nydingi ninapotoka hapa nje na hata kila ninapopita, napokea toka kwa baadhi ya wananchi wengi tu, wanaanza kusema kwamba, mbona Bunge sasa hivi hoja zenu zinakuwa kama mnapambana; mbona kama kuna mpasuko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia hapa niseme na wananchi wanisikie; hakuna mpasuko wowote na wala hakuna ugomvi wowote ndani ya Bunge. Sisi hapa tunazungumzia hoja ambazo tunapewa na wananchi na nydinge sisi wenyewe tunazona, ndiyo tunakuja kuzisemea hapa. Wajibu wetu kuzipokea na waendelee kutupa na sisi ni wajibu wetu kuzisemea. Tatizo linalokuja ni moja tu kwamba, zile hoja zinapokuja, lazima zitahusu watu fulani fulani. Sasa hapo inakuwa ni bahati mbaya sana, ambapo inahu su mtu Fulani, lakini hatumlengi mtu tunalenga ile hoja yenewe. Ukweli unapojulikana, basi mambo yanakwenda jinsi yanavyokwenda. Nitake kuwashakikishia wananchi, sisi Wabunge ni wamoja; hajjalishi tumeingia kwa itikadi gain; kama ni viti maalum, viti vya kuteuliwa na kadhalika. Sisi lengo letu ni moja na nia yetu ni moja, kuhakikisha maisha ya Mtanzania yanatoka hatua moja kwenda nydinge.

Hii dhana ambayo inapita huko kwa kasi sana na wengine wanaiongezea kwa sababu zao, hakuna kitu kama hicho. Ikumbukwe kwamba, kila mtu ana namna yake ya kupitisha maoni yake na mawazo yake. Lengo letu ni lile lile moja, jinsi ya kufikia ni kila mtu na namna yake, lakini naomba niwahakikishie kwamba, hakuna ugomvi tupo kitu kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, baada ya kuangalia mambo yote haya, nimekuja kugundua kwamba, tatizo ni moja; Watanzania hatutaki kufikiri kabisa na wala hatutaki kuwa wabunifu. Hili limejionyesha sehemu nydingi sana, kwa mfano, kila kitu ukienda mara unasikia tunatekeleza Agizo, sijui Waraka, mara Mwongozo na vitu kama hivyo ambavyo vinatoka Serikalini; ni lini sisi tutajifunza kufikiri? Tatizo linalotukumba sana sisi ni kufikiri. Unaenda kwenye Halmashauri unauliza jamani kuna fedha fulani zimekuja; ndiyo zipo kwenye akaanti tumeziona; utekelezaji tunasubiri Mwongozo.

Siku moja nilikaa nikawaza sana; hivi tatizo letu ni nini; kitu gani kimetudumaza? Nikakumbuka hii inaanza hata kwenye historia tulipoanza awamu hii, zilianza semina elekezi kule Ngurudoto. Narudia, semina elekezi za kuelekezwa, kwa hiyo, kila mtu amekaa anasubiri kuelekezwa na sisi sote tumeduwa tunasubiri kuelekezwa badala ya kuwa ingekuwa semina shirikishi. Unaona kwamba, vitu vingine unashanga ni vya

ajabu, kwa mfano, barabara, unakuta mtu anajua mvua zinaanza baada ya miezi miwili; *engineer* anaanza kutengeneza barabara leo. Mvua inanyesha, barabara inakwenda hakuna kitu au unakuta barabara zinatengenezwa nusu nusu mradi tu ikamilishwe hela imekwisha, hamna kitu. Saa nyingine unakuta kwenye barabara linaanza shimo dogo, linaachwa linaendelea mpaka mwisho; wahandisi wako wapi?

Tumejenga shule, tuna watoto ambao wamefeli. Mimi nilifikiri labda tulivyojenga shule, kiwango cha mwisho cha elimu kitakuwa kidato cha nne. Hata hivyo, utashangaa mahali kama Kilindi, watoto 800 walimu wane; watafaulu vipi hawa watoto?

Sasa unashangaa kwamba, nilifikiria labda mtu atawaza kusema tuanzishe darasa moja la wale ambao hawakufanya vizuri, wapewe nguvu zaidi waweze kuendelea; hakuna anayetaka kufikiri. Walimu na wafanyakazi wengine, hawataki kwenda maeneo ambayo yana miundombinu duni. Hakuna mtu anayewaza kwenda, labda tuwape motisha fulani. Sasa nadhani hili ni tatizo na hata hapa Bungeni siku za karibuni, watu wamechoka kufikiri; unangoja mwingine aseme hoja, unarukia hapo hapo unaanza kukosoa na kupongeza. Tuwafikirie wananchi kwa pamoja. Naomba nitoe wito; wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara na wasomi wote; tuwe wabunifu na tufikirie. Tusingoje stadi sijui zitoke nchi za huko, wakati tunalamika rasilimali zinapotea; tutabaki kulalamika kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu wa mwisho, tufikiri tuache haya mambo madogo madogo yanayotuchelewesha. Tunaonekana wajinga, watu wanachuma wanaondoka. Mwisho, nasema Mungu atubariki Bunge hili, Mungu ibariki Tanzania, tufikiri kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Shellukindo. Sasa namwita Mheshimia Haroub Said Masoud, atafuatiwa na Mheshimiwa Ponsiano Damiani Nyami na Mheshimiwa Laus Omar Mhina ajiandae.

MHE. HAROUD SAID MASOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja hii. (*Makofii*)

Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wake, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Vilevile sitaki kuwa mwizi wa fadhila, naipongeza Awamu ya Nne, tangu ilipoanza kipindi hiki, tumeona kazi nzuri zilizofanywa na zinaendelea. Wapo baadhi yetu wanaoona kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne haijafanya chochote, lakini kuna usemi wa Kiswahili unaosema; mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Benki ya Wanawake imekuwa ni ndoto isiyomalizika. Tulipokuwa Dar es Salaam, tuliwahoji Mawaziri na Watendaji, tatizo lipo wapi? Tukakuta kwamba, Serikali mwezi huu wa

Juni unaomalizika, walihidi kutoa shilingi bilioni 2.1 ili benki hiyo ianzishwe, lakini hadi tarehe ya leo, taarifa niliyoipata ni kwamba, fedha zile hazijatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, chonde chonde, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulisimamie suala hili kwa sababu Bajeti ya 2008/2009 vilevile Serikali imepanga kuchangia kiasi fulani kwa ajili ya Benki ya Wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutawasemea sisi hawa; nani atawasemea? Wakijisemea wenyewe mnawacheka, mnawazomea; basi sisi ndiyo wa kuwasemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Inasikitisha, Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni muhimu sana, kwa sababu ni Wizara inayo-*deal* na wanawake, watoto na kadhalika, lakini imepangiwa fedha kama ifuatavyo:-

Fedha za Maendeleo tumepatiwa *only* 6.8 milioni, mishahara, pamoja na mambo mengine ni 7.8. Tuangalie Vyuo vyote vya Maendeleo ya Wananchi Vijijini na Wilayani, vipo chini ya Wizara hii. Inasikitisha, Kamati yetu chini ya Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Mhagama, tuliwahi kutembelea baadhi ya vyuo; ni vichafu, vibovu tena cha mfano kabisa ni Chuo cha Malya; utaona kinyaa, *kinehe* kuingia ndani. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini iwe hivi; Vyuo vya VETA vizuri, hela wanapewa nyingi; sasa kwa nini? Kwa kuwa vipo chini ya Maendeleo ya Jamii, basi vichukuliwe katika Wizara nyingine. Kama haiwezekani, Serikali kusaidia hela za kutosha, basi bora viondolewe. Kwa nini inapewa bajeti ndogo, halafu tunasema tunataka *fifty fifty*; kweli wataweza kuifikia kama tunawabana namna hii hawa? Hebu tuwapiganie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda katika *item* nyingine, hii Mheshimiwa Waziri Mkuu nataka unisikilize kwa makini na ninasema taratibu kabisa. Nawea nikalia hapa hapa juu ya *stage*. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Taratibu usilie Mheshimiwa.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Serikali yetu tunaielewa ni siku na Watendaji ni wazuri, lakini kuna jambo limepita miaka mingi sana, Kamati hii hii kabla hata hatujaingia awamu hii, ilikuwa ikitisemi kuhusu kiwanja cha Shirika la Taifa la Tija (*NIP*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa walimilikishwa Kiwanja Namba 906/S kilichopo Mbezi. Walianza kujenga hawa *NIP*, Shirika letu la Serikali, kwa heshima na taadhima, wakazungusha uzio. Bahati sijui sababu gani, Mheshimiwa Waziri Mkuu, atajua baadaye atakapofutilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanja kile mwaka 2002 walinyang'anywa *NIP*, wakapewa Taasisi moja ya India inaitwa *IMTU*. Hawa waliahidi kujenga hospitali, sijui ya aina gain? Si kitu tunakubali, lakini tathmini ambayo walipewa wakati ule wawafidie *NIP* ilikuwa ni fedha kidogo sana; waka-*appeal NIP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *appeal* yao haikufanikiwa, wakaambiwa wale *IMTU* walipe ziada. Tangu mwaka ule hadi leo hii, kwa ujeuri hawajalipwa hata senti tano, zaidi ya zile za mwanzo. Cha kusikitisha zaidi ni kwamba, kuna barua kadha wa kadha. Sijui ujeuri unatoka wapi, hata Katibu Mkuu anaandikiwa, tarehe ya barua nitaitaja, ngoja ni-*quote* hapa.

Ameisaini Katibu Mkuu wa Vijana, Ndugu Komba. Sio Komba huyu wa Bunge, alimwandikia Katibu Mkuu wa Ardhi, tarehe 2 Agosti, 2007 kuhusu lalamiko hilo. *Walahi*, nakula amini kwa Lugha ya Kiislamu, mpaka hii leo hata ile *acknowledge* ya barua ile haikufanywa. Halafu Mheshimiwa Hawa Ghasia, utapata kazi sana kuhusu Watendaji kama hawa. Isitoshe, Mwenyekiti wangu wa Kamati, ameisaini mwenyewe barua kuipeleka Wizara ya Ardhi na ulikuwepo *Kempinsk*, ulisikia maneno makali yaliyozungumzwa pale kwamba, baadhi ya Watendaji wanatudharau na tumeambiwa tuwe wakali, basi leo ninakuwa mkali.

Mwenyekiti wa Kamati ameandika barua tarehe 1 Desemba, 2007, barua hiyo hadi leo kwa ujeuri hajajibiwa mpaka. Mwenyekiti wa Kamati, ana uwezo mkubwa hakujibiwa. Isitoshe, Waziri Chiligati alipokuwa pale; Mungu akubariki, akuongoze na akupe cheo kuliko hicho; aliandika barua tena Wizara ya Ardhi, tangu tarehe 7 mwezi Desemba, hajajibiwa hadi hii leo. Sasa nilipokuwa katika Kamati, niliwaambia waliokuwepo pale wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwamba, kule Makunduchi zama ambazo kulikuwa hakuna barabara nzuri magari yalikuwa yanatoka saa nane za usiku. Sasa kuna bwana mmoja gari lilitoka saa nane, akaiba tenga la kuku, akalipeleka juu ya gari. Sasa usiku ndiyo kiza haoni, bahati mbaya njiani akateremka abiria mmoja na tenga la kuku likateremshwa. Alipofika safari yake yule aliyeeliiba ambaye ndiyo mwenyewe, akawa anauliza tenga langu la kuku liko wapi? Akajibu mwingine, akaambiwa bei uliyonunulia ndiyo utakayouzia. Kwa akina Mheshimiwa Abdisalaam huko. (*Makofi*)

Sasa mimi nilishangaa kwamba, Mheshimiwa Chiligati ameandika barua kupeleka Ardhi; sasa hivi yeye yupo Ardhi na leo ameandika barua. Leo Mheshimiwa Chiligati, bahati nzuri ameandika barua kumwandikia Waziri wa Elimu, lakini sasa jamani cha kusikitisha; Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili jambo ni la aibu kabisa. Haidhuru, Serikali iwe na mamlaka ya kumilikisha kwa mtu mwingine, lakini hizi barua zimekaa wapi na zinafanya nini, inahuzunisha? Ningekuwa na uwezo wa kusema ardhi ipasuke niingine, ningesema kwani ni aibu. Ujeuri wa Kamati ya Bunge, yenye uwezo si mdogo kwa Serikali, inasimamia barua zinaandikwa na Mwenyekiti hazijibowi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili nakuachia wewe.

Mimi sina tatizo na ofisi yako, wala sina tatizo na Wizara ya Ardhi, lakini nakuomba hili ulisimamie. Hapa nakumbuka Mwalimu Nyerere alimwambia Mzee

Mwinyi; unaweza kuwa kimya lakini wakati mwingine kuwa mkali kidogo. Nakuomba na wewe uwe mkali kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kero za Muungano, sina mengi. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, kutaka Serikali mbili hizi zikae pamoja, ziangalie kero ipi na ipi. Bahati nzuri, mwanzo ilikuwa baina ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi. Sasa hivi imeongezewa nguvu zaidi; na Makamu wa Rais. Sisi tunapongeza na ninaamini kwamba, kazi kubwa imefanywa lakini kuna baadhi ya mambo hayana haja kusubiri. Kama suala la Tume ya Pamoja ya Fedha, kuna *4.5 billion*, miaka mingapi nyuma, hebu tuamueni kuongeza kima na kama itakuwa Zanzibar imepewa zaidi, mtakata baadaye. Hizi fedha zinasaidia, hali ya uchumi ya Zanzibar imekufa, makontena sasa hivi hayaendi kule yanakuja Dar es Salaam na mengine yanakwenda Tanga, hakuna fedha inayoingia, karafuu hakuna hazitakiwi nje; sasa nchi ile itafanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, marafiki wawili wakipendana, hebu tuwe mfano kama mimi na Mheshimiwa Abdisalaam; tumeanza kupendana mimi na yeze tangu 63, sasa hivi chake changu na changu chake. Tupeane, huu ndio undugu. Mimi nasema Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna mambo mengine tunayopeana ni ya heri, hatupeani ya shari; kuna mambo mengine tusingoje mpaka Tume imalize au pande mbili zimalize ... (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Abdisalaam, anakukatalia Mheshimiwa Haroub.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya basi anitenge. Sasa kama hivyo ndivyo, barabara za Zanzibar zinataka bilioni ngapi? Mheshimiwa Karume atazipata wapi fedha zile zote za kujenga barabara? Barabara kidogo sana zile, hebu tujikurupushe safari hii tumwambie Mheshimiwa Karume, wewe kaa kando na barabara zako zote tutazijenga. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo binadamu hatutaki lazima tuambiwe. Mwisho, kama nitawahidi, nitazungumzia suala la kilimo. Nchi yetu ni nchi yenye rutuba, nchi kubwa, ina mvua za kutosha na ina maziwa ya kutosha. Cha kusikitisha, mwezi wa Januari, Februari, Machi, nilikuwa Muscut; Muscut wana jangwa tupu, mvua wanapata baada ya miaka mitatu, wanasafirisha kwenda nje kilo kumi za nyanya, kule ni sawasawa na shilingi 1,500 za Tanzania. Makabeji 15 kwa shilingi 1,500 ya Tanzania, ukii-convert. Wanasafirisha nje vitu hivyo, wana miujiza gani hawa?

Nakuomba sana Waziri wa Kilimo, hebu nenda Muscut na bahati nzuri sasa hivi Balozi yupo pale, Sheikh Hussein; kaonane naye, akupeleke kwa Waziri mwenzako wa Kilimo, akwambie miujiza gani wanaifanya? Jangwa lile, majabali, joto kubwa kama lile, kilimo kikubwa sana, wanasafirisha kila kitu pale! Mabiringanya hatoki mtu, nyanya, hakuna kilichokwuwa hakizalishwi, sisi hapa tuna neema zote, Serikali bado haijatia nguvu zake sana katika kilimo. Naamini kama Serikali itajiandaa vizuri katika kilimo, tutapiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umekwisha, naunga mkono hoja. Nawatakia kila la heri, lakini namwomba Waziri Mkuu, suala la *NIP* alizingatie na alishughulikie. (*Makofi*)

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupewa nafasi ili niweze kuchangia. Awali ya yote, naomba nitoe pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Pinda, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Pili, naomba nitoe pongezi sana kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa kwa ajili ya makadirio ya Ofisi yake, pamoja na wataalamu wake wote, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie na Mkoa wa Rukwa na hasa nijikite katika Miundombinu. Naomba niishukuru sana Serikali, kwa jitihada zake, pamoja na wafadhili ambapo tumefanikiwa kupata mamilioni ya dola kwa ajili ya kujenga barabara ya kutoka Tunduma hadi Sumbawanga, kwa kiwango cha lami. Ninaomba Serikali, kwa masharti waliiyopewa, ijitahidi kuhakikisha kwamba, inawalipa wale watu wote ambao wamepitia eneo la barabara na kwa hiyo kazi ianze mara moja. Vinginevyo, kama Serikali mtasuasua, ninyi ndio mtakuwa mnatuangusha watu wa Mkoa wa Rukwa. Tunalo daraja muhimu sana la eneo la Kaengesa, kwenye barabara hiyo kuu, daraja lile lisombwa na maji na kwa wakati huu magari hayapiti eneo hilo, yanazunguka eneo la mbali, lenye milima mingi na mabonde.

Kwa hiyo, tuliomba fedha ya dharura kupitia *TANROD*, ili tuweze kujenga angalau *barrier bridge*. Mpaka wakati huu, tangu tumeomba takriban kwenye miezi ya pili, ya tatu hivi, hatujapewa pesa hiyo. Tunaomba kwa heshima na taadhima, utusaidie pesa hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara mbili za Sumbawanga Mjini, ambazo zina lami na kwa zote mbili zina urefu wa kilometra kama tano hivi. Mwaka 2007, Serikali mlituletea kama shilingi 300,000,000, maana yake utatengeneza takriban kilometra moja tu. Tulipojaribu kutoa tenda wakandarasi wengi hawakuja, kwa sababu pesa ni chache ya kujenga hiyo kilometra moja. Atoe vyombo vyake Dar es Salaam alete kule Sumbawanga, kwa ajili ya kujenga kilometra moja, wanaona kwamba hasara ni kubwa. Kwa hiyo, tulichokuwa tunaiomba Serikali, mtupati fedha kwa mkupuo, angalau ya kujenga kilometra kama tano, sita hivi pale Sumbawanga. Msituletee kipindi kingine, kwa maana ya kufidia ili kazi iweze kutekelezeka. Hilo tulikuwa tunaliomba sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *Airport*, hatuna *Airport* na mtakumbuka Viongozi Wakuu kama wawili watakuwa ni mashahidi wangu; Mheshimiwa Malecela, alipokuwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Sumaye, alipokuwa Waziri Mkuu, ndege zilikuwa zinazama wakati wa masika wakija kule. Mtakumbuka wale wengine, mliuona Wabunge kule tulikuwa tunasaidia kusukuma ndege kuikwamua ni mambo ya aibu. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba mtusaidie sana kuhakikisha mnatuwekeea lami. Hatuna barabara ya kuaminika wala hatuna kiwanja cha kuaminika, hivi tukipata dharura tunafanyaje; reli yenewe haiaminiki, hivi Mkoa wa Rukwa tumewakosea nini? Tunaomba, sio mtusaidie ni haki yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa, hatuna bandari. Ziwa Tanganyika eneo la Tanzania, ndilo kubwa zaidi kuliko eneo la Burundi na eneo la Zambia, ambapo wana eneo dogo sana. Zambia ina bandari yake nzuri sana inaitwa Mpulungu. Maeneo ya Tanzania, bandari zake za ovyo ovyo kama ile ya Kasanga, Kipili, Korongwe, Kirando, Kabwe, Karema na hata ile ya Kigoma, hazifai kabisa. Ile Bandari ya Mpulungu pale ina uwezo wa ku-dock meli kama nne hivi na ina viwanda nya samaki na umeme. Sisi pale katika Mkoa wa Rukwa na hata Mkoa wa Kigoma, Serikali itutazame upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jimbo la Nkasi; kwanza, naomba nianze kumshukuru aliyekuwa Waziri Mkuu kipindi kilichopita, Mheshimiwa Edward Lowassa, ambaye alipopita katika ziara yake mwaka jana, alisisitiza kwamba, tutajitahidi kuhakikisha kwamba, umeme unakuja. Bahati nzuri, Waziri Mkuu wa sasa naye alikuwepo na suala hili pia lilikuwa linamkera kwa siku nyingi. Baada ya kuwa tumekuja hapa, nilikaa na Mheshimiwa Lowassa na wakati ule Mheshimiwa Karamagi, akiwa Waziri wa Nishati na Madini; wakaniweka kwenye utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba, umeme utaingia Nkasi. Nashukuru Waziri Mkuu aliyepo sasa, Mheshimiwa Pinda, baada ya kuingia madarakani naye ameyachukulia kidete na ameahidi umeme unakuja. Mheshimiwa Ngeleja, naye tayari amekwishanipa taarifa kwamba, umeme unaletwa kwa lazima, sasa ipo kwenye Programu yake. Kwa hiyo, ninaomba niishukuru sana Serikali kwa hilo, nasema asanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru vilevile kwamba, tuna chanzo cha maji ya uhakika eneo la Kate, lakini hatuna maji ya uhakika pale Namanyere, pesa inayotakiwa ni chache sana, kama bilioni tatu na nusu. Ninaiomba Serikali, itusaidie maji katika Wilaya. Ule Mpango mzuri wa Wizara ya Nishati na Madini kwamba, kila Wilaya itapewa umeme, tunaomba sasa na Wizara hii ya Maji nayo iweke mkakati wa kupeleka maji ya uhakika katika kila Wilaya. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba ule mradi kama ni wa kutega maji muweze kutusaidia pesa au kuchimba lambo kubwa eneo la Namanyere ili tuweze kupata maji ya bomba. Ninashukuru vilevile kwa mpango mzuri, ambapo barabara ya lami itapita katika Mji wa Namanyere. Ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niingie kwenye masuala ya Kitaifa. Kuna Kampuni ya *SPM Mgololo*, ambayo ipo Iringa; mengi yameongelewa na baadhi ya Wabunge kuhusiana na kampuni hii ya Mgololo. Kama madai haya ni ya kweli, basi ninaiomba Serikali, iweze kuchunguza suala hili haraka na kuleta taarifa Bungeni. Nasisitiza; na kuleta taarifa hapa Bungeni. Vinginevyo, natamka wazi kuwa, mimi Ponsiano Damiano Nyami, nitaleta Hoja Binafsi juu ya suala hili. Narudia, mimi Ponsiano Damiano Nyami, nitaleta Hoja Binafsi juu ya suala hili hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niingie suala la Makao Makuu Dodoma na hili kwangu ndio litakuwa la mwisho. Hivi ni kweli kwamba, Serikali mmeamua kuyahamishia Makao Makuu Dodoma; mnayo nia? Nasema hivi, pengine kuna ajenda ya siri; kwa nini nasema hivi? Miaka 35 imepita, Serikali haijaleta sheria rasmi ya kuutambua Mji wa Dodoma kuwa ni Makao Makuu. Miaka 35 imepita, Serikali

imekuwa haiipati *CDA* pesa ya kutosha kwa ajili ya upimaji wa viwanja, kwa ajili ya kuendeleza majengo mbalimbali ya Serikali. Uamuzi ulipotoka, hapa nina Sheria ya *CDA* Mamba 230 ya tarehe 12 Oktoba, 1973, ambayo inatokana na *Public Population Act* ya 1969, hii ni Sheria Namba 19 ya 1969. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vifungu vinavyotambua uhalali huo na vinasema hivi, naomba ninukuu: “Katika kufanikisha maandalizi ya shughuli za Serikali kwa kuhamishia Dodoma Makao Makuu, Mamlaka hii ilipewa Sheria ya Mamlaka kama ifuatavyo:-

1. Kutekeleza uamuzi wa kuhamishia Makao Makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda Dodoma.
2. Kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Dodoma kama Makao Makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutekeleza mipango hiyo kama ilivyopitishwa na Rais.
3. Kuishauri na kuisaidia Serikali katika mpango unaofaa katika kuhamisha Ofisi za Serikali kwenda Dodoma.
4. Kutokana na Agizo la Rais, kupata na kumiliki ardhi na mali nyingine zisizoweza kuhamishika.
5. Kutoa huduma yoyote inayohitajika kwa Wizara yoyote, Idara au Kitengo cha Serikali, Kampuni au watu binafsi ili kuhamishia Dodoma shughuli zao za biashara na watumishi katika mpango unaofaa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi leo Serikali haijafanya lolote. Nalipongeza Bunge, ninakipongeza Chama cha Mapinduzi, kwa kuona umuhimu wa kuhamia mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna maneno mbalimbali yanatoka hapa kwamba; viwanja havipimwi na kadhalika. Viwanja vitapimwa vipi kama *CDA* hawapewi pesa, ndio maana mnakuta wananchi wengine wanavamia maeneo wanakuwa wakorofi. Kwa mfano, wale wa maeneo ya Kata ya Tambuka Reli na Mlimwa, nimetembelea maeneo karibu mengi sana; wamevamia maeneo yale si kwamba wamevamia tu, viwanja walipewa na wengine walipewa maeneo ya Kisasa. Matokeo yake, wameuza viwanja vile wamehamia kule wameanza kujenga vibanda vya ajabu ajabu ili eti Serikali kupitia *CDA* ije iwalipe, mimi nasema hapana. Kuna malalamiko hapa kwamba, bomoa bomoa imekuwepo, napenda kuwapongeza wale wote waliofanya bomoa bomoa katika maeneo ya Chang’ombe juu, pamoja na Mtube.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza *RC* wa Mkoa huu, Mheshimiwa William Lukuvi, kwa kusimamia kikamilifu. Zoezi lile kwa taarifa yenu, lilifanyika kihalali, Mkuu wa Mkoa analifahamu, Mkuu wa Wilaya analifahamu, Kamati zote za Ulinzi na Usalama za Mkoa na Wilaya wanafahamu na lilisimamiwa kikamilifu. Tarehe

29 Mei, 2008 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri, Siku ya Alhamisi na Siku ya Jumamosi tarehe 30 Mei, 2008 kuanzia saa mbili na nusu hadi saa saba mchana na lilisimamiwa kikamilifu na Mkurugenzi wa Mipango wa *CDA*, akisaidiwa na SSP Mary Nzuki, huyu ni *OCD* wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha jioni hii kuwa hapa. Pili, nakushukuru wewe mwenyewe, kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu. Tatu, kwa niaba ya Wananchi wa Korogwe Vijijini, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na timu yake, kwa hotuba yake nzuri ilijoja maneno ya hekima na busara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nimeugawa katika sehemu kuu nne; barabara za vijijini, kilimo, umeme vijijini na madini. Nasisitiza vijijini kwa sababu Jimbo langu ni la Korogwe Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza, ningependa niongelee kuhusu Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunaishukuru Serikali kwa ujumla, kwa kuanzisha Programu Maalum ya Uendelezaji wa Masoko ya Mazao. Uendelezaji huu, umetuwezesha kutupatia barabara kwa sababu chini yake kuna kipengele cha matengenezo ya barabara na masoko pia. Nitoe shukrani za dhati kwamba, Korogwe tumepatiwa soko la kisasa la kwa ajili ya kuuzia mazao ya wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya pongezi hizo, lakini pia katika Hotuba ya Waziri Mkuu, Wananchi wa Korogwe Vijijini wamesononeka; hawakusikia lolote kuhusu Bonde la Mkomazi. Kulikuwa kuna mpango wa kujenga bwawa kubwa sana katika Kijiji cha Manga Mikocheni, kwa ajili ya unywesheaji wa Bonde hili la Mkomazi hadi Mazinde, Mombo mpaka Makuyuni, lakini hiki hakikuongelewa. Wananchi wa Korogwe, wangependa waelewe ni kwa nini Mradi huu wa siku nyingi hadi sasa hauongelewi. Hautekelezwi kwa sababu michoro na makisio yalikwishafanyika takriban miaka kumi iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye Sekta ya Kilimo kwa ujumla. Tukubali tusikubali, kilimo ndio tegemeo kubwa la kiuchumi katika nchi. Sekta ya Kilimo kama haikukua basi katika nchi hiyo uchumi pia utadorora. Nizungumze kwa masikitiko kidogo kwamba, katika miaka takriban 20 iliyopita, nchi hii imeongeza takriban asilimia nne tu katika kilimo. Hiki ni kiasi kidogo sana, hasa kwa sisi ambao tunategemea kilimo. Bila sekta hii kukua kwa haraka, Tanzania haiwezi kupunguza umaskini, kwani sote tunafahamu wazi kwamba, asilimia 80 ya Watanzania, maisha yao ni ya vijijini ambayo hutegemea kilimo. Wakati umefika sasa yale Mapinduzi tunayoyazungumzia ya Kilimo tuyashike, ili kufanikisha hilo, hatuna budi kuongeza bajeti yetu kwa upande wa kilimo na hatuna budi kukifanya kilimo kiwe cha kisasa na kibiasara zaidi, kwa maana ya kuachana na kile kilimo cha jembe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujaribu kuhimiza pia wawekezaji wakubwa wajiingize kwenye biashara ya kilimo, vilevile tuijingize sana kwenye viwanda ili mazao yetu tuweze kuyasindika wenyeewe badala ya kuuza kama malighafi, tuuze kitu ambacho kimeshasindikwa. Kilimo cha umwagiliaji, kipewe kipaumbele na pia kipewe kila aina ya msaada.

La mwisho kabisa, nadhani wakati wa kuzungumzia nadharia ya Benki ya Mkulima sasa umepita. Tufanye hilo kwa vitendo, sasa tuanzishe Benki za Wakulima. Wakulima wetu wasitegemee hizi benki za biashara, mkombozi mkubwa atakuwa ni Benki ya Wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niingie kidogo kwenye Sekta ya Barabara Vijijini. Kwanza, kwa niaba ya Wananchi wa Korogwe Vijijini, nataka pia niipongeze Serikali kwa kuanzisha ile Programu ya Uendelezaji wa Masoko ya Mazao, ambapo chini yake kuna kazi za matengenezo ya barabara za vijijini. Korogwe Vijijini tumefaidika sana na Programu hii kwani kuna matengenezo hivi sasa yanayoendelea katika barabara zetu mbili za Msambiazi - Lutindi - Kwa Bluu, yenye kilometra nane. Ya pili ni ya Makuyuni - Zege - Mpakani, yenye kilometra 22. Wananchi wa Kata ya Bungu wanashukuru sana kwa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nisisitize kwamba, maendeleo ya uchumi pia hutegemea mtandao mzuri wa barabara. Kwa hiyo, nchi yetu kwa kuliweka hili, kwa kweli hatuna budi kupongezwa. Upande wa vijijini, barabara ni kitu muhimu sana, tusiwhahimiza wakulima tu kwamba, waongeze mazao, lakini bila barabara watayafikisha vipi sokoni? Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali kwa kulifikiria hili la kuweka Progaramu hii ya Matengenezo ya Barabara chini ya Masoko ya Mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee kidogo kuhusu pesa zinazokwenda Serikali za Mitaa, kwa maana ya kutengeneza barabra. Utaona katika mwaka wa 2007/2008, Serikali ilitenga shilingi bilioni 67 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenyet urefu wa wastani wa kilometra 37,000. Hadi kufikia mwezi uliopita, ambao ndio tunakaribia mwisho wa mwaka huu wa fedha, kiasi cha shilingi milioni 48 kimeshatumika, kwa maana ya asilimia 72 ya fedha zimetumika. Kinachonikera zaidi katika pesa hizo ni kilometra 7,600 pekee ndio zimefanyiwa matengenezo kwa maana ya asilimia 20.

Sasa ukilinganisha hapa utaona hakuna uwiano, pesa iliyotumika ni asilimia 72, kazi iliyofanyika ni asilimia 20, hapa nimeshindwa kuelewa huu uwiano. Katika Programu ya Usafiri na Uchukuzi Vijijini, Serikali mwaka huu wa fedha imetenga shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya Halmashauri 22, lakini mwaka ujao wa fedha imetenga bilioni 1.8, ambazo ni pungufu. Sio tu pungufu, bali ni kwa ajili ya Halmashauri 55. Sasa hapa pia nashindwa kuelewa uwiano upo wapi? Hali hii kwa kweli ni vyema iangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije upande wa madini; Korogwe Vijijini tuna bahati ya kuwa na madini ya vito katika maeneo mbalimbali. Maeneo mengi haya kuna

wachimbaji wakubwa, kwa maana ya wawekezaji na wachimbaji wadogo pia. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, amezungumzia sana kwamba, yametengwa maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo lakini bahati mbaya katika zile sehemu alizozitaja yeye, Korogwe haimo. Hili naomba liangaliwe kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haya madini ya sehemu ya Kalalani na sehemu ya Kigwasi, kwa upande wa Korogwe Vijijini, napenda kwa niaba ya Wananchi wa Korogwe Vijijini, tumshukuru Mkoo wetu wa Mkoa. Matatizo pale yalikuwepo na bdo yapo; kuna mgogoro mkubwa wa mara kwa mara unaotokea kati ya wawekezaji na wachimbaji wadogo, lakini kwa kutumia busara zake, Mkoo wa Mkoa wetu ameunda Tume ya Kujaribu kuangalia ni nini kifanyike kuondoa tatizo lile. Bila shaka, katika muda mfupi taarifa hiyo aidha itakuja kwako Mheshimiwa Waziri Mkoo au itakwenda kwenye Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee kidogo kuhusu nishati kwa maana ya umeme. Hapa ningetilia mkazo zaidi upande wa vijijini. Mfuko wa Nishati ya Umeme Vijijini, ndio utakuwa mkombozi wa huduma hii kwa upande wa vijijini, lakini tunaiomba Serikali sasa isiishie kwenye makaratasii. Korogwe vijijini kuna maeneo mengi tu ambayo tumekwishafanyiwa kazi, nyumba nyingi zimeshafanyiwa *wiring* takriban miaka mitano, sita, iliyopita lakini hazijapatiwa huduma hii. Kila wakienda jibu ni kwamba, hakuna nguzo mara hakuna *transformer*.

Sasa tungeomba Serikali iliangularie hili. Kuna miji au kuna vijiji ambavyo viro tayari kabisa, hata michango imeshafanyika, kwa mfano, kwenye Kijiji cha Dindila, Kijiji cha Kelenge Kibaoni, Kijiji cha Lusanga na Kijiji cha Komasandu, vyote hivi nyumba zao zimejiweka tayari, zimeshakwisha fanyiwa *wiring* lakini cha kushangaza, inachukua muda kupatiwa umeme huu. Cha kuhuzunisha zaidi, shirika moja la kidini la Italy limejenga Kituo cha Afya kizuri sana katika Kata ya Mkalamo na wakatuletea vifaa mbalimbali ambavyo vinanahitaji umeme. Kwa hiyo, kituo kile kimekuwa kama ni pambo tu, tungeomba Serikali au tunaiomba Wizara husika, iliangularie hili kwa undani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa nigongewe kengele ya pili, naomba niishie kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hii hoja muhimu ya Hotuba ya Waziri Mkoo. Ninampongeza sana Waziri Mkoo, kwa kutoa hotuba nzuri na yenye matumaini. Pia nampongeza sana kwa kuwajali Madiwani. Madiwani siku nyingi walikuwa wanalia sana, sasa ninampongeza sana kwa kuona kilio chao na kuwajali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende mbele zaidi, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkoo, apeleke wahasibu kwenye Kata zote za nchi hii. Mheshimiwa Waziri Mkoo, pesa nyingi sana za Serikali zinapelekwa kwenye Kata na kwenye Vijiji, lakini kule hakuna wahasibu. Afisa Mtendaji siyo Mhasibu, anapokea pesa anatumia na anasimamia, lakini yeye siyo Mhasibu. Pesa ya Serikali ikishatoka Halmashauri, Mweka

Hazina akishasema pesa iende kijiji fulani ni kwamba, maana yake imetumika, hakuna anayefuatilia kule kwenye kijiji au kwenye Kata kwamba, pesa iliyopelekwa ya kujenga darasa imetumika vipi. Unapeleka shilingi milioni kumi lakini kwa sababu hakuna wahasibu, inaweza ikatumika shilingi milioni tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madarasa mengi yaliyojengwa ukisukuma ukuta unaanguka! Hebu fikiria Mheshimiwa Waziri Mkuu, kijiji kimoja kinatumia vibaya shilingi milioni tano, kuna vijiji zaidi ya 10,000 Tanzania nzima; shilingi milioni tano kwa vijiji 10,000 ni zaidi ya shilingi bilioni 50,000. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri Mkuu, apeleke wahasibu kwenye Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali zote Duniani, zinaendeshwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni. Serikali ya Tanzania vilevile inaendeshwa kwa mujibu wa Katiba. Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka kutokana na Wananchi. Vilevile kwa mujibu wa Katiba, Bunge ndio chombo cha Serikali ya Muungano, ambacho kina mamlaka ya kusimamia shughuli zote za Serikali, pamoja na vyombo vyake vyote. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri Mkuu, asimamie kwa kikamilifu, maamuzi yote yanayotokana na Bunge lako Tukufu ili yatekelezwe kwa wakati, kwa manufaa ya Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wote waliopo hapa Bungeni, wamekuja kwa kupitia vyama vyao na kila chama kinaendeshwa kwa mujibu wa Katiba na Kanuni. Kwa hiyo, Mbunge anaposema hapa Bungeni, analindwa na Kanuni za Bunge. Mbunge ye yote lazima aweze kuwa na mawazo yake binafsi na aweze kuyatoa hapa Bungeni, kwa maendeleo ya Watanzania wote. Mbunge lazima achukue mawazo ya wapiga kura wake, ayalete hapa Bungeni na ayaseme ili Serikali iweze kutekeleza. Mbunge lazima aweze kutetea nchi yake na aseme kwa maslahi ya Taifa lake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mbunge lazima afuate Kanuni za Chama chake. Ahadi za Chama cha Mapinduzi, ambazo kila Mbunge ameapa kuzilinda nitazitaja baadhi, ahadi mojawapo ni kwamba, nitaitumikia nchi yangu na watu wake wote. Ahadi nyingine inasema, rushwa ni adui wa haki, sitapokea wala kutoa rushwa. Ahadi za Viongozi na Wanachama wa Chama cha Mapinduzi; cheo ni dhamana, sitatumia cheo changu wala cha mwengine kwa manufaa yangu. Ahadi nyingine, nitasema kweli daima fitina kwangu mwiko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa Bungeni Waheshimiwa Wabunge, ukweli ni daima fitina mwiko. Waheshimiwa Wabunge, tukisimamia hilo, maisha bora ya kila Mtanzania yatapatikana na kutakuwa hakuna kunyoosheana vidole. CCM kamwe haitaficha maovu, CCM si mali ya mtu ni mali ya wanachama na inaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni na Katiba. CCM inahimiza Wanachama wake, wafanye kazi ili waweze kupata kipato na kila mtu atakula jasho lake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa, wizi na ubadhifru wa fedha za Serikali, imekuwa ni Wimbo wa Taifa. Kila kiongozi lazima akemee, kwa sababu Watanzania hawapendi. Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, wapo mstari wa mbele

kukemea dhuluma. Kwa hiyo, kazi yetu ni kuwaunga mkono, kama Wabunge wasipounga mkono vita hii; nani mwingine wa kuunga mkono?

Kwa hiyo, ninawaomba sana Wabunge, tuwe mstari wa mbele katika kumuunga mkono Mheshimiwa Rais na Serikali yake, kupiga vita ujisadi. Watanzania hawakuamini kwamba, pesa za *EPA* ziliibiwa mpaka pale Mheshimiwa Rais aliposema ni kweli shilingi bilioni 133 zimeibiwa na akasema atahakikisha zinarudi. Lazima tumuunge mkono, kuhakikisha kwamba zinarudi. Haiwezekani tukakaa kimya, amewapa vyombo vyake vitatoa taarifa, tusubiri taarifa na hatua zitakazochukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu hapa wanasema wanasauti zao kubwa, wengine wanasema wanapayuka, haki yao wapayuke, kama *microphone* zitapasuka Mheshimiwa Spika ataweka nyingine. Wenye kusema taratibu, waseme maneno wayapenyeze kama mwiba uwafikie wale ambao ni waovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Wabunge hapa wanasema sungura ni mdogo; siyo sungura ni tembo mkubwa Tanzania nzima. Tembo mkubwa wanakula wachache mpaka wanasaaza, ndovu ndio wanasema na tembo sawa sawa. Tanzania ni nchi nzuri, ina ardhi nzuri, tukilima tutapata maisha bora. Serikali itusaidie, Tanzania ina bandari tatu; Mtwara, Dar es Salaam na Tanga, hatuzitumii. Tanzania ina madini ya kila aina; almasi, dhahabu, *Tanzanite*, gesi, chuma, makaa ya mawe lakini tunaanza kulalamika bei ya mafuta imepanda.

Sawa, Mwarabu na mafuta yake na sisi na almasi zetu, dhahabu zetu, *Tanzanite* na kila kitu tunacho; tunachotakiwa wakipandisha na sisi tupandishe ili tufidie. Tunacho kila kitu, unataka Mungu atupe nini? Tunataka Wazungu waje watufanyie kazi; hawaji kutufanya kazi wanakuja kuchuma wanapeleka kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo suala la *Tanzanite*; mimi nilitembelea Miradi mwezi huu nikiwa na *Vice President* wa *World Bank*, nilichoona kule ni kwamba, hatuisimamii vizuri rasilimali yetu ya *Tanzanite*. Hakuna mtu anayesimamia kuona mwekezaji mkubwa yule anapochimba madini anapata kiasi gani na anapeleka wapi. La kusikitisha zaidi, nilikutu wale vijana wanaochambua *Tanzanite* kule, wanaingiza mikono yao kwenye boksi halafu wanafungwa kamba; kwa hiyo, mikono inacheza kwenye boksi hata kama akiwashwa hawezikuna, yaani mikono ile haiwezi kutoka kwenye boksi. Kama kweli uchambuzi wa *Tanzanite* ndivyo ulivyo, si jambo zuri kabisa. Halafu kila jioni wanapotoka, wanapigwa *x-ray* mwili mzima; sasa nadhani uchunguzi ufanyike, suala hili siyo zuri kiafya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hawaelewani na mwekezaji mkubwa yule, wanagombana kila siku mpaka vifo vinatokea lakini Serikali haijachukua hatua madhubuti ya kuwaokoa vijana wale. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba hebu nenda kule ukawafungue minyororo wale vijana ili waweze kupata maisha bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Jenerali Mstaafu Mboma, iliandika Ripoti, tunayo ililetwa Bungeni hapa. Walisema kwamba, Serikali itatue mgogoro wa mpaka

kati ya Kitalu B na C kwa njia ya uwazi na irejeshe mipaka iliyowekwa toka mwaka 1997 kwa kutumia ramani ya mwaka 1987 na kwa kuwashirikisha watu walioshiriki zoezi la upimaji mwaka 1987, hajafanyika hiyo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nikuombe yafuatayo; nakuomba upige marufuku ununuzi wa samani za Serikali kutoka nje. Tunayo misitu ya kutosha na wafanyakazi wa kutosha, lakini Serikali inanunua samani kutoka nje; inapeleka pesa za Watanzania China, Singapore, Malaysia na huku vijana wetu hawana kazi! Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba wakati unahitimisha hoja yako, upige marufuku uagizaji wa samani kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, madukani kumejaa bidhaa bandia, ambao zinapoletwa Serikali ikigundua kuwa ni bidhaa bandia wanaziharibu, lakini yule aliyeleta hachukuliwi hatua; hivi ile Sheria ya Uhujumu Uchumi imeenda wapi? Hao ni wahujumu uchumi, anakuletea *bulb* ambayo utawasha baada ya mwezi mmoja ukununue nyingine ambapo ile ungeiwasha mwaka mzima. Watanzania wote wakinunua *bulb* hizo ni hasara kiasi gani? Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba na hilo ulitupie macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ununuzi wa magari; Magari ya Serikali yanapaswa kununuliwa *in a central pool*. Unaponunua magari yote ya Serikali kwenye kiwanda, unapunguziwa nusu ya bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. MERYCE M. EMMANUEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya mpendwa wetu Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba moja kwa moja, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Waziri Mkuu, kwa hotuba yake iliyokuwa ikizungumzia marekebisho ya posho, usafiri, matibabu na mambo mengine kama hayo ya Madiwani. Nakumbuka mwanzo wa bajeti, Waheshimiwa Wabunge walikuwa wameshaanza kulalamika sana juu ya hili, japokuwa limekuwa likizungumzwa muda mrefu.

Nami pia ninaweza nikasema kwamba wakati nikiondoka kule Maswa, Madiwani waliniambia kwamba nitakapokuja hapa nizungumzie hili. Kwa hiyo, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri Mkuu, kwa marekebisho na maboresho makubwa sana ya maslahi ya Madiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mchango wangu unakwenda kwenye matatizo ambayo nina hakika, Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Serikali yake ya Chama cha Mapinduzi, kama watayachukua na kuyafanya kazi, nadhani yatawasaidia sana angalau kusafisha jina lao, pamoja na kwamba, sasa hivi limeshaharibika vibaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia jinsia ndani ya Kamati za Madiwani, Halmashauri ya Wilaya ya Maswa. Nasema jambo hili hapa ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwingine anaweza akajiuliza kwa nini asiliseme Maswa?

Hili suala nimelizungumzia Maswa zaidi ya mara nne au tano, lakini leo imebidi nililet hapa kwa sababu limeonekana limeshindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri, miaka mitano kuachia 2005, nilibahatika kupata nafasi ya Udiwani wa Viti Maalum ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Maswa. Nilichojifunza ndani ya Halmashauri hiyo kutoka kwa Mwenyekiti aliyeppita, alikuwa akichanganya wanawake kwa wanaume ndani ya Kamati zote za Halmashauri. Ninaskia uchungu mkubwa na ndio maana ninalileta hapa, mama yangu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Celina Kombani, ninakuomba ulichukue ulifanyie kazi; hili ni tatizo, tena Madiwani wako wa CCM ndio wanapata tabu kuliko watu wangu ambao ni wachache.

Mwenyekiti hataki kuweka wanawake ndani ya Kamati ya Mipango na Fedha. Kamati hii inakuwa na wanaume tisa na mwanamke mmoja, lakini ndani ya Halmashauri kuna wanawake saba. Sasa nikawa ninamuuliza Mwenyekiti, unazingatia nini kuweka wanawake wachache na wanaume wengi? Mwenyekiti hakupata la kuniambia, hata hivi sasa ninapoongea nadhani anakumbuka kwamba, nilimuuliza lakini hakupata la kuniambia. Nikamuuliza unataka kuniambia wanawake hatuna uwezo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikamuuliza kwamba, humu ndani wanaume ninaowaona kwenye Kamati yako ya Mipango na Fedha, mbona wengine hata uwezo tunawazidi? Mwenyekiti hakupata la kuniambia lakini nataka niseme kwamba, pamoja na maboresho yanayofanyika ndani ya Halmashauri, tumekwenda Halmashauri nydingi katika semina za maboresho mzima wa Shinyanga, tumekuta na Kamati nydingine zote. Ninawapongeza Wenyeviti, wanaojua utendaji wa kazi na maagizo ya Serikali ya kwamba, wanawake wanatakiwa wachanganywe ndani ya Kamati zote, hasa kiutendaji. Tukajikuta sisi Maswa ndio tuna mwanamke mmoja, ambaye ni wa Kamati ya Mipango na Fedha. Sasa hawa watu wakisafiri, yule mama kama yupo peke yake hata akibanwa kuharisha, hana mtu wa kwenda kumsaidia mle ndani ya chumba chake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi sipati picha, ninaomba nisaidiwe ni kwa sababu gani huyu Mwenyekiti anakuwa na jeuri na kiburi cha namna hii; je, ndivyo mlivyomuagiza ninyi Chama cha Mapinduzi kwamba, afanye hivyo ndani ya hiyo Halmashauri? Cha kushangaza, mbona Madiwani waliomo wengi ni wanawake wa Chama cha Mapinduzi! Pigeni basi makofi, maana nawawakilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, ninaomba suala hili lifanyiwe kazi, Madiwani hawana pa kusemea; kama mnavyoju, Mwenyekiti akishakuwa Mwenyekiti wa Halmashauri, basi naye amekuwa kigogo hataki kusemwa. Diwani anaogopa kusemwa, sasa leo nasema badala yao, suala hili kabla ya uchaguzi wa Kamati za Halmashauri mwezi wa saba, ninaomba apewe barua, aandikiwe kabisa kwamba, wanawake wana umuhimu ndani ya Kamati zote za Halmashauri, hususan Kamati ya Mipango na Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo, ninakumbuka mwaka jana wakati Waziri Mkuu wa sasa akiwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuna barua

niliipeleka ndani ya Ofisi yake, inayolalamikia juu ya Madiwani wanaotoka Upinzani, kutochanganywa kabisa, yaani hawatakii kunusa wala kuchungulia ndani ya Kamati ya Mipango ya Fedha. Ninachokikumbuka, Waziri alisimama hapa akasema tunashauri kwamba, lazima wachanganywe kwa sababu ya kuondoa mashaka na wasiwasi ndani ya Kamati hiyo kuwa peke yao. Nakumbuka alisema hicho kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka kumthibitishia kwamba, hajawahi kufanya kitu kama hicho, pamoja na kwamba, Waziri alitamka hapa akiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sasa ninachoshangaa ni kwa nini msimfute mtu wa namna hiyo, anaendelea kuwa na kiburi mpaka anakaidi? Mpaka leo ninavyoongea, sasa ni miaka mitatu imepita, hajawahi kuwekwa Diwani anayetoka Kambi ya Upinzani ndani ya Kamati ya Mipango na Fedha. Kipindi kile mimi nikiwa Diwani walikuwa wanawekwa ndani ya Kamati na yule alikuwa ni Mwenyekiti anayetoka Chama cha Mapinduzi; hao ndio tunaowahitaji ni waadilifu na wanajua maana ya uongozi. Yeye hataki kufanya hivyo, leo ni mwaka wa tatu, tuna miaka miwili iliyobaki.

Sasa mnataka kuniambia yule naye na mimi nimpigie magoti, nimnyenyekiee nimwambie kwamba, huyu ni Mwenyekiti? Si Mwenyekiti, wala hastahili kuwa Mwenyekiti, lakini badala yake anawadhalisheni ninyi. Naomba mchukue hatua ili muweze kufanya utekelezaji na hili libadilike kabisa. Hilo naomba mllichukue, mkalifanyie kazi, litaleta kizaa zaa; kura mtazikosa. Mimi huwa nasema, halafu baada ya siku chache mnaona majibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie suala la michango ya ujenzi wa shule. Sina tatizo na michango, viongozi waliojaliwa kufika Wilayani Maswa, rekodi yangu wanaijua; ninachanga vizuri sana michango ya shule. Ujenzi ninakubaliana nao, lakini ninachotaka kujua utaratibu wa hii michango ukoje? Mimi hata sielewi, kwa sababu kila mtu anapokuwa katika eneo lake, anapanga jinsi anavyojuu. Sasa leo ninaomba Waziri Mkuu, atakapokuwa anatoa majibu, ajaribu kutueleza utaratibu wa michango hii ukoje? Mfano, nimeenda Mkoa wa Kagera mwezi uliopita tu, nikaenda Wilaya ya Nkenge, Kata ya Ishozi, nikakuta hawa watu wanachanga michango, ndani ya ile nyumba kuna mume na mke wake. Mchango unasema kwamba, mama Sh.20,000 na baba Sh.20,000, lakini bado unasema matofali baba 20 na mama 20, mchanga kama ni nusu gunia basi nusu gunia mwanamke na nusu gunia mwanamume, mawe na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, naomba ninukuu Biblia inasema hivi, wasomaji wa Biblia: “Warumi 4:4, Mwana atamwacha baba yake ataambatana na mume wake nao watakuwa mwili mmoja.” Wewe unayechangisha baba na mama, wale ni mwili mmoja au unataka kuwatenganisha kisiasa? Kwa sababu kama baba amemuoa mama, wale ni kitu kimoja, kama ni Sh.20,000 basi baba ndio mtautaji na ndio kichwa cha mji achage. Sasa wanatafuta ujanja wa kuchanga Sh.20,000, Sh.20,000 hii siyo Sh.40,000; ina maana pale zinatakiwa Sh.20,000, zile Sh.20,000 ni za wizi, mafisadi wapo kule watafuteni jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwananchi anachangia mchanga, mawe, tofali, mwananchi anachangia Sh.20,000 baba na Sh.20,000 mama; hebu piga hesabu ya haraka

haraka, wezi si wapo kule chini na mnawaacha wanafanya hiyo kazi? Haiwezekani, mji mmoja hauwezi ukatoka, yule baba kama ana wake watatu, basi wanawake wote wawili wanatakiwa wachange, sasa ndugu zangu wale ambao lazima waoe wake wawili watafanya nini? Tatizo hili nimeliona kwa macho na nina uhakika, sisemi kitu cha kubahatisha, hata ukitaka nikupeleke nitakupeleka na nitakuonyesha risiti zipo. Si utaratibu wa Wizara ya Elimu, wanataka kuwafanya watu washindwe kuchangia na haya ninayoyasema, msipofuatalia zile zahanati zile nyingi mnazotaka kumwaga kama nyasi, hazitatekelezeka vizuri.

Kwa hiyo, ninaomba msaidie hao wananchi, sijajua maeneo mengine lakini nasema pale nilipofika nikawaona, mama achange Sh.20,000, baba akichanga mama anatiwa kibano, anakimbia asubuhi asubuhi ameshaondoka nyumbani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoke hapo nihamie kwenye michango shule. Shule za Serikali wanasema ada Shule za Kata ni Sh.20,000, lakini ukiangalia michango inayofuata baada ya ada, nataka nikuhakikishie ni zaidi ya Sh.200,000. Naomba hapo mjaribu kuangalia; yule mtoto asipokwenda na nusu ya mchango, ambayo ni zaidi ya Sh.100,000, ina maana haingii darasani. Sasa hii isije ikawa danganya toto.

Ninachotaka kusema, inawezekana ni walimu walioko kule au watu walioko katika maeneo husika, michango inakuwa ni mingi. Mbunge mmoja jana alipochangia alisema, siwezi kurudia, michango ni mingi, unakuta ile Sh.20,000 haina maana. Naomba msaidie watoto, kwa sababu wengine wanashindwa kuingia shule kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haraka haraka nitasema kwamba, wakati nakwenda kule Nkenge, nilipita mjini pale Kituo cha Polisi, nikakuta baisedeli zimepaki nyingine zimeshapata kutu zimeharibika, nikauliza je, jana kulikuwa na msako wa majambazi? Wakaniambia hapana, hizi baisedeli zina zaidi ya mwaka mzima; kulikoni? Eti wanasema walikuwa sijui wanafanya biashara mjini kwa hiyo zimekamatwa zipo kituoni. Sawa walizikamata sikatai, lakini ni kwa sababu gani zina mwaka mzima zipo pale; hakuna kesi, hawajapelekwa mahakamani na hakuna kinachoendelea baisedeli zimeegeshwa? Wapeni baisedeli zao, haiwezekani peleka utitiri wote mahakamani, ijulikane wanafanya nini, maisha bora kwa kila Mtanzania kwa kuegesha baisedeli kituoni wala hayataonekana mpaka kesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia habari za usalama wa raia; hawa matrafiki waliosimama wote barabarani sijajua wanafanya kitu gani? Bahati nzuri ninapenda sana kupanda mabasi, Waheshimiwa Wabunge wakati mwingine acheni kupanda magari yenu pandeni mabasi, muone kinachofanyika barabarani. Watu wanapakiwa ndani ya basi kwa wingi, yaani wanapakiwa kiasi kwamba wakifika hata Singida, wengine wanashushwa wanasubiri magari mengine yanayokuja nyuma. Hali ni mbaya kupita maelezo, lakini cha kushangaza yaani kila mnapofika alipo trafiki, anasimamisha gari anaongea na dereva kule mbele. Wanachoongea siwezi kuzungumza chochote, sijui wanosalimiana, lakini akimaliza basi linapita.

Ninaloliongea hili nimeliona kwa macho na ni zaidi ya mara nne. Kwa hiyo, ninaomba mjaribu kufuatilia barabarani, mabasi yanapakia watu wengi, matrafiki wanajipanga kama kawaida, lakini hakuna kinachoonekana, abiria wanahangaika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili ulichukue, lakini unajua nimesema haraka haraka kiasi kwamba, ninapata shaka kwamba, hoja zangu zinakaribia kukosa nafasi, haziwezi kwisha hata nikipewa dakika 40. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea suala la Elimu ya Sekondari. Tuna malengo mazuri sana ya kuwasaidia watoto wetu, lakini kusema kweli tatizo linalojitokeza ambalo linajaribu kufanyiwa marekebisho ni kuhusu suala la walimu. Sizungumzii kwamba walimu ni wachache au nini, ninachotaka kusema, hawa walimu jamani madai yao ya likizo na matibabu kila siku wanasema yamepunguzwa, yanarekebishiwa, sijui vitu gani, hawapati kabisa. Mnachonishangaza, kila siku huwa ninasema ikifika 2009 jamani Watanzania mnisikilize, marekebisho yote walimu wanafanyiwa, nashangaa hivi wao huwa hawaelewi kwamba, wanadanganywa? Haiwezekani ukaacha kurebishiwa kutoka mwaka wa kwanza, wa pili, wa tatu na wa nne mpaka wa tano ndio wanakurekebishiwa! Kwa hiyo, hili ninaweza nikasema ni makusudi na nina hakika Waziri ana uwezo wa kulitatua na niliposema hivi limemuwasha masikioni na ninajua atalifanya kazi; asipolifanya kazi 2010 teke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua baada ya muda mchache, kengele itagongwa lakini nataka kusema kwamba, ninakushukuru kwanza, nimeponea chupu chupu kupata hii nafasi. Kimsingi nataka niwaambie, sisi kama Wapinzani, tunachokisema hapa tunatetea maslahi ya Wananchi wote. Tunaposimama hapa, hatumchukii mtum tunafanya marekebisho. Isifikie mahali kwa kweli tunaposimama, mtu anamwona fulani yule anakisema chama, mimi sikisemi chama.

Heleni yangu imedondoka! (*Kicheko*)

Mheshimiwa mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Dr. Zainab Gama ili atumalizie kwa leo.

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nilishakata tamaa, umeniokoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia kwa kumshukuru Waziri Mkuu, kwa kufikiria kutupa pesa ili kuiendeleza Hospitali ya Tumbi. Sote tunajua kwamba, Hospitali ya Tumbi inapokea asilimia 30 ya majeruhi wa nchi hii. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuona katika bajeti isipokuwa nimeambiwa kwamba, ile Barabara ya Mkoani angalau imepangiwa shilingi milioni 300; kama hivyo ndivyo, nashukuru sana. Nimeambiwa na Mkurugenzi wangu, nilikuwa namuuliza na imesemwa kwenye RCC, naamini hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa pili nilikuwa nazunguka kwenye jimbo langu, nilionana na Viongozi wa Serikali za Mitaa. Nikiwa huko, niligundua sikuwa na wataalam kutoka Halmashauri, nilipouliza nikaambiwa wanaandaa bajeti, nikatafuta ajenga kama bajeti ni shirikishi?

Nilipozunguka, ukiacha Kata moja tu ya Kibaha, lakini Kata zote zilikuwa hazijapeleka mapendekezo yao kwenye Halmashauri. Nyingine mapendekezo yapo kwenye mitaa yao na nyininge kwenye Kata. Sasa nikauliza; inakuwaje hawa Watendaji wanapata mapendekezo kutoka kwa nani au ya kwao wenywewe? Nikaambiwa waliitwa huku Dodoma; Mkurugenzi wangu na Mwenyekiti wakaambiwa, bajeti haraka haraka. Sasa nilikwenda katika Kata ya Machocho, ambayo Mwenyekiti anatoka katika Kata hiyo, nikaomba nililingize hilo kuwauliza na wao wakasema bado hawajapeleka hata *RCC* haijaka.

Baadaye nikiwa nazunguka pale Ofisi ya Bunge ya Dar es Salaam, nikaona Watendaji wengi wa Halmashauri wanakuja kufanya utaratibu wa kutazama bajeti kidogo wanataka wapunguze. Wakati huo hata *RCC* ya Mkoa wa Pwani haijaka, wakasema wanapunguza *sealing*. Sasa nikasema huu utaratibu unakuwaje; kutoka kule chini si inaingia Wilayani, inakuja Mkoani, inakwenda Taifani; ilikuwaje tena inaishia Taifani inafikia *sealing* halafu ndiyo inakuja kwenye *RCC*? Nina mashaka, ninaomba jamani tuwe *serious* katika kuwashirikisha wananchi kwenye bajeti, tutapata malalamiko mengi ya bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nitazungumza na nitarudia tena; Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumza vizuri sana kuhusu suala la ardhi kuanzia ukurasa wa 36 mpaka 40. Mimi nasema, yakitekelezwa hayana mgogoro, lakini hayatekelezwi Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa ile ahadi yako ya mwisho kwenye ukurasa wa 40 ya kusema umeagiza Halmashauri zipange bajeti na ufuatilie; hivi sasa umesema ardhi ikitumika na kugawanywa bila utaratibu ni chanzo cha mgogoro.

Sasa hivi Jimboni kwangu kwenye Mtaa wa Sofu, kuna mgogoro mkubwa umefikia hatua wananchi wamepelekwa Polisi, wamesema wapo tayari hata Polisi wawapige risasi mpaka wafe, lakini hawawezi kukubali. Wanasema wamedhulumiwa na hiyo fidia waliyopewa haistahili. Mgogoro ule umepelekwa kwenye Halmashauri, umepelekwa Mkoani na mpaka kwa Waziri. Walifikia hatua ya wanakwenda Mahakamani, mimi Mbunge ninaomba niingilie na nimeanza tena upya.

Halmashauri imekutana na wananchi; wananchi wale wanazo sheria, mpaka *Hansard* za Bunge za Magufuli wanazo na mpaka Magufuli alipokwenda Kiluvya kwenye mgogoro; wanawauliza wataalam wangu wanashindwa kujibu. Nashindwa kujibu kwa sababu si mtaalam. Tumekwenda Mkuu wa Mkoa akapata hii habari, maana niliambiwa na Naibu Waziri kwamba, peleka kwa Mkuu wa Mkoa; Mkuu wa Mkoa akapata habari akamwagizia *DC* aende. Bahati mbaya, siku hiyo *DC* alikuwa na kazi,

ikabidi nikurudi na wataalam; Mkurugenzi na Madiwani. Tulifika pale hatukupata jibu. Maafisa Ardhi, wanashambuliwa kwa aibu; huyu hapa kampelekea Mhindi na huyu kamletea fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri aliyejekuwe po mwanzo wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, aliniambia niandike barua; nimeandika nimeipeleka lakini hakuna kitu kinachofanyika mpaka nimepeleka ombi langu Wizara ya Ardhi. Kwa nini tuendeleze kwa mgogoro? Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, umtume Waziri wako twende mimi na yeye, nisingependa kuinuka na ninashukuru sana kwa leo kunipa nafasi, kwa sababu nilitaka nishike shilingi kwa hili.

Naomba Waziri twende mimi na yeye ili wale Wananchi wakamwone; wananyanyasika na wametoa mpaka ushahidi wa Maafisa Ardhi walipogawa na pesa walizokula ovyo. Sasa naomba hili msilichukulie kwa utani, kwani kesho na keshokutwa watu watauwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu kasema vizuri kuhusu suala zima la wananchi wanaovamia maeneo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, analijua hili ninalotaka kulisema, Waziri wake wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa analijua na mpaka mimi nimeandikwa vibaya kwenye magazeti; eti Dr. Gama amekwenda kuweka alama za X, kwa sababu ya hujuma ya mwananchi ambaye analindwa na Maafisa wa Ardhi.

Mwananchi huyo ni ngumbaru na wanaojua neno ngumbaru mnalijua, hana cheo chochote katika Serikali, kwenye chama kafanya fojali, kagawa zaidi ya viwanja 50 bila Halmashauri kupata hata senti tano, anaweka mguu anapima, nimesema hapa. Mwanasheria aliyejekuwa mzuri alilichukua hili jambo akalifuatilia tumekwenda Mahakamani. Mwanasheria huyu, siku hizi kachukuliwa yupo Makao Makuu na kesi zimesimama. Haiwezekani, mtu anafika wanamuwekeea X anapangusa, anakwenda wanamwambia demolition anasema go to hell, lakini hakuna hatua inayochukuliwa. Sasa hivi nimemsikia mtu anazungumzia hatua iliyochukuliwa hapa Dodoma, walikwenda kuvunjiwa akampungeza mpaka Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwaje Kibaha? Imefikia hatua mpaka wanatumia jina la Mkuu wangu wa Mkoa, ambaye yupo *innocent* kabisa kwamba tunajenga kwa sababu mimi ni ndugu yake Mkuu wa Mkoa. Nimemweleza lakini hakuna hatua iliyochukuliwa, kulikoni? Je, kuna hujuma humu ndani au Wizara inahusika? Nimesema katika Bunge la Bajeti la 2007/2008, niki-refer Bajeti ya 2006/2007, hakuna hatua inayochukuliwa mpaka wanataka kuniharibia mimi sifa yangu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu; kulikoni; je, kuna siri gani au hamumtaki Dr. Gama katika Jimbo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza kwa uchungu sana.

Baada ya kusema hivyo, Ahadi za Rais; inatia aibu, Rais amekuja anauliza kwa nini huu Mji wa Kibaha kwanza ni mdogo kwa nini usiendelee? Rais anashangaa; mimi je na mwananchi wangu wa kawaida; kulikoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Rais ana nia nzuri kabisa, Watendaji wako wanakuangusha, wameshazoea miji ikiwa inaanza inakuwa shagalabaghala katika *shanty town*, hawakuzoea kuipanga. Umesema kuna Tume ya Mipango ya Kutumia Ardhi; je, Tume hii inafanya kazi gani na kwa nini isiwe na ofisi hata mpaka Wilayani iwasaidie Maafisa wetu, wanashindwa inawezekana elimu zao ni ndogo au walishazoea masuala ya rushwa? Mimi naomba unisaidie sana hili linaniuma, imefikia hatua mpaka watu wananielewa vibaya, wanafikiri nina *interest. Interest* yangu, niliahidi nikipata Jimbo; kwanza, nitahakikisha Mji huu wa Kibaha hauanzishwi kiholelaholela, utapangwa.

Mheshimiwa Waziri Mkoo, nimekuletea barua wameshindwa kuanda, mimi nimetafuta Mtaalam, nimechukua pesa yangu mwenyewe. Nimeshirikiana na Halmashauri tumepitisha, nikaleta mpango ule ambao umezungumzia katika bajeti yako, lakini cha kusikitisha mpaka leo, nimeambiwa hela hakuna. Hivi sasa mji ule watu wa Dar es Salaam wanakuja tu kuchukua mashamba. Sheria inasema wasichukue mashamba, lakini mpaka mwaka jana waligawiwa mashamba. Wenyeviti wangu wa Serikali za Mitaa, wanarubuniwa na Maafisa wa Ardhi; *Town Planner* amefikia hatua hata ya kuuza kiwanja kwa shilingi milioni mbili.

Juzi juzi walimchuza Banduka, wakataka kumchuza na dada yangu hapa Mkoo wa Mkoa, kwa kutaka kuvamia ule msitu uliomwagiwa maji. Miti imemwagiwa maji na wananchi. Rais wetu Kikwete akasema ni marufuku, matokeo yake wakataka kwenda kumwambia kwa nini atukatalie?

Nashukuru Mkoo wangu wa Mkoa akasema bwana, hakuna. Eneo ambalo nimewaelekeza walitaka walifiche wawape watu, lakini nimesema bwana hao mmewapa viwanja katika msitu pelekeni eneo lile. Sasa naomba hao Wataalam wako waje tuzungumze nao na ninamwomba Waziri aje tuzungumze, kwenye hili sina mzaha nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari la zimamoto hatulioni mpaka leo. Gari la zimamoto halionekani, nyumba ya zimamoto imejengwa, watu wanapewa posho kila siku gari lipo wapi? Taarifa siyo nzuri, najua lile gari hela zilitaka kuibiwa; Mama Gama nimepiga kelele hapa hela zikanunua gari na gari lenyewe bodi nzima injini mbovu. Sasa naomba ulifuatilie. (*Makofi*)

Ninyi mnalalamika jamani umeme umeme; Kibaha kuna mitaa mingine pale hii *highway* haina umeme. Tumekwenda kuomba tukaambiwa *TANESCO* haina pesa, mkitaka changeni wenyewe. Nashangaa katika bajeti, inasemekana kuna maeneo wamebekewa mgao wa pesa; je, Kibaha ina matatizo gani jamani. Kibaha ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani; je, kuna Makao Makuu gani yenye kufanana na Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani? Makao Makuu haina barabara!

Waziri Mkuu wa zamani alisema, jamani Makao Makuu porini; kweli tuna nia au tulikuwa tunawadanganya Wananchi wa Kibaha? Mimi hilo nataka nisaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekit, namalizia kwa kusema kwamba, elimu ya watu wazima hii ya kuchukua mwaka mmoja *form one-two*, mwaka wa pili *form three-four*; wananchi wengi walishindwa kuendelea, hawana pesa. Leo unamwambia ili aweze kuendelea, achangie tena hiyo elimu ya watu wazima shilingi 235,000 kwa mwaka ule wa kwanza, mwaka wa pili zaidi ya Sh. 240,000; ataweba huyu?

Nashukuru nimemwambia Waziri, amesema atalifanyia kazi na yeye alikuwa halijui, watabaki walewale wenye uwezo, ndiyo watakaosoma sekondari. Basi nakuombeni leo nimezungumza *politely*, lakini kweli kabisa niliamua kama nisingepata nafasi ningeshika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, huyo alikuwa ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa usiku wa leo. Kwa hiyo, kesho nadhani ndiyo tutakuwa tunaanza kuhitimisha Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa vile hakutakuwa na mchangiaji isipokuwa atakuwa akijibu hoja zilizochangiwa tangu Jumatatu.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kulahirisha Bunge hivi sasa mpaka kesho saa tatu barabara asubuhi.

(*Saa 01.45 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 27 Juni, 2008 Saa Tatu Asubuhi*)

